

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Nane - Tarehe 16 Juni, 2005

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatavyo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka 2005/2006.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 70

Namna ya Kumuenzi Baba wa Taifa

MHE MBARUK K. MWANDORO (k.n.y. MHE. ELIACHIM J. SIMPASA)
aliuliza:-

Kwa kuwa utumishi wa Hayati Mwalimu J. K. Nyerere hauna mfano katika taifa letu, Afrika na Ulimwenguni kote na kwa kuwa, njia mojawapo ya kuwaenzi watu wenye sifa kama hizo ni kuhakikisha kuwa majina yao yanawekwa kwenye kumbukumbu za vitu vikubwa ili majina yao yaendeleo kukumbukwa:-

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kubadilisha jina la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Dar es Salaam kuwa Uwanja wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere (*Nyerere International Airport*) au Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwa , *The Mwalimu Nyerere University* ili jina hili liendeleo kutajwa kwenye Taasisi kubwa kama hizo kuliko kulumia jina hili kwa vitu vidogo vidogo ambavyo havijulikani sana Kimataifa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Simpasa kuwa utumishi Hayati J. K. Nyerere hauna mfano katika Taifa letu, Afrika na Ulimwenguni kote na kuwa moja ya njia nzuri za kuenzi watu wenye sifa kama za Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume, ni kutumia majina yao kwenye kumbukumbu za vitu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu ya msingi wakati nikijibu swali Na. 259 la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, na sehemu (a) ya swali Na. 3777 la Mheshimiwa Simpasa, ambalo analiuliza mara ya pili, kuwa kutunza kumbukumbu za nchi na hususan za Viongozi Wakuu Waasisi wa Taifa, ni jambo la msingi na tayari sheria kuhusu kuwaenzi Viongozi Wakuu Waasisi wa Taifa Na. 18 ya Mwaka 2004 inayoitwa, *The Founders of the Nation (Honouring Procedure) Act* iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Novemba 2004 imeanza kutumika kuanzia tarehe 1 Machi, 2005.

Mheshimiwa Spika, sheria hii imeeleza utaratibu wa kufuata katika utumiaji wa jina au majina ya waasisi hawa na kuzuia utumiaji holela wa majina yao yasiyoendana na hadhi zao. Hivyo basi, mtu au Taasisi yoyote itakayohitaji kutumia jina la waasisi hao wa taifa, haina budi kuzingatia utaratibu unaoelekezwa na sheria hii ikiwa ni pamoja na kuomba kibali kwa Waziri mwenye dhamana ya jambo hili. Aidha ufafanuzi zaidi kuhusu utaratibu wa kufuata katika kuwasilisha maombi au mapendekezo ya matumizi ya majina utaelezwa katika Kanuni ambazo zinakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapendekezo ya kumuenzi Baba wa Taifa yaliyotolewa na Mheshimiwa Simpasa, Wizara na Taasisi husika katika kutimiza azma hiyo zimechukua jitihada za awali. Ni mategemeo yetu kuwa wahusika ambao ni sekta ya

uchukuzi na elimu sawia watazingatia ushauri huo wakati wanatafakari namna ya kumuenzi Baba wa Taifa na Ofisi yangu itatoa ushirikiano wake. (*Makofi*)

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba sifa za Mwalimu J.K. Nyerere zinaeleweka na nashukuru kwamba Waziri anakubali kwamba suala hili linaweza kufanyika. Sasa kuna haja gani ya kupindapinda au kuweka konakona wakati Mwalimu J.K. Nyerere anajulikana na watu wakiingia wanatakiwa wafahamu kwamba wameingia kwa Mwalimu Nyerere kwa nini tusikubali badala ya kupindapinda hiki kikaenda moja kwa moja? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba kuwaenzi waasisi hawa si jambo la Mjadala wala kupinga, isipokuwa katika nchi yoyote ni vizuri kufuata taratibu na nimeeleza waziwazi wale wanaohusika wameanza jitihada za awali na ni mategemeo yangu kwamba siku moja uwanja huo utapewa jina la Hayati Baba wa Taifa. (*Makofi*)

Na. 71

Vibali vya Kuajiri Watumishi

MHE. ARIDI M. ULEDI aliuliza:-

Kwa kuwa miaka ya hivi karibuni Halmashauri na wananchi wa Wilaya ya Masasi wamehamasika kuongeza idadi ya shule, zahanati, vituo vya afya na hospitali kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, lakini huduma zote hizo hazina Watumishi kulingana na ikama zao na kwa kuwa majibu yanayotolewa na Wilaya juu ya upungufu huo wa Watumishi ni kule kukosekana kwa vibali vya kuajiri kutoka Utumishi Makao Makuu.

- (a) Je, Serikali haioni kukosekana kwa watumishi kwenye huduma hizo kunawanyima wananchi huduma bora?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa hali hiyo inawavunja moyo wananchi kuendelea kujenga miradi mingine kama hiyo kwa mujibu wa Ilani ya CCM?
- (c) Je, Wilaya italimaliza lini tatizo la watumishi Wilayani Masasi kwa kuhakikisha vibali vinavyohitajika vinatolewa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Aridi M. Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, napenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kutekeleza azma ya Serikali ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa raia wake, kipaumbele kimetolewa katika upanuzi wa huduma za jamii hususan sekta ya elimu na afya, kama sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000. Aidha vibali vya ajira hutolewa kutokana na vipaumbele vya sekta kwa kuzingatia mipango ya muda wa kati wa matumizi ya Serikali, mwajiri kuwa na nafasi iliyoombwa na iliyoidhinishiwa ikama na uwezo wa Bajeti wa kulipa mshahara. Sambamba na vigezo hivyo kipaumbele katika Bajeti ya Serikali, kimetolewa katika kuajiri wataalam wa afya na elimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Serikali za Mitaa ndiyo watoaji wakubwa wa huduma za jamii katika Wilaya mbalimbali. Kukosekana kwa wataalamu katika sekta tajwa kunatokana na Serikali kushindwa kupata watumishi inaowahitaji kutoka katika soko ambalo kwa sasa ni huria na limetawaliwa na uhaba mkubwa wa wataalamu wa sekta ya afya. Kwa kutambua umuhimu wa huduma za afya, Serikali iliamua kulegeza masharti ya utaratibu wa kuajiri watumishi wa sekta ya afya na elimu kwa kuwapangia vituo vya kazi moja kwa moja wanapomaliza masomo yao. (*Makofi*)
- (b) Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua zilizokwishachukuliwa kuimarisha sekta ya afya na sekta nyinginezo, bado kuna tatizo la kuwapata wataalam kufanyakazi hususan maeneo ya pembezoni. Hili ni tatizo kubwa ambapo pamoja na watumishi wachache waliopo kuelemea na kazi, upungufu huo huambatana na taaluma duni kwa baadhi ya watumishi, hali hii hupelekea mikakati ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini kutofikiwa. Ili kutatua tatizo hili, Wizara ya Afya na Halmashauri zinashauriwa kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuwapatia vivutio watumishi wanaopangwa sehemu za pembezoni ikiwa ni pamoja na kuwahudumia vizuri na kwenda Mijini wakati wanapotaka kuajiri watumishi wapya.
- (c) Mheshimiwa Spika, ili kupambana na tatizo hilo napenda kutoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na Wizara ya Afya, kutumia fursa iliyopo kuwapata Madaktari, Madaktari Wasaidizi, wafamasia na tabibu wote wanaomaliza masomo, bila kuzingatia utaratibu wa ushindani. Ofisi yangu inatarajia vile vile kwamba waajiri wote zikiwemo Halmashauri za Wilaya watachukua fursa hiyo, kuwapata wataalam wa afya wanaowahitaji ili kuimarisha sekta ya afya vijijini. Wakati huo Serikali ikiongeza watakaohitimu. (*Makofi*)

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

- (a) Kwa kuwa tatizo la Masasi siyo kupatikana kwa wataalam ni kupatikana kwa vibali ili Halmashauri iweze kuajiri Wafanyakazi wanaohitajika. Je, Serikali itakuwa tayari kutoa vibali hivyo ili Halmashauri ya Wilaya ya Masasi iweze kuajiri watumishi inaowahitaji? (*Makofi*)
- (b) Kwa kuwa hivi sasa kuna vyo vingi vya watu binafsi ambavyo vinafundisha taaluma hizo za huduma za afya. Je, Serikali iko tayari sasa kuvitambua vikundi hivyo na wafanyakazi hawa ambao wanajifunza kwenye Taasisi binafsi ili nao wachukuliwe kuhudumia kwenye zahanati, vituo vya afya na shule zetu? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aridi Uledi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi Ofisi ya Rais, Utumishi, imetoa kibali cha jumla kwa Halmashauri na waajiri wengine wote kuwaajiri wafanyakazi katika sekta ya afya na hata sekta elimu kwa kutambua kwamba sekta hizo ni muhimu sana katika kuondoa umaskini na kuondoa kero za wananchi. Kwa hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, inapaswa kuona kwamba mwanzo wa mwaka ina ikama inayohitajika ili iweze kuajiri na vile vile ihakikishe kama ina Bajeti ya kuwalipa wale itakaowajiri kwa sababu haitakuwa na maana kumwajiri daktari kama hakuna fedha za kumlipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu ya pili ya swali kama ninavyofahamu kwa mfano Hospitali ya Marehemu Dr. Kairuki imekubaliwa hata wanafunzi wanaolipiwa na Serikali kupata mafunzo ya udaktari kule. Huko ni njia ya kuonyesha nia ya Serikali ya kutambua sekta binafsi katika kuleta kwa haraka maendeleo ya wananchi. Lakini ninatambua kwamba kuna utaratibu wa kuweza kutambua vyo hivi na hiyo itakuwa ni jukumu ya Wizara ya Afya na wale wenye vyo hivyo wafuate taratibu. Nina hakika Serikali haitasita kutambua kama vigezo vyote vinavyotakiwa vimefikiwa. (*Makofi*)

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kuuliza kwamba kwa hivi sasa kumezuka matatizo hasa katika watumishi wanaopangwa Wizara ya Afya na Elimu, mara kwa mara huwa hawafiki katika maeneo haya hasa wakipangwa vijijini. Sasa naomba Wizara itueleze inatoa mwongozo gani linapotokea tatizo la namna hii ambapo watumishi hawaji na wengine wanakuja na barua za uhamisho toka Makao Makuu wakati wanapofika pale Masasi, sasa sisi tunategemea tufanye nini? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna matatizo ya watumishi kukubali

kufanyia kazi maeneo ya pembezoni ikiwemo Masasi. Naamini baada ya barabara kukamilika Masasi haitakuwa tena eneo la pembezoni na ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba lazima tujaribu kuwa wabunifu na kuweza kuangalia mazingira ya kazi ambayo yatakutia watumishi wa afya na elimu kukubali kwenda kufanyia kazi katika maeneo ya pembezoni, ikiwa na vivutio vingine ambavyo ofisi yangu na Wizara ya Afya pamoja na ile ya Wizara ya Elimu itaiangalia ili wananchi walio katika maeneo haya ya pembezoni wasikose haki yao ya kupata huduma kutoka Serikalini. (*Makofi*)

Na. 72

Vitalu vya Uwindaji – Rufiji

MHE. BAKARI M. MBONDE aliuliza:-

- (a) Je, ni vitalu vingapi (kwa majina) vya uwindaji wa kitalii vipo Wilayani Rufiji?
- (b) Je, vitalu hivyo vimechangia fedha kiasi gani kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, kati ya mwaka 1999 hadi 2004 kutokana na asilimia 25 ya mapato ya Serikali?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbonde, Mbunge wa Rufiji, naomba kutoa maelezo ya ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pato la asilimia 25 kwa Halmashauri za Wilaya hutokana na ada za wanyamapori wanaowindwa katika maeneo (vitalu) yaliotengwa kwa ajili ya uwindaji wa kitalii kwenye Wilaya husika kila mwaka. Mapato hayo hupelekwa kwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya husika.

Wizara yangu imetoa maelekezo ya namna ya kutumia fedha hizo ambayo yanazitaka Halmashauri za Wilaya zinazopata mgao huo kutumia asilimia 60 ya fedha hizo katika kuchangia miradi ya maendeleo ya wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya uwindaji. Aidha, asilimia 40 ya fedha hizo zielekezwe kwenye shughuli za uhifadhi wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya msingi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbonde, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ina jumla ya vitalu 7 vya uwindaji wa kitalii. Kati ya hivyo, kitalu kimoja (1) cha Ngarambe/Tapika kinachomilikiwa na Kampuni ya *Game Frontiers (T) Ltd* kipo kwenye eneo la wazi (*open area*) na vitalu sita (6) vipo ndani ya Pori la Akiba la *Selous* kama ifuatavyo:-

Selous Game Reserve LL1;
Selous Game Reserve LL2 ;
Selous Game Reserve UA ;
Selous Game Reserve LL3;
Selous Game Reserve RU1;
Selous Game Reserve MS I.

- (b) Katika kipindi cha mwaka 1999 hadi 2004, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji imepata jumla ya TZS 80,996,069.00 kama mapato ya asilimia 25 kutokana na ada za wanyamapori waliowindwa.

MHE. BAKARI M. MBONDE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

- (a) Kwa kuwa asilimia 25 imekuwa ikisadia sana maendeleo katika Wilaya ya Rufiji na Wilaya zingine nchini lakini mgao huo huwa unachelewa sana pengine inachukua mwaka mzima kabla ya mgao huo haujapelekwa kwenye Wilaya husika. Je, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba mgao huo unapelekwa mapema sana? (*Makofi*)
- (b) Kwa kuwa kiwango cha asilimia 25 kiliwekwa miaka 15 iliyopita. Je, Serikali iko tayari kufanya marejeo ili kiwango hicho kiongezwe kiwe asilimia 30 katika jitihada za kupambana na umaskini? (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, suala la fedha hizi za asilimia 25 kwamba kufika kwa wakati tunapenda kuahidi tutafanya hivyo. Lakini niseme ni kwamba ni kweli mwaka huu wa fedha, fedha hizi zilikuwa zimechelewa na zilichelewa pia kwa sababu kulikuwa na makato mbalimbali ambayo tulipata kutoka Wizara ya Fedha. Lakini tumeziweka pia kwenye Bajeti ya mwaka 2004/2005 ili kuhakikisha kwamba Wilaya zile ambazo zilikuwa hazikupata fedha hizi zitapata. Lakini napenda pia kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba fedha hizi tutajaribu ziende kwa wakati. Suala la kuongeza asilimia 25 naomba suala hili tulifanyie utafiti ili kujua hali itakavyokuwa. (*Makofi*)

MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Katika Vijiji vile ambavyo vinazunguka *Selous* na ambako kuna hivi vitalu vya uwindaji katika maeneo mengine wenzetu huwa wanafaidika kutengenezewa barabara, zahanati na kadhalika.

Lakini sisi Rufiji tunapata hiyo asilimia 25 lakini mambo mengine kama wenzetu wanavyofanyiwa hayafanyiwi. Je, sasa inawezekana tukaweza kufanyiwa kama wanavyofanyiwa katika maeneo mengine yaliyokuwa na vitalu vya uwindaji?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, katika sera za maliasili za kushirikisha wananchi na kwamba wananchi wafaidike na mali hii ndiyo mpango huu kwa kweli wa kutengeneza barabara katika maeneo hasa ya *Selous* ili maeneo haya yaweze kupitika na wananchi waone faida ya wanyamapori.

Ni kweli kabisa kwamba jambo hili limefanyika katika barabara kadhaa na tunapenda kusema kwamba hatuwezi kumaliza barabara nzima yote kwa wakati mmoja, inakwenda kwa awamu. Lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba suala hili ni la kudumu na kwamba nina hakika kwamba siku moja litafika kwake pia.

Na. 73

Utalii Katika Mkoa wa Kagera

MHE. GWASSA A. SEBABILI aliuliza:-

Kwa kuwa Wilayani Ngara vipo vivutio vingi vya utalii kama vile maporomoko ya Rusumo kwenye Mto Kagera, ukaribu wa vyanzo vya maji vya Mto Nile, mapori ya Akiba ya Shimisi na Burigi yenye wanyama wengi, wadudu na uoto wa kupendeza, bonde tambarare la Mto Kagera wanakoishi viboko na mamba wengi, chemichemi za maji moto na kadhalika na kwa kuwa Wilaya ina miundo mbinu muhimu kama watalii na wawekezaji zikiwemo barabara, uwanja wa ndege, umeme na hali ya hewa ya kuvutia:-

- (a) Kwa sifa hizo na nyingine nyingi; je, ni lini Serikali itaitangaza Ngara kuwa Wilaya ya utalii na uwekezaji?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza na kuimarisha rasilimali hiyo muhimu kuwa vitega uchumi ili kuondoa umaskini Wilayani Ngara na Taifa letu kwa ujumla?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Wizara yangu kwa ushirikiano wa Tawala za Mikoa imeorodhesha vivutio vya utalii katika Mikoa iliyo mingi nchini. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kuwa Wizara yangu inatambua urithi mkubwa wa utalii uliopo Mkoani Kagera kwa ujumla na Wilayani Ngara kipekee. Hata hivyo, ningependa kumwarifu Mheshimiwa Mbunge, kuwa Sera ya Serikali ni kutangaza nchi nzima kama kituo cha utalii, kazi inayofanywa kwa ushirikiano na wadau wengine. Hata hivyo, hii haizuii jitihada za uongozi wa Wilaya au Mkoa za kujitangaza. Shughuli za kitalii na maendeleo katika sekta ya utalii ndizo zitakazokuwa

chachu ya kuitangaza Wilaya ya Ngara kama Wilaya ya utalii na uwekezaji, ndani na nje ya nchi.

- (b) Mheshimiwa Spika, jukumu la kuendeleza utalii ni jukumu la sekta ya umma pamoja na sekta binafsi. Sekta binafsi inalo jukumu la kuendesha biashara ikiwa ni pamoja na kujenga hoteli, kuanzisha biashara za wakala wa utalii, kama kusafirisha watalii katika maeneo ya vivutio na hata kutangaza. Pamoja na kutangaza wakati huo huo Serikali inalo jukumu la kuhakikisha kwamba usalama, miundo mbinu kama barabara, maji njia za mawasiliano zinakuwepo ili kuchochea maendeleo ya eneo husika. Wizara yangu kwa kushirikiana na sekta binafsi Mkoani Kagera imekwishaanza shughuli za kuendeleza utalii Mkoani humo. Sekta binafsi imeanza kuboresha huduma za malazi kwa kujenga hoteli nzuri na za kisasa, kama vile Hoteli ya *Walkguard*, Loji ya *Travelers* na Hoteli ya *Eden*. Pia sekta binafsi imeboresha maeneo ya kambi za wageni na kuanza kutoa huduma za wakala wa kusafirisha watalii. Aidha, Shirika la Ndege binafsi limeongeza huduma zake Mkoani humo na hivyo kuufanya Mkoa kufikika kirahisi.

Katikati ya mwezi Oktoba Wizara yangu ilituma wataalam kutembelea Wilaya zote za MKoa wa Kagera kwa ushirikiano na Uongozi wa Mkoa. Lengo kuu la ziara hiyo lilikuwa kubaini na kutathmini vivutio vya utalii na maeneo ya uendelezaji utalii Mkoani humo.

Ujumbe huo ulifuata baada ya ziara yangu katika Mkoa wa Kagera na hususan Wilaya ya Ngara iliyofanyika tarehe 20 -22/05/2004. Katika ziara hiyo, majadiliano yalifanyika kati ya wataalam hao na wadau wengine kuhusu uendelezaji Utalii na masuala mengine yanayohusu utalii. Kama ilivyo kwa Mikoa mingine, taarifa na picha zinazopatikana zitatumika katika jitihada za kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje.

MHE. GWASSA A. SEBABILI: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Bado nizidi kumshukuru kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ngara kwamba katika ziara yake mwaka jana mwezi tano aliahidi kuandikisha Pori la Wanyama la Shimisi kuwa Hifadhi ya Taifa na hakika Serikali ikafanya hivyo na majumba yanajengwa kupeleka walinzi kulinda pori hilo. Pamoja na hayo naomba niulize mawili kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa timu hiyo imejaliwa kufika Kagera na imebaini vivutio vingi katika Wilaya ya Ngara. Je, ni lini Serikali itaweza kutangaza Wilaya ya Ngara kwa sababu ya kujenga kwa mfano hoteli ya watalii kando kando ya Mto Kagera palipo na maporomoko ya maji ya Rusumo?
- (b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la wawekezaji mara nyingi ni Miundo mbinu na kwa kuwa Wilaya ya Ngara, ina bahati ya kuwa miundombinu ya kutosha kwa wakati huu kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza na aliona

mwenyewe na kwa hivi sasa tunategemea kwamba itajengwa reli kutoka Isaka kwenda Ruanda kupitia Wilayani ngara.

SPIKA: Uliza swali, Mheshimiwa Mbunge.

MHE. GWASSA A. SEBABILI: Wakati huo huo kuna uwanja mzuri wa ndege katika Wilaya ya Ngara.

Je, ni lini Serikali itakubali sasa kuitangaza Wilaya ya Ngara kwamba inavyo vivutio vya kutosha na kwa hiyo wawekezaji waweze kuja kuinua maisha ya Watanzania wanaoishi upande huo? (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kama vile nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba baada ya wataalam kufika Ngara na kuona vivutio vya utalii, Wizara imeamua kuendelea kutangaza sehemu hii. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba mara kwa mara kila anapokuja mwekezaji basi pia tunazungumzia Kagera na tunazungumzia Ngara kwa ujumla wake. Tuombe kwamba baada ya Miundo mbinu hii kuimarika zaidi kwamba wawezekezaji pia watakuja katika maeneo haya muda si mrefu.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linahusu vivutio vya utalii na kwa kuwa kule Kihansi kwenye maporomoko ya Mto wa Kihansi kulikuwa na vyura ambao walikuwa wanazaa na walikuwa kivutio kikubwa kwa watalii. Je, Serikali inajua kwamba vyura hao sasa wametoweka na inasemaje? (*Makofi*)

SPIKA: Ni swali jipya lakini nadhani majibu unayo Mheshimiwa Waziri endelea kulijibu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, mtakumbuka kwamba vyura hawa wa Kihansi walipelekwa Marekani kwa utafiti ili kuhakikisha kwamba wanadumu katika maeneo haya baada ya eneo hili kutumika kwa ajili ya umeme.

Vyura hawa wamepelekwa katika *zoo* mbalimbali kule lakini siwezi kusema kwamba vyura hawa wamemalizika kule Kihansi. Kwa taarifa ambazo nilizopata kutokana na wataalam wangu ni kwamba vyura hawa wapo lakini ni wachache waliobakia.

Na. 74

Kuongeza Kiwango cha Bajeti kwa Kilimo

MHE. JOB Y. NDUGAI aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkutano uliofanyika huko Maputo - Msumbiji Julai, 2003 Wakuu wa Nchi za Afrika (*African Union*) walizitaka nchi za Afrika kuongeza kiasi cha bajeti za nchi zao kinachotengwa kwa ajili ya kilimo hadi kufikia kiwango kisichopungua asilimia 10 ya bajeti zao:-

Je, kilimo kimekuwa kikitengewa kiasi gani na kiasi hicho ni asilimia gani ya bajeti katika maeneo yapi kwa bajeti za kati ya mwaka 2000/2001 hadi 2004/2005?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Sekta ya Kilimo inahusisha Wizara ya Kilimo na Chakula, Ushirika na Masoko, Maji na Maendeleo ya Mifugo (Mifugo), Maliasili na Utalii (Uvuvi, misitu, wanyamapori na ufugaji wa nyuki) na Ujenzi (Barabara Vijijini).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa 2000/2001 hadi 2004/2005, sekta ya Kilimo ilikuwa ikitengewa wastani wa shilingi bilioni 101.05 kwa mwaka, sawa na wastani wa asilimia 5.2 ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2000/2001 Sekta ya Kilimo ilitengewa shilingi 62.4, sawa na asilimia 5.7 ya Bajeti ya Serikali, mwaka wa 2001/2002 ilitengewa shilingi bilioni 52.1 sawa na asilimia 3.6 na mwaka wa 2002/2003 ilitengewa shilingi bilioni 84.5 sawa na asilimia 4.5. Katika mwaka wa 2003/2004 kulikuwapo ongezeko kubwa la kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya sekta ya kilimo, shilingi bilioni 148.6, sawa na asilimia 6.8 zilitengwa. Aidha, katika mwaka wa 2004/2005 shilingi bilioni 157.7 sawa na asilimia 5.5 zilitengwa. Katika mwaka wa 2005/2006 sekta ya kilimo imeomba jumla ya shilingi bilioni 253.2. Endapo maombi hayo yatapitishwa na Bunge hili tukufu, jumla ya shilingi bilioni 253.2 zitakuwa zimetengwa kwa ajili ya sekta ya kilimo sawa na asilimia 7.2 ya Bajeti yote ya Serikali ya mwaka wa 2005/2006.

Kuanzia mwaka wa 2001/2002 hadi 2004/2005, Sekta ya Kilimo ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 446.6. Kati ya fedha hizo sekta ndogo ya mazao ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 176.61 sawa na asilimia 39.5 ya bajeti ya serikali ya Kilimo, Maliasili lina Utalii ilitengewa shilingi bilioni 134.46 sawa na asilimia 30.1, Barabara za Vijijini zilitengewa shilingi bilioni 66.6 sawa na asilimia 14.9, Mifugo ilitengewa shilingi bilioni 39.5 sawa na asilimia 8.9 na Ushirika na Masoko ilitengewa shilingi bilioni 29.4 sawa na asilimia 6.6.

Kutokana na takwimu hizo, Serikali imekuwa ikiongezewa fedha zinazotenga kwa ajili ya sekta ya kilimo mwaka hadi mwaka kuelekea kwenye lengo lililowekwa na Wakuu wa Nchi za Afrika (*African Union*) katika mkutano uliofanyika Maputo Julai, 2003 la kuongeza kiasi cha bajeti za nchi wanachama kwa jumla hiyo kinachotengwa kwa ajili ya sekta ya kilimo kufikia asilimia 10 ya bajeti ya Serikali ifikiapo mwaka 2007/2008.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, na nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na ningependa kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri kwa kukubali kutembelea Kijiji cha Kibaigwa kujionea mwenyewe mapambano dhidi ya umaskini. Nina maswali mawili madogo tu ya nyongeza

La kwanza, Mheshimiwa Waziri ameelezea asilimia ambazo zimekuwa zikitengwa kuelekea kwenye Wizara ya Kilimo kwa miaka yote hii kuwa kati ya 5, 6, na mwaka huu 7.2. *Naturally* swali langu ni kwamba kwa kuwa Rais wetu alikuwa mmoja wa Wakuu wa nchi za Afrika waliokubaliana kwamba asilimia sasa iwe ni 10. Swali langu kwanza nini mnam-*let down* kwa nini mnamwangusha Rais wetu katika hili, kwa nini haiwi asilimia 10? (*Maokfi*)

La pili, kwa kuwa wakulima wetu wengi vijijini wanatumia jembe la mkono na nia ya kuongeza bajeti ya Kilimo ni kuwawezesha wananchi hawa kuondokana na kilimo cha jembe la mkono kwenda kwenye plau na matrekta. Je, masharti magumu ambayo yanaendelea kuwepo katika kuwakopesha wananchi matrekta yanaweza kweli kusaidia kupambana katika mkakati huu mpya unaoitwa MKUKUTA? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu ongezeko hadi kufikia asilimia 10 kama nilivyojibu katika swali la msingi mwelekeo ni kuwa imeongezeka mwaka hadi mwaka kuelekea huko kwa asilimia 10. Na kwa kuwa mwaka 2007/2008 bado hazijafika na tayari tuko kwenye asilimia hiyo niliyotaja basi tuingeze ndugu yangu. Tunajitahidi kufikia huko. (*Makofi*)

Pili, kuhusu lengo la kuondokana na jembe kufikia plau na trekta kwa kupitia Mfuko ule wa pembejeo na akasema kuwa Mheshimiwa kuwa kuna masharti magumu. Kwa kweli napenda kumthibitishia Mheshimiwa Ndugai kuwa masharti yamewekwa hivyo kuulinda huo mfuko. Mara ya kwanza tulikuwa hatuna masharti magumu sana. Matokeo yake tukawa na deni la bilioni 5 na hivyo tukakwama kukopesha. Kwa hivi

napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kuwa masharti ya kuulinda mfuko na hata hivyo, watu tayari wameshapata msaada wa matrekta na maplau kupitia mfuko huu. Kwa hivyo unakaribishwa Mheshimiwa kuwahamasisha wananchi wako waombe. Lakini si lazima wapate wote kwa sababu ya ufinyu wa bajeti iliyopo.

MHE. THOMAS NGAWAIYA: Nashukuru Mheshimiwa Spika, nilitaka nimwulize Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa mimi napata shida sana ninaposikia kutokana na jibu lake la msingi kwamba kilimo ni maji, ni barabara, mifugo, na mara nyingi nimekwishasikia vinasemwa hapa. Kwa nini tusijibiwe kama Wizara kwamba Wizara ya Kilimo *per se* bajeti yake ni vipi kwa sababu nazo zingine zina bajeti zake. Kwa nini tunaambiwa Kilimo ni maji, ni barabara, ni ushirika? Naomba jibu hilo. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, kilimo kama kilimo kinahusisha mambo mengi, hii Wizara ya Kilimo na Chakula inahusikana na mazao tu. Lakini kilimo kwa maana pana ya *FAO* inahusu mifugo vile vile.

Kwa mfano, ng'ombe, mbuzi, kuku na kadha wa kadha na kwa upande wa Maliasili kama nilivyosema, samaki ni sehemu ya kilimo na vile vile Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo *sorry* na Wizara ya Ushirika na Masoko yanahusiana na Kilimo kwa sababu ndani ya Ushirika, Ushirika wetu hasa katika Tanzania unahusu mazao na uchukuzi wake na ndiyo suala la barabara vijijini.

Kwa hivi, ninachotaka kusema ni kuwa kilimo ina maana pana kama mtu akitaka kuuliza asiseme tu kilimo, aseme anataka kujua ongezeko la sehemu ya bajeti kuhusu uzalishaji wa mazao. Hapo tutatoa jibu linalohusiana na mazao tu. Kwa hivi ni sahihi niliyokuwa nimetamka. *(Makofi)*

Na. 75

Zao la Chakula na la Biashara kwa kila Wilaya

MHE. JOEL N. BENDERA (K.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO) aliuliza:

Kwa kuwa Serikali katika kuimarisha kilimo nchini imeimarisha utaratibu wa kila Wilaya kuchagua zao moja la chakula na moja la biashara:-

- (a) Je, zao la ngano lililochaguliwa kuwa zao la chakula kwa Wilaya ya Lushoto limefanikiwa kwa kiwango gani?
- (b) Kwa upande wa zao la biashara la kahawa lililochaguliwa kwa Wilaya hiyo, je, ni kiasi gani cha fedha zimetolewa kama msaada na zimetumika vipi kuendeleza zao la kahawa?

- (c) Je, ni vijiji gani vya jimbo la Bumbuli vimefaidika na msaada huo kwa zao la kahawa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka wa 2004/2005 niliyotoa hapa Bungeni katika kikao cha 14 cha mkutano wa 16, nilifuta wazo la zao moja la chakula na zao moja la biashara kwa kila Wilaya na kuziachia Wilaya jukumu la kuamua ni mazao gani yapewe kipaumbele kwa kuzingatia mazingira ya kila Wilaya na mipango yao ya maendeleo. Baada ya maelezo haya mafupi sasa napenda kujibu swalila Mheshimiwa Shellukindo kama ifuatavyo:-

- (a) Wakulima wa Tarafa ya Bumbuli, Soni, Mlalo na Mtae wa Wilaya ya Lushoto wamekuwa wakilima ngano kama zao la chakula la kujikinga na njaa. Zao hilo hupandwa katika miezi ya Mei na Juni ambacho ni kipindi cha baridi kali na kisichokuwa na mvua za kutosha. Kutokana na zao hilo kupandwa wakati wa baridi kali na upungufu wa mvua na kutokana na udongo wa milima ya Usambara kuwa na rutuba kidogo na kuathiriwa na mmomonyoko wa udongo, zao la ngano limekuwa likitoa mavuno machache sana. Kwa mfano, kati ya msimu wa 2001/2002 na 2003/2004, wastani wa mavuno ya ngano kwa mwaka ulikuwa tani 13.7 tu. Kutokana na hali hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto haikuliweka zao hilo katika mpango wake wa maendeleo ya kilimo.
- (b) Mheshimiwa Spika, kahawa ni miongoni mwa mazao ambayo Wilaya ya Lushoto inayapa kipaumbele katika uchumi wake. Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara ya Kilimo na Chakula iliipa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto jumla ya shilingi 46,460,000 kwa maelekezo ya kuzitumia kununua mashine ya kupokuchua kahawa. Kwa kuzingatia kiwango kidogo cha uzalishaji wa kahawa kwa sasa, uongozi wa Wilaya ya Lushoto ulileta pendekezo Wizarani kutaka fedha hizo zitumike kuendeleza zao la kahawa badala ya kununua mashine hizo. Wizara iliafiki mapendekezo ya Wilaya na fedha hizo sasa zitatumika kugharamia ununuzi wa miche bora ya kahawa kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (*TACRI*) na kugharamia mafunzo ya kilimo bora cha kahawa kwa wataalamu na wakulima.
- (c) Vijiji vya Tarafa ya Bumbuli vitakavyonufaika na mradi wa uendelezaji zao la kahawa ni pamoja na Dule, Kwehangala, Bumbuli Kaya, Bumbuli *Mission*, Wena na Mbokoi.

MHE. JOEL N.BENDERA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutamka wazi kwamba zao la chakula lisiwe moja kwa sababu kuna maeneo mengine kama Mwambao wa Pwani wao wanakula vyakula vingi tu muhogo, mahindi, wali, ukiondoa Wasukuma ambao wao wanakula ugali tu kila siku.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba pamoja na majibu mazuri nilitaka nifahamu kwamba je, huu mpango wa kuchagua zao moja la chakula Serikali mpaka sasa hivi katika utafiti wake nchi nzima ni Wilaya ipi ama ni Mkoa upi ambao wameona umefanikiwa kwa zao hilo kwa wingi katika eneo hilo ambalo wameamua toka mpango huu umeanza mwaka jana?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tulitamka kuwa imefuta na utafiti hatukufanya. Sasa kama utatakiwa tufanye sasa basi tutaanza upya. Ukweli ni kuwa Wilaya kama nilivyosema ziamue mazao gani wanataka kuotesha kama wanataka moja hiari, mawili, matatu, manne au mengi zaidi ruksa. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na kwamba Serikali imeondoa mpango wa kufadhili au kusaidia zao moja. Na mpango huu kwa sisi ambao hatupati ruzuku kama Mikoa mingine inayopata ruzuku tuliichukulia ndiyo itakuwa ruzuku ya Serikali katika maeneo yale ambayo hatupati ruzuku.

Sasa kwa kuondoa mpango huu ina maana Wilaya nyingine au Mikoa mingine haitapata ruzuku kabisa katika mazao mbalimbali. Serikali ina mpango gani kueneza ruzuku katika Mikoa yote, kwa sababu mazao ni muhimu kila Mkoa? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, ninavyoelewa mimi ni kuwa kila Wilaya inastahili msaada fulani kutoka Wizara ya Kilimo hasa kwa kupitia ule mradi wake wa *DADAP – District Agriculture Development Programme*) ambapo karibu ziko shilingi bilioni 4 Wizara ya Kilimo lakini yenyewe haiagizi nini kifanywe. Inaibuliwa huko inakuja halafu tunashauriana na hapo mgao unaanza. Kwa hivi, Mheshimiwa Mbunge unashauriwa ukirudi nyumbani ushirikiane na Halmashauri husika ya Lushoto kusudi muibue mradi munufaike na ruzuku hiyo ipo, fedha zipo.

Na. 76

Ranch za NARCO – West Kilimanjaro

MHE. LEKULE M. LAIZER aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuiuza au kuitoa *ranch* niliyoitaja *NARCO* na *NAFCO* kwa wawekezaji na wapo wananchi wanaoishi kando kando mwa *ranch* hizo:-

- (a) Je, wananchi wa vijiji ambavyho vipo jirani na ranchi hizo na wanalisha mifugo yao huko, isingekuwa busara wakapewa maeneo hayo ili waendeleo kuyatumia kwa mifugo yao?
- (b) Kwa kuwa Serikali ilipochukua maeneo hayo m ara ya kwanza walifungua *ranch*, Lakini wananchi hao hawakulipwa fidia walipoondolewa kwa amri na maeneo yao kufanywa ranchi za Taifa. Je, kwa nini wasipewe eneo hilo kwa matumizi ya mifugo yao?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Umilikishaji wa maeneo ya ranchi ndogo ndogo katika ranchi za Taifa (*NARCO*) inatekelezwa kwa kuzingatia maelekezo ya Baraza la Mawaziri kupitia Waraka Na. 2 wa 2002. Waraka unaelekeza kuhusu umilikishwaji wa baadhi ya *ranch* za Taifa kwa wawekezaji Watanzania. Kulingana na utaratibu huo, *NARCO* itabakia na eneo la hekta 20,000 tu za mfano kwenye *ranch* zake, isipokuwa *ranch* za Kongwa na Ruvu ambazo hazitagawanywa. Hadi sasa ranchi ndogo 45 zimemilikishwa kwa Watanzania na shughuli hii itakuwa imekamilika ifikapo Julai, 2005.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali kuhusu ranchi za Taifa ikiwa ni pamoja na *ranch* ya *West Kilimanjaro* ni kuigawa katika maeneo ya *ranch* ndogo ndogo ambazo zitamilikishwa kwa wawekezaji Watanzania wenye nia na uwezo wa kufuga kisasa na kibiashara na si kwa shughuli nyingine. Baada ya umilikishaji huo *ranch* hizo hazitauzwa isipokuwa wawekezaji watatakiwa kuziendesha kwa utaratibu uliokubaliwa.

Madhumuni ya mpango huu ni kuwawezesha wawekezaji Watanzania kuingia kwenye ufugaji wa kisasa na wa kibiashara. Wananchi waishio jirani na *ranch* hizi ni washiriki muhimu wa mpango huu na wanahimizwa kujiandaa kushiriki ili waweze kumilikishwa *ranch* hizo. Napenda kuwahakikishia wananchi hao kwamba Serikali inazingatia sana mahitaji ya namna hiyo kama ilivyokwisha kutoa kipaumbele kwa baadhi ya wananchi na *ranch* zilizokwisha kupimwa na kumilikishwa katika sehemu nyingine nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huo huo, *ranch* ya *West Kilimanjaro* yenye ukubwa wa hekta 31,000 itagawanywa kwenye *ranch* ndogo ndogo na kubaki na hekta 20,000 za mfano. Eneo litakalobaki la hekta 11,000 litamilikishwa kwa wawekezaji binafsi wakiwemo wanavijiji waishio jirani na *ranch* hiyo. Wakati utakapowadia wa kumilikishwa ranchi ya ***West Kilimanjaro***, matangazo yatatolewa kwenye vyombo vya habari ili kuwapa fursa watu wote wenye nia na uwezo kushiriki kikamilifu.

Ni matumaini yangu kuwa Mheshimiwa Mbunge atawahamasisha wananchi wa Jimbo lake wajitokeze ili waweze kuomba kugawiwa maeneo ya kufuga kisasa na kibiashara katika ranchi ya West Kilimanjaro pale matangazo yatakapotolewa.

- (b) Mheshimiwa Spika, *ranch* ya *West Kilimanjaro* imetokana na jumla ya mashamba kumi ya wakulima wa kikoloni. Mashamba haya yalianzishwa kati ya mwaka 1939 na mwaka 1964 na kupewa hati miliki. Serikali iliyachukua mashamba hayo tangu mwaka 1965 na kuyaendesha chini ya Shirika la Maendeleo ya Taifa (*NDC*) na badae *NARCO* mwaka 1970. Hivyo siyo sahihi kusema kwamba mashamba haya yalianzishwa kwa kuwanyang'anya ardhi wananchi wa maeneo haya kama anavyodai Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, rashi ya *West Kilimanjaro* ni mali ya Serikali na hakuna mpoango wa kuiuza ama kuirudisha kwa wakoloni wamiliki wa awali bali Serikali ina mpango wa kuigawa na kuwamilikisha wananchi wazalendo ili waendeleze ufugaji wa kisasa na wa kibiashara kama ilivyo azma yake kuhusu ufugaji bora.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ardhi ya *West Kilimanjaro* imegawanywa katika maeneo makubwa, hifadhi ya Taifa, Msitu wa Taifa wa *West Kilimanjaro*, Mashamba makubwa ya wazungu pamoja na hizi *ranch* na wananchi wa Jimbo la Longido na Jimbo la Siha hawana maeneo. Kwa nini wapewe wawekezaji wengine wasipewe wananchi walioko katika maeneo hayo? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa wananchi wamekwishavamia kwa wingi sana mashamba haya kutokana na kwamba hakuna kinachofanyika katika hayo mashamba. Je, Serikali kwa nini isiwape hao waliopo kuliko kuwatafuta wawekezaji wengine walioko mbali? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, kwenye jibu la msingi nimeeleza kwamba watakaomilikishwa ni wananchi wanaozunguka maeneo hayo ndiyo watapewa kipaumbele.

Pili, nimeeleza vizuri kwamba maeneo hayo ni mali ya Serikali sasa wavamizi ambao wameingia siyo kihalali. Lazima waelewe kwamba wanatenda kosa. Lakini wakati huo huo ningependa kuwaomba wananchi wote hapa nchini kupitia Bunge lako

Tukufu kwamba tungechukua kwa umakini zaidi dhana ambayo alieleza hapa Waziri wa Kilimo kwamba katika hekta moja badala ya kuzalisha mfano unazalisha kilo 250 za pamba ingekuwa vizuri tufuate utaratibu wa ukulima wa kisasa ili ufikie kilo 800 mpaka 1,200 badala ya kutafuta kupanua maeneo na ndiyo haya yanayotusababishia kuvamia maeneo yasiyohusika. Kwa hiyo, naomba wananchi waliovamia maeneo hayo wajue kwamba ikifika wakati wa kumilikisha kwa waombaji halali itabidi wayaachie.

Na. 77

Mpango wa Kuboresha Huduma ya Maji – Musoma

MHE. IBRAHIM W. MARWA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AfD*) iko katika mpango wa kuboresha mfumo wa majisafi na majitaka katika mji wa Musoma, Bukoba na Misungwi ili kuwaondolea kero wakazi wa miji niliyoitaja hapo juu ambayo inalizunguka Ziwa Victoria. Kwa kuzingatia ni baada ya miradi kama hiyo kukamilika katika Jiji la Mwanza.

Kwa kuwa mji wa Musoma unaendelea kukua kwa kasi na hivyo mahitaji ya huduma ya maji yanaongezeka vivyo hivyo katika Kata za Bweri, Nyakato, Buhare, Makoko, Nyamatara na Kagera; na kwa kuwa, Serikali ilishatoa tamko kuwa kazi hiyo ingeanza mwaka 2005:-

- (a) Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu utekelezaji wa mradi huo katika mji wa Musoma ikizingatiwa kuwa hiyo ni ahadi ya muda mrefu?
- (b) Je, ni gharama kiasi gani zinazotarajiwa kutumika katika mradi huo?
- (c) Kama jibu katika sehemu (a) ya swali hili ni ndiyo. Je, Mradi huo utatekelezwa katika awamu ngapi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendeleo la *AfD* iligharamia mradi wa uchunguzi (*Feasibility Study*) wa Majisafi na Majitaka kwa miji ya Bukoba, Musoma na Misungwi. Uchunguzi huo ulikamilika Desemba 2004. Ripoti ya uchunguzi huo imewasilishwa kwa Mfadhili *AfD* Kwa ajili ya kuomba fedha za ujenzi wa mradi. Uchunguzi huu uliharimu jumla ya shilingi milioni 226.1.

- (b) Mheshimiwa Spika, uchunguzi nilioutaja uliainisha hatua za haraka zinazotakiwa kuchukuliwa hivi sasa (*immediate measures*), hatua za muda mfupi (*short term measures*) na hatua za muda mrefu (*long term measures*), zenye lengo la kukidhi mahitaji ya muda mrefu (hadi 2025) ya huduma za majisafi na uondoaji majitaka katika miji niliyoitaja. Jumla ya gharama za kutekeleza mradi mzima ni kiasi cha shilingi bilioni 34.2. Kazi zilizopangwa kufanyika hivi sasa ni zile za haraka (*immediate measures*) ambazo ni pamoja na usanifu wa majisafi na majitaka, utayarishaji wa vitabu vya zabuni, ufungaji wa dira za maji, ukarabati na upanuzi wa mfumo wa majisafi kwenye maeneo mbalimbali yakiwemo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Kazi hizi zinakisiwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 3.1.
- (c) Mheshimiwa Spika, kutokana na ripoti ya uchunguzi, mradi huu utatekelezwa katika awamu tatu kama nilivyozitaja:-
- (i) Awamu ya 1, usanifu wa majisafi na majitaka, utayarishaji wa vitabu vya zabuni, ufungaji wa dira za maji, ukarabati na upanuzi wa mfumo wa majisafi uliopo. Lengo la awamu hii ni kuimarisha huduma inayotolewa hivi sasa.
 - (ii) Awamu ya pili, ujenzi wa mifumo mipya ya majisafi na majitaka ili kukidhi mahitaji ya muda mfupi na wa kati (hadi 2015) kwa huduma hizo.
 - (iii) Awamu ya tatu, kuendelea na ujenzi wa mifumo ya majisafi na majitaka ili kukidhi mahitaji hadi kufikia mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, Serikali imewasilisha maombi ya fedha za kutekeleza mradi huu kwa Shirika la Maendeleo la Ufaransa. Ujenzi wa mradi utanza mara tu fedha zitakapopatikana.

MHE. IBRAHIM W. MARWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwanza nashukuru kwa jitihada ambazo Serikali imeonyesha. Lakini ningependa tu kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba mradi huu toka tumeanza kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu sasa ni mwaka wa tano, na wananchi kule jimboni walidhani ni porojo. Kwa hiyo, nataka awatamkie kupitia Bunge lako Tukufu kwamba si porojo isipokuwa ni mradi ambao unatekelezeka? Ahsante sana Mheshimiwa Spika, (*Kicheko*)

SPIKA: Nadhani kutokana na majibu yake, wananchi wa Musoma watakuwa wamesikia kwamba unatekelezwa. Kwa hiyo, hana haja ya kutamka tena.

Na. 78

Chumvi Isiyo na Madini Joto

MHE. LEONARD M. SHANGO (K.n.y. MHE. DIANA M. CHILOLO)
aliuliza:-

Kwa kuwa akina mama wa kijiji cha Nkonkilangi, Kata ya Ntwike Tarafa ya Shelui, Wilayani Iramba, wanajishughulisha na mradi wa kupika chumvi ambayo ni nyingi na nzuri sana na kwa kuwa chumvi hiyo haina madini joito:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia tatizo hilo ili chumvi hiyo iweze kuwa na faida kwa watumiaji na pia kupata soko zaidi la Kitaifa na Kimataifa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa akina mama wa kijiji cha Nkonkilangi, Wilayani Iramba, wanazalisha chumvi nyingi na nzuri na kwa muda mrefu chumvi yao haikuwa na madini joito.

Kwa kutambua ukweli huo Maafisa wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Wizara ya Afya pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*) wametembelea maeneo ya Manyoni na Misugaa (Wilaya ya Singida Vijijini) na Nkonkilangi Wilayani Iramba, Mkoani Singida.

Aidha wamefanya warsha mbili za kitaifa mwezi Juni mwaka 2001 na mwezi *March* mwaka 2004 na wamesafirisha madini joto kutoka Dar es Salaam hadi kwenye Maabara ya Madini hapa Mjini Dodoma. Lengo la hatua zote hizo ni:-

Kwanza, kutoa mafunzo na pili kuhamasisha matumizi ya madini joto. Pamoja na mafunzo hayo na hatua hizo nyingine zilizochukuliwa, kiasi cha kilo 400 cha madini joto pamoja mitambo midogo ya kuchanganyia madini joto katika chumvi ipatayo 582 zilitolewa na *UNICEF* na ambavyo vilitumiwa kwenye mafunzo niliyoyataja vimekabidhiwa kwa Halmashauri ya Mji wa Singida kwa ajili ya kusambazwa baadaye kwa wazalishaji chumivi Mkoani Singida.

Usambazaji wa vifaa hivyo ulifanyika mwezi Novemba, mwaka 2004 chini ya usimamizi wa Wataalam wa Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Afya ambapo wazalishaji walikumbushwa na wataendelea kukumbushwa tena matumizi ya vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini itaendelea kushirikiana na Wizara ya Afya, *UNICEF* na Taasisi mbalimbali na watu binafsi watakaokuwa tayari kusaidia uboreshaji wa shughuli za uzalishaji chumvi katika Kijiji cha Nkonkilangi na maeneo mengine nchini. *(Makofi)*

Hata hivyo, jukumu la kupata soko linategemea kwanza juhudi za wazalishaji au mzalishaji katika kujiandaa na kujitangaza na kutangaza chumvi yake kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali hapa nchini zinazoshughulika na masuala ya biashara.

Mheshimiwa Spika, na mwisho kabisa Mheshimiwa Mbunge atapata jibu ambalo lina ufafanuzi zaidi kuliko hili ambalo nimelisoma kwa kuzingatia muda.

SPIKA: Sawa sawa!!

MHE. LEONARD M. SHANGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa akina mama hawa katika kijiji Nkonkilangi wanaojishughulisha na kupika chumvi na pia akina mama wa kijiji cha Senkenke wanaojishughulisha na uchimbaji wa madini ya dhahabu wanafanya kazi zao katika mazingira magumu sana kwa sababu hawana vitendea kazi muhimu. Je, Serikali au Wizara ipo tayari kuwasaidia akina mama hawa katika vijiji hivi kusudi wafanye kazi zao kwa urahisi na kwa faida zaidi? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nitoe pongezi za dhati kabisa kwa akina mama hawa ambao wanafanya kazi zao za kujipatia kipato halali. *(Makofi)*

Pili, kwa kutambua hilo, Serikali imekuwa ikihakikisha kwamba ofisi za madini za kanda ikiwepo ile ya Singida inatoa mafunzo, maelekezo ili kazi hizo ziweze kufanywa kwa utaalum.

Kutokana na swali la Mheshimiwa Mbunge, nitachukua hatua ya kuwakumbusha Maafisa wa Madini waende tena mahususi kwenye maeneo hayo ili wakaendeleo kutoa

mafunzo kwa akina mama hawa na pia wawaelekeze ni namna gani basi wanaweza kujitahidi kupata vifaa kuwaelekeza mahali ambapo vifaa vinaweza kupatikana.

Na. 79

Umeme Nyatwali

MHE. DR. RAPHEL M. CHEGENI (K.n.y. MHE. TEMBE K. NYABURI)
aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kupeleka umeme kijiji cha Nyatwali kabla ya mwaka 2000 na kwa kuwa mnamo mwaka 2002/2003 ujenzi wa njia ya umeme ulianza na kukomea kuchimbia nguzo tu bila kuweka waya na hadi sasa kazi hiyo haijakamilika:-

- (a) Je, kwa nini mradi huo umesimama bila kukamilika kwa zaidi ya miaka miwili sasa?
- (b) Je, wananchi wa Nyatwali watarajie nini na ni lini mradi huo muhimu utakamilika?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyaburi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

- (a) Mradi wa upelekaji umeme kijiji cha Nyatwali ulikuwa ni sehemu ya upelekaji umeme kwenye mji mdogo wa Lamadi. Upelekaji umeme katika mji mdogo wa Lamadi ulikamilika mwaka 2003. Gharama za mradi wa Lamadi pamoja na kijiji cha Nyatwali zilikadiriwa kuwa jumla ya kiasi cha shilingi 140 milioni.

Baada ya kukamilika mradi wa umeme Lamadi, Shirika la Umeme lilianza ujenzi wa njia ya umeme ya kijiji cha Nyatwali. Hata hivyo kutokana na matatizo ya ufinyu wa bajeti unaolikabili Shirika la Umeme, uendelezaji wa ujenzi wa njia ya umeme kwa ajili ya kijiji cha Nyatwali ulisimama kwa muda. Ujenzi wa nguzo kwa ajili ya kijiji cha Nyatwali umekamilika kwa kiasi cha asilimia 80. Vifaa vingine kwa ajili ya kukamilisha mradi wa umeme kijiji cha Nyatwali vimepatikana isipokuwa nyaya kwa ajili ya ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33 na nyingine kiasi cha mita 10,000.

- (b) Shirika la umeme linategemea kukamilisha ujenzi wa njia ya umeme kijiji cha Nyatwali katika muda wa miezi miwili, mara baada ya kupata nyaya za msongo 33 na urefu wa mita 10,000.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika Bunge lililopita kazi ya kupeleka umeme Nyatwali itahusisha pia kazi ya kufikisha umeme toka Lamadi hadi Nyashimo kupitia Kalemela-Nyamikoma na Kabita kwenye Jimbo la Busega la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni Msabaha. *(Kicheko/Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaarifu kwamba muda wa maswali umekwisha, kwa hiyo msamehe maswali ya nyongeza.

MHE. DR. RAPHAEL MASUNGA CHEGENI: Mheshimiwa Spika, kusahihisha tu kidogo ili Hansard ikae vizuri.

SPIKA: Haya, endelea na masahihisho.

MHE. DR. RAPHAEL MASUNGA CHEGENI: Sio Raphael Msabaha ni Dr. Raphael Masunga Chegeni na siyo Dr. Raphael Chegeni. Msabaha. *(Kicheko)*

SPIKA: Haya.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, kama kawaida kuna matangazo ya vikao lakini kwa leo kuna kikao kimoja cha Kamati ya Fedha na Uchumi. Mwenyekiti wake anawaarifu wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 16/6/2005 kitafanyika kikao cha Kamati saa tisa mchana katika chumba Na.428, jengo la utawala.

Baada ya tangazo la kikao, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba sasa kwa mujibu wa ratiba yetu tumerudi nyuma siku moja moja. Chief Whip wa Serikali ameshawaambia Mawaziri wajiandae kuwa tayari kwa ratiba iliyorekebishwa.

Sasa na mimi napenda kuwambusha Wenyeviti wa Kamati na Wasemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba wawe tayari siku moja kabla ukilinganisha na ratiba iliyotolewa.

Mwisho wa matangazo Waheshimiwa Wabunge, Katibu endelea na ajenda inayofuata!

HOJA ZA SERIKALI

SPIKA: Leo ni zamu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu hapimiwi muda wa kutoa Hotuba yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa namwita Mtoa Hoja Mheshimiwa Waziri Mkuu awasilishe Makadirio ya Ofisi yake. *(Makofi)*

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006 Ofisi ya Waziri Mkuu

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili taarifa ya mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali na mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2004/2005 na mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2005/2006. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Asasi zilizo chini yake na yale ya Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kwa takriban siku tano Waheshimiwa Wabunge wamejadili na hatimaye kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2005/2006 pamoja na taarifa kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa mwaka 2004 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2005/2006. Napenda kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha, kwa hotuba zao na kwa jinsi walivyoweza kutoa maelezo kuhusu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Ninawashukuru vilevile Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri ambayo itaisaidia sana Serikali wakati wa utekelezaji wa Bajeti na Mpango wa mwaka 2005/2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge lako Tukufu kwa kuchambua Bajeti na Mpango wa Maendeleo wa Serikali wa Mwaka 2005/2006 na kutoa ushauri kwa Serikali wa namna ya kuboresha upangaji na utekelezaji wa Bajeti na Mpango huo. Kama ilivyokuwa kwa muda wote wa Serikali ya Awamu ya Tatu, wadau wengi wamepata fursa ya kushiriki katika hatua mbalimbali za utayarishaji wa Bajeti na Mpango wa Serikali. Napenda niwashukuru wote kwa michango yao. Ninazishukuru vilevile Kamati za Kudumu za Bunge lako Tukufu kwa kupitia Makadirio ya Matumizi ya kila Wizara, Ofisi na Idara za Serikali zinazojitegemea na kwa michango na ushauri uliotolewa. Natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Katiba, Sheria na

Utawala chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kupitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 2 Juni, 2005 tulimpoteza Mbunge mwenzetu marehemu Abu Towegale Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kilombero. Napenda kutumia fursa hii kuwapa pole ndugu na wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa msiba huo mkubwa. Kifo chake kimefanya idadi ya Wabunge wenzetu waliofariki katika kipindi cha mwaka 2004/2005 kufikia watano. Wabunge wengine waliofariki ni marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Raha Leo; marehemu Kapteni Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ulanga Mashariki; marehemu Frank Michael Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki na marehemu Yete Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini. Kwa mara nyingine tena napenda kuwapa pole ndugu, wanafamilia na wananchi wa majimbo hayo kwa misiba hiyo. Tutaendelea kuwakumbuka marehemu hao kwa michango yao ndani na nje ya Bunge lako Tukufu ambayo ililenga katika kuleta maendeleo kwa wananchi wa Majimbo yao na Taifa kwa jumla. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nampongeza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake makini ulioiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuweza kila mara kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu hoja mbalimbali ambazo zimeliwezesha Bunge kutoa maamuzi muhimu kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu. Akiwa sehemu ya Bunge hili, Rais ametia sainsi Miswada yote ya sheria iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu. Vilevile, ameweza kuongoza na kusimamia kwa makini utekelezaji wa ahadi za Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa wananchi. Tunampongeza na kumshukuru kwa kazi nzuri aliyowafanyia Watanzania na tunamtakia maisha mema na marefu. Tarehe 4 Mei 2005, Mkutano Mkuu wa CCM ulimteua Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kuwa mgombea wa kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM iliidhinisha uteuzi wa Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein kuwa mgombea mwenza. Aidha, kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM kilimteua Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuwa mgombea wa kiti cha Rais wa Zanzibar. (*Makofi*)

Napenda kutumia fursa hii kwa mara nyingine tena kuwapongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuteuliwa kubeba bendera ya CCM katika Uchaguzi Mkuu ujao. Furaha na shamrashamra zilizorindima nchi nzima mara baada ya teuzi hizo, zinaashiria na kutupa imani kuwa CCM itapata ushindi mkubwa kwenye Uchaguzi Mkuu ujao. Furaha na shamrashamra zilizorindima nchi nzima mara baada ya uteuzi huo, zinaashiria na kutupa imani kuwa CCM itapata ushindi mkubwa kwenye Uchaguzi Mkuu ujao.

Napenda vilevile kuipongeza CCM kwa kuendelea kuwa Mwalimu wa demokrasia nchini. Kufanikiwa kwa mkutano wake mkuu kumetokana na jinsi CCM

ilivyojizatiti kujenga misingi imara ya demokrasia ndani ya Chama. Bila shaka baadhi ya vyama vya siasa vitakuwa na mambo ya kujifunza kutokana na mchakato wa CCM wa kupata mgombea wake wa kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano na kile cha Rais wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vyama vya *Civic United Front (CUF)*, *Tanzania Labour Party (TLP)*, *National League for Democracy (NLD)*, *CHAUSTA*, *United Democratic Party (UDP)* na Jahazi Asilia navyo vimefanya uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wagombea wenza na baadhi ya vyama kuteua wagombea wa kiti cha Rais wa Zanzibar. Napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Ibrahim Haruna Lipumba; Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema; Mheshimiwa Dr. Emmanuel Makaidi; Mheshimiwa James Mapalala na Mheshimiwa John Momose Cheyo kwa kuteuliwa na vyama vyao kuwa wagombea wa kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad na Mheshimiwa Musa Haji Kitole kwa kuteuliwa na vyama vyao kuwa wagombea wa kiti cha Rais wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu imefanya kazi kubwa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita. Yapo mafanikio mengi yanayoonekana katika nyanja ya siasa na sekta mbalimbali zinazogusa maendeleo na ustawi wa Taifa letu. Katika mkutano huu, Bunge lako Tukufu litapata maelezo na taarifa kuhusu mafanikio hayo. Mafanikio hayo ni kielelezo cha utekelezaji wa sera sahihi za CCM zinazolenga kukuza uchumi na kuondoa umaskini kama zilivyoielezwa katika Ilani za Uchaguzi wa CCM za mwaka 1995 na mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi ya Serikali ya Awamu ya Tatu, shughuli za kisiasa nchini zimeendelea kutekelezwa kwa amani na utulivu chini ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa. Hali hiyo imewezesha vyama vyenye usajili wa kudumu kushiriki katika chaguzi mbalimbali zilizofanyika kati ya mwaka 1995 na 2000. Chaguzi hizo ziliendeshwa kwa uhuru na haki chini ya usimamizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Aidha, katika kipindi hicho viongozi wa vyama vya siasa wameweza kufanya ziara mbalimbali nchini zilizowawezesha kufanya mikutano ya hadhara na kutafuta wanachama wapya. Nchi yetu imeweza kufanya chaguzi kuu mbili chini ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi yaani mwaka 1995 na 2000 ambapo vyama 13 vya siasa vilishiriki na mara zote Chama cha Mapinduzi kilishinda na kuunda Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. (*Makofi*)

Serikali imefanikiwa kuweka mazingira yaliyowezesha kuongezeka kwa idadi ya vyama kutoka vyama 13 mwaka 1995 hadi 18 mwaka 2005. Mazingira hayo ni pamoja na kutoa uhuru wa kueneza sera zao na kutoa ruzuku kwa vyama vinavyostahili kisheria ili vitekeleze majukumu yao. Katika mwaka 2004/2005, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imetoa usajili wa kudumu kwa vyama viwili vya Jahazi Asilia na Sauti ya Umma. Baadhi ya vyama vilivyokuwa na usajili wa muda vilifutwa kwa mujibu wa sheria kwa kushindwa kutekeleza masharti ya maombi ya usajili wa kudumu. Vyama hivyo ni Chama cha Umoja Tanzania (*CHAUTA*), *Union for Liberation Movement (ULIMO)*, *Solidarity of Factual Theory (SOFT)*, Siasa Safi na *Tanzania Peoples Congress (TPC)*.

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa pia imesimamia na kuhakikisha matakwa ya sheria ya kujenga demokrasia ndani ya vyama vya siasa yanafuatwa. Mwezi Novemba 2004, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ngazi za vijiji, vitongoji na mitaa uliosimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, ulifanyika nchini kote Tanzania Bara. Jumla ya vyama vilivyoshiriki katika uchaguzi huo ni 16. Katika uchaguzi wa wenyeviti wa vitongoji, kati ya viti 54,094, CCM ilipata asilimia 92.37; CUF asilimia 3.94 na CHADEMA asilimia 1.02. (*Makofi*)

Kwa upande wa uchaguzi wa wenyeviti wa vijiji, kati ya viti 10,066, CCM ilipata asilimia 93.9; CUF asilimia 2.9 na TLP asilimia 1.1. Kwa upande wa uchaguzi wa wenyeviti wa mitaa, kati ya viti 2,628, CCM ilipata asilimia 88.28; CUF asilimia 6.01 na CHADEMA 4.53. Katika uchaguzi wa Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji, kati ya Wajumbe 161,902, CCM ilipata asilimia 92.76 na CUF asilimia 3.99. Vyama 13 vilivyobaki vilipata viti vichache ambavyo ni chini ya asilimia moja. (*Makofi*)

Katika maeneo mengi nchini, uchaguzi huo uliendeshwa kwa amani na utulivu isipokuwa katika maeneo machache hasa ya mijini ambapo kulijitokeza vurugu na fujo zilizosababishwa na baadhi ya wanasisia ambao walifanya hivyo kwa maslahi yao binafsi. Navipongeza vyama vyote vilivyoshiriki chaguzi hizo. Kipekee naipongeza CCM kwa ushindi mkubwa kwenye chaguzi za ngazi zote za Serikali za Mitaa. (*Makofi*)

Aidha, napenda kutoa wito kwa viongozi wa vyama vya siasa na Watanzania wote kujihadhari na kukwepa kuanzisha fujo na ghasia katika uchaguzi kwani watakuwa wanakwamisha mchakato wa kidemokrasia.

Mheshimiwa Spika, moja ya mafanikio makubwa yaliyopatikana kuhusiana na shughuli za uchaguzi, ni uanzishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Kazi ya uandikishaji ilianza rasmi katika Kanda ya Kusini tarehe 7 Oktoba, 2004 na kuhitimishwa rasmi tarehe 10 Mei, 2005 huko Zanzibar. Kwa jumla, zoezi la uandikishaji wapiga kura limefanyika vizuri. Kwa mujibu wa Taarifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, watu 15,942,824 wameandikishwa Tanzania Bara kati ya watu au lengo la watu 16,570,230 waliotarajiwa kuandikishwa. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 96.2.

Tume inaendelea kukamilisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili liwe tayari kutumika katika Uchaguzi Mkuu, mwezi Oktoba, 2005. Kwa mujibu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, idadi ya wananchi waliojiandikisha katika chaguzi hizo imekuwa ikiongezeka kutoka Watanzania 8,929,969 mwaka 1995; 10,088,484 mwaka 2000 na sasa 15,942,824 mwaka 2005. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu unaendelea kuimarika siku hadi siku. Kero zilizopo ni sehemu ya mchakato wa maendeleo unaotokana na juhudi za kuendeleza mshikamano na undugu uliopo baina ya wananchi wa pande zote mbili. Serikali zote mbili zimechukua hatua za kuimarisha na kuondoa kero mbalimbali za Muungano. Hatua hizo ni pamoja na Asasi za Muungano kujenga na kufungua Ofisi katika pande zote za

Muungano. Asasi hizo ni Benki Kuu ya Tanzania, Ofisi ya Bunge, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Kituo cha Utafiti wa Viumbe wa Baharini. (*Makofi*)

Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imefungua akaunti katika Benki Kuu ya Tanzania na hivyo kuendelea kupata huduma za Benki hiyo ikiwemo gawio la mapato ya Benki na misaada ya wafadhili na wahisani la asilimia 4.5. Vile vile, Tume ya Pamoja ya Fedha imeundwa kufuatia mapendekezo ya Tume ya Kuondoa Kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Kamati ya Wataalam ya kushughulikia maeneo ya Muungano yenye matatizo ya matumizi ya rasilimali za pamoja, hasa mafuta, gesi, madini, uvuvi na samaki katika Bahari Kuu, iliundwa na imewasilisha mapendekezo yake Serikalini. Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zimeendelea kuwasiliana na kujadiliana, ili kuweza kukubaliana namna ya kuondoa kero zilizobainishwa na kamati hiyo. Kadhalika vikao vya ushirikiano kati ya Wizara, Taasisi na Asasi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar vinaendelea kufanyika, na masuala mengi yameweza kutatuliwa kwa mashauriano ya kidugu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mazingira mazuri yaliyoliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba inavyostahili. Kutokana na hali hiyo, katika kipindi cha miaka kumi, Bunge limetunga sheria 201 na kupitisha maazimio na itifaki 153. Hatua mbalimbali zimechukuliwa kuboresha utendaji wa Bunge. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha shughuli za uchapishaji wa kumbukumbu za kila siku (*Hansard*), kuanzishwa kwa maktaba ya kisasa ya Bunge yenye kompyuta na mtandao wa Intaneti, kuanzishwa kwa tovuti ya Bunge na kukarabatiwa Ofisi za Bunge Dar es Salaam na Zanzibar. Katika mwaka 2004/2005, zoezi la kukarabati Ofisi ya Bunge Dar es Salaam na Zanzibar limeendelea. Aidha, ujenzi wa ukumbi mpya wa Bunge Dodoma nao umeanza. Ili tuweze kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Serikali imeandaa na kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali. Mipango na Mikakati hiyo ina lengo la kuondoa umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2025 na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata maisha bora na mazuri, upo uongozi bora na utawala wa sheria na tunajenga uchumi imara wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani. Serikali imechukua hatua za kutunga na kuhuisha sera ya uchumi jumla na sera za fedha zinazolenga katika kutengeneza vigezo muhimu vya uchumi ili kujenga uchumi imara, unaokua na wenye ushindani. Vile vile, sheria na kanuni zimetungwa ili kuongoza taratibu za uwekezaji rasilimali nchini pamoja na kusimamia na kudhibiti uchumi wa soko huria. Hatua hizo zimewezesha ukuaji halisi wa Pato la Taifa kufikia asilimia 6.7 mwaka 2004 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.6 mwaka 1995. Aidha, kasi ya upandaji bei nayo iliendelea kudhibitiwa na kufikia kiwango cha wastani wa asilimia 4.1 kwa mwaka ikilinganishwa na kiwango cha wastani wa asilimia 27.1 mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza mapato, Serikali imeboresha sera za mapato na matumizi kwa kiwango kikubwa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuwa na mfumo mzuri na maandalizi ya bajeti na usimamizi wake, kuboresha mfumo wa kodi ambapo kodi mbalimbali zimeainishwa na zingine zenye tija ndogo na kero kwa wananchi zimefutwa ikiwemo kodi ya maendeleo. Hatua hizo zimewezesha mapato ya Serikali

kutokana na kodi na ada mbalimbali kuongezeka hadi kufikia wastani wa shilingi 145 bilioni kwa mwezi katika mwaka 2004/2005 ikilinganishwa na mapato ya wastani wa shilingi 37 bilioni kwa mwezi kwa kipindi kama hicho mwaka 1995/1996. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imekiimarisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania ili kiweze kuhamasisha na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa kuboresha vivutio, kujenga mazingira bora ya uwekezaji, kutangaza fursa na vivutio vya uwekezaji na kuoanisha miradi ya ndani na wawekezaji kutoka nje ya nchi. Aidha, Kituo cha Uwekezaji kimepunguza kwa kiasi kikubwa urasimu na hivyo kuongeza ufanisi na kuboresha utendaji uliowezesha kutolewa kwa huduma zote muhimu katika eneo moja. Mwezi Novemba 2004, kituo kilipata tuzo ya kuwa mshindi wa Kituo Bora cha Uwekezaji Barani Afrika na hivyo kufanya Tanzania kuwa mojawapo ya nchi zinazoongoza katika Bara la Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, kwa kuvutia wawekezaji wengi kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi hizo, kituo cha uwekezaji kimeidhinisha jumla ya miradi 2,436 yenye thamani ya Shilingi 8,245 bilioni inayokadiriwa kutoa nafasi za ajira 457,132. Miradi 1,057 sawa na asilimia 43.4 inamilikiwa na wawekezaji wa ndani, miradi 643 sawa na asilimia 26.4 inamilikiwa na wawekezaji wa nje, na miradi 736 sawa na asilimia 30.2 ni ya ubia baina ya wawekezaji wa ndani na wa nje. Aidha, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ya nchi, umeongezeka kutoka Dola za Marekani 150.0 milioni mwaka 1995 hadi Dola za Marekani 260.2 milioni mwaka 2004. Utekelezaji wa sera ya kurekebisha na kubinafsisha mashirika ya umma umeendelea kuwa na ufanisi ambapo hadi Aprili 2005, mashirika yapatayo 312 yalikuwa yamebinafsishwa. Aidha, mali za mashirika zisizohusiana moja kwa moja na uzalishaji zilizouzwa ni 499. Mashirika mengi yaliyobinafsishwa yanafanya kazi vizuri baada ya kufufuliwa.

Katika zoezi hilo, Watanzania wengi wamepata fursa ya kushiriki katika uwekezaji ambapo hadi Aprili 2005, mashirika yapatayo 160 yalikuwa yamenunuliwa kwa asilimia 100 na Watanzania. Mashirika 24 yalinunuliwa na wawekezaji wa nje na mengine yaliyobaki 128 yalinunuliwa kwa njia ya ubia baina ya Serikali na wawekezaji wa ndani na nje. Vilevile, hadi Desemba, 2004 zaidi ya wananchi 67,081 walikuwa wamenunua hisa kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam katika mashirika yaliyobinafsishwa na hivi sasa wanapata gawio kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu iliandaa na kutekeleza programu mbalimbali za kuboresha utawala na uongozi Serikalini na kuboresha Serikali za Mitaa. Chini ya Programu ya Kuboresha Utumishi Serikalini, Serikali imejiiondoa katika uendeshaji wa baadhi ya majukumu, na hivyo kupunguza miundo ya idara kwa asilimia 20. Katika kutekeleza Sera ya Menejimenti ya Ajira, Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 ilitungwa kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji wa taasisi na watumishi wote katika sehemu za kazi na kuweka taratibu za ajira zenye kujali ushindani, uwazi na sifa.

Sheria ya Maadili ya Viongozi ya mwaka 1995 pamoja na marekebisho yake imewezesha kuundwa kwa chombo cha kuratibu na kusimamia maadili ya viongozi na watendaji wakuu wa Serikali. Vilevile, Serikali imetekeleza mpango wa kuboresha maslahi ya watumishi wake kwa kuongeza mishahara, kuhuisha miundo ya utumishi, kuongeza motisha na kutunza vizuri kumbukumbu zao na hivyo kuondoa usumbufu hasa wakati wa kustaafu. Kima cha chini cha mishahara kwa watumishi wa Serikali kimeongezeka kutoka shilingi 17,500 kwa mwezi mwaka 1995/1996 hadi shilingi 60,000 kwa mwezi mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Serikali za Mitaa zimeimarishwa nchini kwa kuandaa na kutekeleza Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa. Programu hiyo iliyoanza kutekelezwa mwaka 2000, imewezesha kuongezeka kwa kiwango cha ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri kutoka sh.21.9bn/= mwaka 1996 hadi sh. 55.2bn/= mwaka 2003. Makusanyo hayo yalishuka na kufikia sh. 20.8bn/= Mei 2005 kutokana na kufutwa kwa baadhi ya kodi zenye kero. Hata hivyo, Serikali imeweka utaratibu wa kufidia pengo hilo. Aidha, Serikali ilirekebisha muundo wa Jiji la Dar es Salaam na kuanzisha muundo wenye Jiji na Manispaa tatu za Kinondoni, Ilala na Temeke. Hatua hiyo imeweka misingi bora ya utendaji, ukusanyaji wa mapato, usafi wa mazingira, ujenzi wa miundombinu ya barabara pamoja na utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii. Jiji limepata sura mpya ya kuvutia na kutuletea sifa nyingi kuliko miaka kumi iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uimarishaji huduma Mijini, Serikali ilianza kutekeleza Programu ya Uimarishaji wa Huduma Mijini mwaka 1997 kwa lengo la kutengeneza na kukarabati miundombinu muhimu ya barabara, vituo vya mabasi, mifereji ya maji machafu na maji ya mvua na maeneo ya kutupia taka. Programu hiyo ilitekelezwa katika Manispaa za Arusha, Iringa, Moshi, Mbeya, Morogoro, Tabora, Tanga na katika Majiji ya Mwanza na Dar es Salaam ambapo jumla ya kilometa 116.5 za barabara na vituo 12 vya mabasi vilijengwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha maeneo mapya ya utawala ili kupeleka huduma karibu na wananchi, kurahisisha utendaji na kufanikisha utawala bora. Maeneo hayo ni pamoja na Mkoa mpya wa Manyara na Wilaya nane za Kilindi, Nyamagana, Ilemela, Namtumbo, Kishapu, Kilolo, Uyui na Mvomero. Serikali vilevile ilianzisha mamlaka mpya za Halmashauri za Wilaya za Bukombe, Misungwi, Sikonge, Kongwa, Karatu, Mkuranga, Ruangwa, Tandahimba na Mbarali. Halmashauri mpya za Miji zilizoundwa ni za Korogwe, Kibaha na Babati. Aidha, Mji wa Shinyanga ulipewa hadhi ya Manispaa na Manispaa ya Mwanza kuwa Jiji. Kadhalika, Tarafa mpya nane, Kata 17 ziliundwa na Vijiji vipya 155 vilisajiliwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuziwezesha Mahakama kusimamia utekelezaji wa sheria na kulinda haki za raia. Ujenzi wa majengo kwa ajili ya Mahakama katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Mbeya, Iringa na Moshi ulikamilishwa. Vilevile, ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya za Kongwa, Ludewa, Sumbawanga na Mbarali na ya Mahakama za Mwanzo 13 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Manyara, Kilimanjaro, Iringa, Shinyanga na Tanga ulikamilishwa. Mahakama ya Biashara na

Mahakama ya Ardhi nazo zimeanzishwa. Aidha, Serikali iliwezesha Mahakama ya Tanzania kuanzisha Chuo cha Uongozi wa Mahakama huko Lushoto. Ili kuwezesha Mahakama kukabiliana na ongezeko la majukumu, idadi ya Majaji na Mahakimu imeongezwa. Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wameongezeka kutoka 564 mwaka 1995 hadi 680 Desemba 2004. Aidha, idadi ya Mahakimu wa Wilaya, Mahakimu Wakazi na Majaji imeongezeka kutoka 192 mwaka 1995 hadi 319 mwaka 2004. Serikali vilevile imeanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora mwaka 2001 kwa lengo la kushughulikia kero za wananchi zinazohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza sekta ya kilimo, Serikali ilianzisha programu mbalimbali zilizowezesha kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uzalishaji katika kilimo. Baadhi ya programu hizo ni pamoja na Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo, Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji na Mipango ya Wilaya ya Maendeleo ya Kilimo. Kutokana na utekelezaji wa mipango hiyo, kilimo kimeendelea kukua kutoka kiwango cha chini cha asilimia 1.9 mwaka 1998 na kufikia asilimia 6 mwaka 2004. Chini ya Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji, hadi mwaka 2004/2005 jumla ya hekta 250,573 zimeendelezwa ikilinganishwa na hekta 143,000 mwaka 1995/1996.

Serikali pia imeweka kipaumbele katika upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo. Upatikanaji wa mbegu bora za mazao ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta umeongezeka kutoka tani 2,750 mwaka 1995/1996 hadi tani 10,650 mwaka 2003/2004 sawa na ongezeko la asilimia 287.

Kwa upande mwingine, kampuni za watu binafsi zinazofanya biashara ya mbegu bora ziliongezeka katika kipindi hicho kutoka kampuni mbili hadi 18. Kwa kuzingatia mchango wa sekta ya kilimo katika kuondoa umaskini na kuhakikisha kuwa Taifa linajitosheleza kwa chakula, katika msimu wa mwaka 2003/2004, Serikali ilirejesha utaratibu wa kutoa ruzuku ya mbolea kwa kutenga jumla ya Shilingi 2 bilioni kwa ajili ya ruzuku ya usafirishaji wa mbolea kwa baadhi ya mikoa nchini. Ruzuku hiyo iliongezwa hadi kufikia shilingi 7.244 bilioni mwaka 2004/2005. Hadi mwishoni mwa mwezi Aprili 2005, kiasi cha tani 72,883.67 za aina mbalimbali za mbolea sawa na asilimia 89.1 ya lengo, zilisambazwa na kuuzwa kwa wakulima kupitia vituo 14.

Mheshimiwa Spika, kulingana na takwimu za mwaka 2002, Tanzania ilikadiriwa kuwa na ng'ombe 17.7 milioni, mbuzi 12.5 milioni, kondoo 3.5 milioni. Takwimu hizo pia zinaonyesha kwamba idadi ya mifugo ya aina zote imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 1.7 kwa ng'ombe wa kienyeji, asilimia 4.6 kwa ng'ombe wa maziwa, na asilimia mbili kwa mbuzi na kondoo. Serikali imetekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo, ambapo kati ya mwaka 2001 hadi 2004 ilinunua chanjo 20,240,000 za kudhibiti ugonjwa hatari wa homa ya mapafu na kuweza kupunguza vifo vya mifugo kutokana na ugonjwa huo kutoka 3,590 mwaka 1996 hadi 696 mwaka 2003. Tanzania imefanikiwa kutokomeza ugonjwa wa sotoka nchini, hali ambayo ilithibitishwa na Shirika la Afya ya Mifugo Duniani. Kati ya mwaka 2000 na 2004, Serikali imekarabati

malambo 250, na kujenga machinjio kubwa na ya kisasa pamoja na Chuo cha Ukataji Nyama katika Manispaa ya Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua za kisera na kisheria kuhakikisha kuwa ushirika unastawi na kuendelezwa nchini kama njia muhimu ya kuwawezesha wananchi kuondokana na umaskini. Sera ya Ushirika ya mwaka 2002 na Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003, zina lengo la kujenga ushirika shirikishi, endelevu na unaostahimili nguvu za soko. Katika kutekeleza Programu za Mageuzi ya Ushirika, kumekuwepo na ongezeko la Vyama vya Ushirika wa akiba na mikopo kutoka vyama 803 mwaka 1995 hadi 1,719 Desemba 2004, likiwa ni ongezeko la asilimia 112. Aidha, hisa za wanachama zimeongezeka kutoka shilingi 7.4 bilioni mwaka 1995 hadi shilingi 16.1 bilioni mwaka 2004. Vilevile, wanaushirika wamehamasishwa kuanzisha benki zao ambapo wanaushirika wa Mikoa ya Kilimanjaro na Kagera wameanzisha benki. Pamoja na hayo, Serikali imeanzisha utaratibu wa kutoa dhamana ya mikopo ili Vyama vya Ushirika viweze kununua mazao ya wakulima. Vyama sita vimefaidika na utaratibu huo na kupata mkopo wa jumla ya sh.12.48b/= . Marejesho ya mkopo huo umekuwa wa kuridhisha na kuonyesha kuwa vyama vya ushirika vinakopesheka.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya mabadiliko makubwa katika usimamizi na uendeshaji wa sekta ya madini nchini ili kuiwezesha sekta binafsi kumiliki na kuendeleza taasisi zinazoshughulika na utafutaji na uchimbaji wa madini. Serikali iliandaa Sera ya Madini ya Mwaka 1997 ambayo ilifuatiwa na kutungwa kwa Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 na kanuni zilizotolewa mwaka 1999. Hatua hizo ziliboresha mazingira ya uwekezaji ambapo leseni za utafutaji wa madini ziliongezeka kutoka 113 mwaka 1995 hadi leseni 2,200 mwaka 2004. Aidha, kuanzia mwaka 1995 hadi Mei 2005, jumla ya Dola za Marekani 1.4 bilioni zimewekezwa katika sekta ya madini sambamba na kufunguliwa kwa migodi sita mikubwa ya dhahabu ya Lusu-Nzega, Geita, Bulyankulu, Tarime, Buhemba na Tulawaka, hivyo kuongeza uzalishaji wa dhahabu kutoka kilo 320 mwaka 1995 hadi tani 46.2 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa nao umeongezeka kutoka asilimia 1.4 mwaka 1995 hadi asilimia 3.2 mwaka 2004. Kwa jumla sekta ya madini imekua kutoka asilimia 9.7 mwaka 1996 hadi asilimia 15.6 mwaka 2004. Kwa upande wa fedha za kigeni mchango wa sekta ya madini uliongezeka kutoka Dola za Marekani 44.88 milioni mwaka 1995 hadi kufikia Dola za Marekani 686.5 milioni mwaka 2004. Maduhuli ya Serikali kutokana na ada za leseni na mrabaha kwa watafutaji na wachimbaji wa madini, yaliongezeka kutoka sh. 432m/= mwaka 1995/1996 hadi sh. 22,786m/= mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa sekta ya madini, na kwa kuitikia ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge, katika mwaka 2004, Serikali iliunda Kamati ya Kudurusu Sera ya Madini kwa lengo la kuangalia taratibu za uwekezaji kwenye sekta hiyo. Taratibu hizo zinahusu umiliki wa hisa kwenye migodi, mfumo wa kodi, vivutio kwa wawekezaji, uwezekano wa kuongeza thamani ya madini kabla ya kuyasafirisha nje, kuimarisha usimamizi wa shughuli za uchimbaji na utoaji huduma kwa wachimbaji wadogo, kuwa na namna bora ya kuondoa vikwazo kwenye biashara ya

madini na kuondoa migongano kati ya wadau wa shughuli za madini. Kamati hiyo iliwasilisha taarifa yake mwezi Februari, 2005 na Waheshimiwa Wabunge walipatiwa nakala za taarifa hiyo. Serikali inayafanyia kazi mapendekezo yaliyopo kwenye taarifa hiyo kwa lengo la kuboresha utendaji katika sekta ya madini ili Taifa letu lifaidike zaidi na mapato yatokanayo na madini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilibuni Mpango wa Miaka Kumi wa Kuendeleza Uvuvi ulioanza kutekelezwa mwaka 2002. Mpango huo umewezesha kutoa elimu kwa wafugaji wa samaki, kujengwa kwa mabwawa ya samaki, kusindikwa kwa mazao ya samaki na kujengwa kwa masoko ya samaki ya kisasa Dar es Salaam na Mwanza. Aidha, Watanzania wenye uwezo wamehimizwa na kutiwa moyo ili waweze kutumia vyema na kwa ufanisi Ukanda wa Uchumi wa Bahari. Serikali vile vile iliendelea kulinda rasilimali za uvuvi dhidi ya uvuvi usio endelevu kwa kuimarisha doria za majini na nchi kavu, kushirikisha jamii katika kusimamia rasilimali hiyo na kuelimisha jamii juu ya ufugaji wa samaki. Kutokana na juhudi hizo, maduhuli yatokanayo na biashara ya uvuvi yameongezeka kutoka sh. 630m/= mwaka 1995 hadi kufikia sh.9.7bn/= mwaka 2003/2004. Aidha, biashara ya samaki na mazao ya uvuvi ndani na nje ya nchi iliongezeka kutoka sh. 11.9bn/= mwaka 1995 hadi sh. 132bn/= mwaka 2003. Viwanda 12 vya kusindika samaki vilijengwa katika Ukanda wa Ziwa Victoria na 17 katika ukanda wa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa utalii, Serikali iliandaa na kutekeleza Mpango Kabambe wa Utalii unaohusu kuendeleza vivutio asilia vya utalii na kubaini vipya, kuboresha miundombinu, kutafiti masoko na kutangaza mazao ya utalii kwa kutumia vyombo vya habari, Ofisi za Balozi zetu nje na kushiriki maonyesho mbalimbali duniani. Kutokana na juhudi hizo, mapato yatokanayo na utalii yaliongezeka kutoka Dola za Marekani 258.14 milioni mwaka 1995 hadi Dola za Marekani 746.1 milioni mwaka 2004. Idadi ya watalii waliotembelea nchi yetu imeongezeka kutoka 295,000 mwaka 1995 hadi 582,000 mwaka 2004. Vile vile, mapato ya uwindaji wa kitalii yaliongezeka kutoka Dola za Marekani 7.3 milioni mwaka 1995/1996 hadi Dola za Marekani 8.8 milioni mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kutekeleza Sera Endelevu ya Viwanda kwa kuweka mkazo katika uendelezaji wa viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuongeza thamani ya mazao na hivyo kukuza mapato kwa wakulima na mapato ya fedha za kigeni kwa kuuza nje ya nchi bidhaa zilizosindikwa badala ya mazao ghafi. Vile vile, Serikali imeendelea kutekeleza Sheria ya Maeneo Maalumu ya Kuzalisha Bidhaa za kuuza nje. Aidha, utekelezaji wa programu za sera za viwanda vidogo na biashara ndogo iliendelea kwa kuanzisha Mfuko wa Dhamana, uendeshaji wa mafunzo ya ujasiriamali, utoaji wa ushauri katika nyanja mbalimbali na huduma za ufundi. Programu ya ubinafsishaji wa viwanda na mashirika ya umma pia imefufua viwanda vingi ambavyo vimeongezwa upatikanaji wa bidhaa na ajira. Kwa mfano, uzalishaji wa nguo uliongezeka kutoka mita za mraba 31.2 milioni mwaka 1995 hadi mita za mraba 107.4 milioni mwaka 2002. Utengenezaji wa bati uliongezeka kutoka tani 18,142 mwaka 1995 hadi tani 41,725 mwaka 2004. Aidha, ajira viwandani imeongezeka kutoka wafanyakazi 126,052 mwaka

1995 hadi wafanyakazi 207,571 mwaka 2003. Vile vile, viwanda vipya vya bidhaa mbalimbali vimeanzishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya mabadiliko makubwa katika uendeshaji wa biashara nchini kwa kuanzisha Sera ya Biashara ya mwaka 2003. Lengo la sera hiyo ni kuondoa vikwazo na urasimu usio na tija ili kuharakisha ukuaji wa sekta ya biashara. Vikwazo vilivyoondolewa ni pamoja na sharti la kulipa kodi ya makisio kabla ya kuanzisha biashara na kutokuwepo uwazi kuhusu masharti ya kuanzisha biashara na viwango vya ada zinazotakiwa. Serikali pia imeanzisha kitengo cha taratibu bora za kusimamia biashara kinachoratibu utekelezaji wa Programu Maalum ya Kuboresha Mazingira ya Kibiashara nchini. Kufuatia hali hiyo, mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi yaliongezeka kutoka Dola za Marekani 682.9 milioni mwaka 1995 hadi Dola za Marekani 1,334.9 milioni mwaka 2004. Sekta ya biashara nayo ilikua kutoka asilimia 3.1 mwaka 1995 hadi asilimia nane mwaka 2004. Mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa ulikua kutoka asilimia 15.4 mwaka 1995 hadi asilimia 17 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005, Serikali imepata mafanikio makubwa katika sekta ya ardhi kufuatia kutungwa kwa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995. Katika kutekeleza sera hiyo, sheria zifuatazo na kanuni zake zilitungwa:-

- Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 na Kanuni zake;
- Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 na Kanuni zake;
- Sheria ya Mahakama za Ardhi Na. 2 ya Mwaka 2002 na Kanuni zake;
- na
- Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ardhi Na. 2 ya Mwaka 2004 na Kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kuboresha mazingira ya matumizi ya ardhi kisera, kisheria na kiutendaji ili kuwawezesha wananchi kuitumia ardhi yao vizuri. Katika kufanya hivyo, Serikali iliendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sera, sheria za ardhi na kanuni zake katika Mikoa na Wilaya mbalimbali nchini na kupima ardhi kwa matumizi mbalimbali Mijini na Vijijini. Serikali hivi sasa inatambua miliki za wananchi kisheria kwenye makazi yaliyojengwa kiholela nchini ili kuwawezesha wananchi kuzitumia rasilimali hizo kujipatia mitaji na kuanzisha miradi ya kujiongezea kipato. Kwa hiyo, maeneo ya makazi holela yanatambuliwa na wamiliki wa nyumba wanapewa leseni za makazi. Katika mwaka 2004/2005, jumla ya nyumba 200,000 zimetambuliwa katika Jiji la Dar es Salaam ambapo inakadiriwa kuwa asilimia 80 ya nyumba ziko katika maeneo yasiyopimwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kutekeleza zoezi la upimaji ardhi Mijini na Vijijini. Katika kipindi cha miaka 10, jumla ya Vijiji 3,999 vilikuwa vimepimwa. Kwa upande wa Mijini, jumla ya viwanja 266,110 vilipimwa. Aidha, Serikali ilibuni mradi maalum wa kuongeza kasi ya kupima viwanja Mijini. Kwa kuanzia, viwanja 27,712 vilipimwa katika Jiji la Dar es Salaam. Vile vile, Serikali iliziwezesha Halmashauri za Wilaya za Kilombero, Mafia, Handeni, Iringa, Njombe, Songea, Tunduru, Mbinga na Kyela kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kutumia mipango shirikishi. Makusanyo ya kodi ya pango la ardhi yameongezeka kutoka sh. 236m/= mwaka

1995/1996 hadi sh. 5.5bn/= mwaka 2003/2004. Serikali vile vile imeanzisha hazina ya ardhi ili kuhamasisha uwekezaji. Vipande 286 vyenye ukubwa wa hekta 416,442 vimependekezwa kuwa hazina ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha shughuli za hifadhi ya mazingira, Sheria mpya ya Mazingira imetungwa na Serikali imeendelea kutekeleza Mikataba mbalimbali ya Kimataifa ya hifadhi na utunzaji wa mazingira nchini. Kwa vile misitu ni rasilimali muhimu katika hifadhi ya mazingira, Serikali kupitia Programu ya Taifa ya Misitu, imewashirikisha wananchi wa Wilaya 13 katika usimamizi shirikishi wa misitu ya Kijiji, Wilaya na ya Kitaifa katika maeneo yao. Juhudi hizo zimewezesha hekta 1,085,300 kuhifadhiwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 1995 hadi Desemba, 2004. Utaratibu huo umepunguza uharibifu unaofanywa na baadhi ya wananchi ambao huvamia maeneo ya misitu kwa ajili ya makazi, malisho ya mifugo, uchomaji mkaa, uchimbaji madini, ujenzi na kilimo. Siku ya Kupanda Miti Kitaifa imeongeza hamasa kubwa ya upandaji miti nchini. Katika kipindi cha 1995/1996 hadi 2004/2005 hekta 13,200 za misitu zilipandwa miti upya na hekta 33,555,000 za miti ya misitu zilihifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nishati ni muhimu katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Sera ya Nishati imewezesha na kutoa fursa kwa sekta binafsi kuchangia katika uzalishaji wa nishati. Kutokana na mabadiliko hayo, uwezo wa kuzalisha umeme nchini umeongezeka kwa asilimia 47 kutoka megawati 587 mwaka 1995 hadi megawati 865 mwaka 2004. Ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa miradi ya umeme wa nguvu za maji ya Kihansi na Pangani pamoja na miradi ya gesi ya Songosongo na mitambo ya mafuta ya IPTL inayotekelezwa na sekta binafsi. Katika juhudi za kusambaza umeme, Vijiji 249, Miji Mikuu ya Wilaya za Geita, Mbarali, Biharamulo na Ngara na Mji Mdogo wa Nkinga Mwasi ilipatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, sekta ya ujenzi ni miongoni mwa sekta muhimu za huduma za kiuchumi yenye mchango mkubwa katika kufanikisha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, Serikali imepata mafanikio makubwa ya kuboreka kwa mtandao wa barabara hasa baada ya kufanya mabadiliko ya muundo wa utendaji katika sekta ndogo ya barabara.

Serikali ilianzisha Wakala wa Barabara (*TANROADS*) uliopewa jukumu la kujenga, kukarabati na kuzifanyia matengenezo barabara kuu na za Mikoa zenye urefu wa kilometa 35,000. Serikali pia ilianzisha Bodi na Mfuko wa Barabara ili kutunza na kugawa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara na Halmashauri za Wilaya na Miji na kusimamia matumizi yake. Kati ya mwaka 1995 na 2005, jumla ya kilomita 1,423 za barabara za lami zilijengwa na hivyo kufanya mtandao wa barabara za lami nchini kuwa kilomita 4,957.

Aidha, Serikali imejenga Daraja la Mkapa katika Mto Rufiji, ambalo linaunganisha Mikoa ya kusini na maeneo mengine ya nchi pamoja na madaraja mengine 23 ya barabara za Tanga-Horohoro (7), *TANZAM* (5) na Tunduru-Sumbawanga (11). Miradi ya ujenzi wa Barabara Kuu iliyokamilika katika mwaka 2004/2005, ni barabara za

Makuyuni hadi Lango la Ngorongoro yenye urefu wa kilometa 77, Chalinze-Morogoro-Melela yenye urefu wa kilometa 129, Mtukula-Muhutwe, kilometa 112, Somanga-Masaninga-Matandu, kilometa 33, TANZAM-Sehemu ya Mlima Kitonga, kilometa 7.64, barabara za Mwanza zenye urefu wa kilometa 58, Shelui-Nzega, kilometa 108 na Kyabakari-Butiama, kilometa 12.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya mabadiliko katika utoaji wa huduma katika sekta ya mawasiliano kwa kuondoa ukiritimba na kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi. Mabadiliko hayo yamewezesha idadi ya kampuni za simu kuongezeka kutoka kampuni mbili mwaka 1995 hadi kufikia kampuni saba mwaka 2004.

Aidha, njia za simu zilizounganishwa zimeongezeka kutoka 90,198 mwaka 1995 hadi 1,836,583 mwaka 2004. Sambamba na ongezeko hilo, idadi ya wateja wenye simu za mkononi imeongezeka kutoka 2,198 mwaka 1995 hadi 1,694,000 mwaka 2004. Vile vile, huduma za intaneti zimeongezeka kufikia watoa huduma 25 na vituo au maduka 4,000 ya intaneti nchini kote.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano imekamilisha ujenzi wa mtambo maalumu wa kudhibiti masafa ili iweze kutekeleza jukumu lake la uratibu na udhibiti wa masafa. Aidha, Serikali iliainisha miradi ya teknolojia ya mawasiliano ya habari Vijijini kwa msaada wa Shirika la Kimataifa la Simu, hivyo kuweza kuanzisha vituo vya mawasiliano vinavyosimamiwa na wanawake katika Miji ya Singida, Mtwara, Morogoro na Mpwapwa. Miradi hiyo ina lengo la kuwawezesha wanawake kuongeza vipato vyao na kuboresha maisha yao na ya jamii kwa jumla na vile vile kutoa huduma ya mawasiliano na upatikanaji wa habari katika sehemu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, usafiri na usafirishaji majini umekuwa wa mafanikio kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu na utunzaji wa mazingira katika bandari zetu. Kati ya mwaka 1995 na 2004, Serikali imepanua lango la Bandari ya Dar es Salaam kufikia upana wa mita 120 na kina cha mita 10.4 na hivyo kuwezesha meli kubwa za uzito wa tani 40,000 kuingia na kutoka bandarini kwa saa 24.

Uboreshaji huo umeipandisha hadhi bandari na umechangia ongezeko la ufanisi na tija na hivyo idadi ya meli zinazolingia bandarini kwa mwaka kuongezeka kutoka 962 mwaka 1995 hadi 1,256 mwaka 2004. Aidha, viwango vya utoaji wa huduma za meli vimeboreshwa.

Katika kitengo cha mizigo ya kawaida, muda wa meli kusubiri kuhudumiwa umeshuka kutoka wastani wa saa 28.48 mwaka 1995 hadi saa 7.12 mwaka 2004. Mafanikio mengine ni pamoja na kupanuliwa kwa gati la mafuta la Kurasini na kuwekwa kwa vifaa muhimu vya kupakua mafuta na vifaa vya kupambana na moto, hali ambayo imeongeza kasi ya upakuaji mafuta na usalama wa bandari.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu imepata mafanikio makubwa katika sekta ya elimu hasa baada ya kuandaa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995. Serikali ilibuni mipango na mikakati iliyowezesha uboreshaji wa utoaji wa elimu ya awali na msingi nchini. Mikakati hiyo pamoja na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEM) umeleta mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu.

Uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza katika shule za msingi uliongezeka kutoka wanafunzi 712,467 mwaka 1995 hadi wanafunzi 1,376,467 mwaka 2005. Ajira ya walimu iliongezeka kutoka walimu 105,280 mwaka 1995 hadi walimu 145,895 mwaka 2004. Idadi ya shule za msingi imeongezeka kutoka 10,927 mwaka 1995 hadi 13,765 mwaka 2005. Vyumba vya madarasa vimeongezeka kutoka 57,708 mwaka 1995 hadi 141,892 mwaka 2004. Nyumba za walimu zimeongezeka kutoka 25,189 mwaka 1995 hadi 44,797 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuimarika kwa uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kutoka kitabu kimoja kwa wanafunzi wanane hadi wastani wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu kuanzia darasa la kwanza hadi la nne na wastani wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watano kwa darasa la tano hadi la saba.

Taaluma katika shule imeimarika ambapo kiwango cha kufaulu kimeongezeka kutoka asilimia 21.3 mwaka 1998 hadi asilimia 48.7 mwaka 2004. Kuhusu elimu ya sekondari, idadi ya shule imeongezeka kutoka 549 mwaka 1995 hadi shule 1,333 mwaka 2004. Ushirikiano wa wananchi na Serikali umewezesha ujenzi wa madarasa ya shule za sekondari 4,932, nyumba za walimu 816, hosteli 260, maabara 315 na maktaba 76.

Mheshimiwa Spika, idadi ya vyuo vikuu vya umma na binafsi vipatavyo 23 vimepata hati za usajili za ngazi mbalimbali kulingana na masharti ya Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu. Idadi ya wanafunzi waliojiunga na vyuo vya elimu ya juu vya umma imeongezeka kutoka wanafunzi 7,785 mwaka 1995/1996 hadi wanafunzi 28,910 mwaka 2003/2004. Aidha, idadi ya wanafunzi wa kike katika vyuo vikuu vya umma imeongezeka kwa asilimia 635 katika kipindi hicho.

Vile vile, idadi ya wanafunzi waliojiunga na vyuo vikuu binafsi imeongezeka kutoka wanafunzi 947 mwaka 1999/2000 hadi wanafunzi 2,764 mwaka 2003/2004. Wanafunzi waliojiunga na vyuo vya ufundi vya umma iliongezeka kutoka 1,896 mwaka 1995/1996 hadi wanafunzi 2,103 mwaka 2003/2004 sawa na asilimia 11 na idadi ya wanafunzi wa kike waliojiunga na vyuo hivyo iliongezeka kwa asilimia 109. Ili kujenga uwezo wa kugharimia elimu ya juu, Serikali imeanzisha Bodi ya Mikopo ambayo itahusika katika utoaji wa mikopo na usimamizi wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Programu ya Mabadiliko katika Sekta ya Afya. Katika mabadiliko hayo, huduma za kinga zimeimarishwa kwa kutoa chanjo dhidi ya magonjwa hatari kwa watoto ambapo kiwango cha chanjo kimefikia wastani wa asilimia 89.4 katika kila Wilaya kutoka asilimia 30 mwaka 1995. Aidha, ugonjwa wa polio ulitokomezwa mwaka 1996. Idadi ya wanawake wanaotumia huduma za Kliniki

iliongezeka kutoka asilimia 70 mwaka 1995 hadi asilimia 90 mwaka 2005. Serikali imeongeza bajeti ya kukabiliana na ugonjwa wa malaria kutoka Shilingi milioni 44 mwaka 1997/1998 hadi Shilingi bilioni 1.8 mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za tiba, Serikali imeimarisha mfumo wa upatikanaji wa dawa kwenye Zahanati na Vituo vya Afya. Aidha, huduma za uchunguzi zimeimarika baada ya Serikali kuzipatia mashine mpya za *X-Ray* hospitali 98 zikiwemo za Wilaya, Mikoa, za Rufaa na zile maalumu. Vilevile, Hospitali za Rufaa nchini zimepatwa vifaa vya uchunguzi wa magonjwa vya *CT-Scan*, mashine za *ultrasound* na *X-Ray* kubwa. Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* imepatwa mashine mbalimbali zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.78. Serikali pia inazifanyia ukarabati na kuweka vifaa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na katika Hospitali za Bugando, Mbeya, *KCMC*, Kibong'oto, Mirembe, Isanga, Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili na Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya mwaka 2001 kwa ajili ya watumishi wa Umma. Hadi Aprili, 2005 Mfuko umesajili wanachama 248,829 ambapo asilimia 44 ni wanawake. Idadi ya wanaonufaika na Mfuko huo imeongezeka kutoka watu 691,774 mwaka wa 2001 hadi 1,144,614 mwaka 2004/2005. Kati ya wanaonufaika wapo wazee 468,148 wenye umri zaidi ya miaka 60 walioandikishwa kama wategemezi. Mfuko umesajili jumla ya Vituo 3,558 vya matibabu ambapo asilimia 70 ya Vituo hivyo vipo Vijijini.

Mheshimiwa Spika, huduma ya maji nayo imeendelea kutiliwa mkazo. Katika kipindi cha miaka kumi, visima vifupi 9,247 na virefu 2,019 vimechimbwa na mabwawa 718 na matanki 2,450 ya uvunaji wa maji ya mvua yalijengwa. Ujenzi wa miradi mikubwa ya maji ya Wami - Chalinze na wa Mjini Dodoma ilikamilika. Kamati za Maji za Vijiji zimeanzishwa na kuongezeka kutoka 3,726 mwaka 1995 hadi 10,515 mwaka 2004. Jumla ya Mifuko ya maji 10,006 yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.3 nayo ilianzishwa. Serikali ilianzisha Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini. Mamlaka hizo zimeweza kuongeza utoaji wa maji safi kutoka lita bilioni 79 mwaka 1997 hadi lita bilioni 110 mwaka 2004. Aidha, ukusanyaji wa mapato umeongezeka kutoka Shilingi bilioni 4.6 mwaka 1998 hadi Shilingi bilioni 14.85 mwaka 2004. Mamlaka 10 kati ya 19 zinajitegemea kimapato na kiuendeshaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua hizo, hali ya upatikanaji wa maji Mijini na Vijijini imeboreka ikilinganishwa na hali ilivyokuwa miaka kumi iliyopita. Hivi sasa asilimia 53.56 ya wananchi waishio Vijijini na zaidi ya asilimia 74 ya wakazi wa Mijini wanapata huduma ya maji safi. Hadi mwezi Aprili 2005, Mamlaka za Maji 60 zilikuwa zimeundwa katika Halmashauri za Wilaya ili kusimamia huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji midogo na miradi mikubwa ya maji ya Kitaifa iliyomo kwenye Miji hiyo. Utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama na Shinyanga pamoja na Vijiji 54 vya Mikoa ya Mwanza na Shinyanga nao umeanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio makubwa katika huduma za jamii yanayoonekana katika baadhi ya Wilaya nchini, yanatokana na mchango mkubwa kutoka katika Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*). Mfuko huo ulianzishwa na Serikali kwa lengo la kujenga uwezo wa jamii wa kuainisha kero, kuweka vipaumbele, kutekeleza, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Katika Awamu ya Kwanza, *TASAF* ilichangia kupatikana kwa madarasa 2,586, Ofisi za Walimu 468, nyumba za Walimu 335, matundu ya vyoo 951, Maabara za Shule za Sekondari 18 na majengo ya Utawala 26.

Mchango mwingine ni wa ujenzi wa mabweni 13, Zahanati 312, nyumba za Waganga na Wauguzi 922, matundu ya vyoo vya wagonjwa 613, matanuri ya kuchomea taka 304, Miradi ya Maji ya Bomba 65, mabwawa matano, visima vifupi 559, ukarabati wa barabara tano zenye urefu wa Kilometa 85, Miradi ya Umwagiliaji Maji miwili, ujenzi wa majosho mawili, ujenzi wa masoko manne, ghala moja na Ofisi moja ya Kijiji. Kadhalika, kupitia mfuko huo, Kilometa 2,173.6 za barabara zilitengenezwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka 10, Serikali imewezesha kuimarishwa kwa uhuru wa kupata na kutoa habari, kuundwa kwa Baraza la Habari na kuandaliwa kwa Sera ya Habari na Utangazaji kwa lengo la kupanua uhuru wa Vyombo vya Habari na kusimamia maadili ya taaluma ya Uandishi wa Habari. Kumekuwepo na ongezeko kubwa la Vyombo vya Habari hasa vya binafsi. Vyombo vya habari vya umma hususan Idara ya Habari, Magazeti ya Serikali na Taasisi ya Utangazaji vimeongeza huduma zao kwa wananchi.

Idadi ya magazeti na majarida yaliyosajiliwa rasmi imeongezeka kutoka 353 mwaka 1995 hadi 507 mwezi Machi, 2005. Kwa upande wa Vyombo vya Habari vya elektroniki, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2004, jumla ya Vituo vya Radio 32 na Vituo 63 vya Huduma ya Televisheni vilikuwa vimeanzishwa na kusajiliwa rasmi ikiwemo Televisheni ya Taifa ambayo inarusha matangazo yake kupitia *satellite* na hivyo kuonekana katika sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Aidha, huduma za habari zinapatikana pia kupitia mtandao wa *internet*. Serikali iliendelea kuimarisha Radio Tanzania na kuyawezesha matangazo yake kufikia asilimia 80 Desemba 2004, hivyo kuweza kuhimili ushindani. Televisheni ya Taifa imekamilisha ujenzi wa Vituo vidogo vya kurushia matangazo yake katika Mikoa ya Dodoma, Arusha na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu imedumisha na kuendeleza uhusiano mzuri na nchi zote duniani na Mashirika ya Kimataifa. Uwakilishi wetu nchi za nje uliokuwa na Balozi 25 mwaka 1995, sasa una Balozi 29 baada ya kufungua Balozi mpya Falme za Kiarabu, Rwanda, Burundi na Malawi. Ili kupunguza gharama za ukodishaji majengo, Serikali ilijenga na kununua majengo mapya katika nchi kadhaa na kufanya jumla ya majengo kuwa 72 kutoka 55 yaliyokuwepo mwaka 1995/1996. Majengo hayo yanatumika kama Ofisi na makazi ya Maofisa katika Balozi. Kutokana na jitihada za Serikali, deni sugu la Shilingi bilioni tisa ambalo Balozi zetu zilikuwa

zinadaiwa hadi mwaka 1995/1996, lililipwa lote kufikia mwaka 2003 na hivyo kurudisha heshima na hadhi ya Balozi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitunga Sera Mpya ya Mambo ya Nje mwaka 2001, ambayo inatilia mkazo zaidi diplomasia ya kiuchumi. Mafanikio ya sera hiyo yameanza kuonekana kwani kumekuwepo na ongezeko kubwa la mitaji ya wawekezaji kutoka nje, kufutiwa madeni na ongezeko la watalii na wafanyabiashara walioitembelea Tanzania na kuingia mikataba kwenye miradi mbalimbali ya kilimo, viwanda, madini, afya, utalii, usafiri wa majini na uzalishaji. Ongezeko hilo limekwenda sambamba na Tanzania kuendelea kupata misaada na mikopo kutoka nchi rafiki, Vyombo vya Fedha vya Kimataifa na Vyama na Asasi mbalimbali za maendeleo duniani.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, ilipewa heshima ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Viongozi wa Nchi za Jumuiya hiyo mwaka 2003 na hivyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Kwa upande wa Umoja wa Afrika, Tanzania ilipata nafasi za kutoa wataalamu wake kwenye Kamisheni za Kilimo na Maendeleo pamoja na Tume ya Haki za Binadamu ya Afrika. Aidha, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge, alichaguliwa kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika. Tanzania vilevile, imechaguliwa kuwa Mjumbe asiye wa kudumu kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa kipindi cha miaka miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Umoja wa Ushuru wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeanza kutekelezwa Januari, 2005. Kutokana na uhusiano wa kidugu miongoni mwa wananchi wa nchi zetu tatu, hivi sasa nchi zetu zinaangalia uwezekano wa kuharakisha uanzishwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki. Kamati iliyoundwa kutafiti na kuchunguza kwa kina suala hilo, iliwasilisha mapendekezo yake ambayo yalijadiliwa katika Mkutano wa Sita wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Novemba, 2004.

Tanzania iliunda Timu ya Wataalamu kuchambua ripoti hiyo na kutoa maoni ambayo yalijadiliwa na Wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama hatua ya mwanzo ya kutafuta mshikamano wa nchi. Serikali bado inaendelea kuyafanyia kazi maoni ya Wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia utawala bora na umakini wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa katika medani ya Kimataifa, aliteuliwa kuwa Mwenyekiti Mwenza pamoja na Rais Tarja Halonen wa Finland, kuongoza Tume ya Kimataifa kuhusu masuala ya kijamii katika utandawazi. Kazi hiyo ilikamilika na ripoti iitwayo “Utandawazi Wenye Haki” imetolewa. Aidha, Mheshimiwa Rais aliteuliwa pia na Waziri Mkuu wa Uingereza, Mheshimiwa Tony Blair kuwa Mjumbe katika Tume Maalumu ya kuangalia matatizo ya Bara la Afrika na kupendekeza mbinu ya kuyatatua. Tume hiyo

imekamilisha kazi na kuwasilisha ripoti yake. Kitaifa, ripoti hiyo ilizinduliwa hapa Bungeni tarehe 9 Juni, 2005 na Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi hiyo nzuri na kwa kuinua hadhi na heshima ya nchi yetu katika medani ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya mipaka ya nchi yetu kwa jumla ilikuwa shwari isipokuwa mipaka ya nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi ambazo zimekuwa na migogoro ya wenyewe kwa wenyewe. Migogoro hiyo imesababisha wimbi la wakimbizi kutoka nchi hizo kukimbilia Tanzania. Hadi Machi, 2005, kulikuwa na jumla ya wakimbizi 603,046. Suluhisho la kudumu la tatizo la wakimbizi ni kwa wakimbizi hao kurudi kwenye nchi zao za asili pindi hali inapokuwa shwari. Serikali imeendelea kushirikiana na Shirika la Wakimbizi la Umoja wa Mataifa na wadau wengine kuwarejesha wakimbizi makwao. Kati ya Julai, 2004 hadi Machi 2005, jumla ya wakimbizi 92,060 walirejeshwa makwao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kudumisha na kuendeleza amani na utulivu nchini, hali ambayo imejenga mazingira mazuri kwa wananchi kutekeleza majukumu yao na kuwavutia wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi. Sheria mpya zimetungwa na nyingine zimerekebisha ili ziendane na mazingira yaliyopo. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1996, Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka 1996, Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1998, Sheria ya Pasi za Kusafiria ya mwaka 2002 na Sheria ya Ugaidi ya mwaka 2002.

Vyombo vya ulinzi na usalama vimeimarishwa kwa kupatiwa zana za kisasa za kufanyia kazi na kujenga mazingira mazuri ya kutekeleza wajibu wao ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo ndani na nje ya nchi. Vyombo hivyo vimeweza kuendesha doria na operesheni mbalimbali za kudhibiti uhalifu nchini. Aidha, juhudi za kupeana taarifa za uhalifu zimeendelezwa kwa kushirikiana na Majeshi ya Polisi ya nchi jirani. Vilevile, wananchi wamehamasishwa kujilinda na kusaidia Polisi katika utoaji taarifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia iliendelea kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa ulinzi wa umma ili kuongeza nguvu ya Vyombo vya Dola, ambapo mafunzo ya Mgambo yalitolewa nchi nzima na hadi mwaka 2004 Wanamgambo 789,988 walikuwa wameandikishwa kikanda. Kwa kutambua umuhimu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Serikali ilirejesha mafunzo ya Jeshi hilo mwaka 2001. Zaidi ya vijana 7,954 wamepata mafunzo ya JKT hadi Desemba, 2004. Kati ya hao 1,890 wameajiriwa na Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Hivi sasa kambi 15 zinatoa mafunzo ya ulinzi, maadili, nidhamu na stadi mbalimbali ili kuwaandaa vijana hao wawe raia wema wanaoweza kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza kwa awamu kazi ya kustawisha Makao Makuu. Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu ilitekeleza Mpango Kabambe wa Ustawishaji Makao Makuu kwa kusanifu maeneo mbalimbali yenye jumla ya viwanja 11,164 sawa na asilimia 74.68 ya lengo la viwanja 14,950. Hekta 532 zilitengwa na kutolewa kwa Taasisi 32 mbalimbali ikiwa ni pamoja na Hospitali kubwa inayojengwa na KKKT, Dayosisi ya Dodoma (Ha.125), Chuo cha Polisi (Ha.76),

Makaburi ya Kitaifa (Ha.100) na Uwanja wa Maonyesho Nane Nane (Ha.56). Ili kufanikisha shughuli hizo, ramani za maeneo mbalimbali zilichorwa upya.

Maeneo hayo ni Hazina, Chinangali, Kilimani, Nkuhungu, Mji wa Zamani na Eneo la Kati ya Mji la Biashara. Aidha, ramani za maeneo matatu ya makazi yaliyojengwa holela ya Chang'ombe, Ostabei na Maili Mbili yenye wakazi kati ya 35,000 na 50,000 zilichorwa upya. Zoezi la kuhamishia Serikali Makao Makuu Dodoma, lilipewa msukumo mpya katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005 hasa kufuatia maagizo ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa. Hatua hiyo ilifanya Bunge na Wizara tatu kuhamia Dodoma. Wizara hizo ni Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Ushirika na Masoko na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Aidha, baadhi ya Idara katika Ofisi ya Waziri Mkuu nazo zimehamia Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi ili washiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Kata, Vijiji na Vitongoji wamehimiza wananchi kushiriki katika kuandaa mipango shirikishi na endelevu pamoja na kuitekeleza. Kutokana na uhamasishaji huo, wananchi wameshiriki kutekeleza mipango ya maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari, upatikanaji wa huduma za afya na kufanikisha miradi maalum kama vile miradi inayofadhiliwa na *TASAF*.

Vilevile, elimu na uhamasishaji huo vimechangia katika kuwawezesha wananchi kupiga vita mila na desturi potofu zinazowakandamiza wanawake na watoto. Katika kuwaimarisha wanawake katika Siasa na Uongozi, Serikali imeongeza nafasi za uwakilishi wa wanawake Bungeni kutoka asilimia 15 mwaka 1995 hadi asilimia 22.5 mwaka 2004.

Aidha, uwakilishi katika Mabaraza ya Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Vijiji umefikia asilimia 34.5 kutoka asilimia 25 mwaka 1995. Marekebisho ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), yameongeza nafasi za uwakilishi wa wanawake Bungeni kupitia Viti maalum hadi kufikia si chini ya asilimia 30 ya Wabunge wote. Serikali imeendelea kuwezesha Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, Mfuko wa Mikopo ya Uzalishaji Mali kwa Wanawake na Vyama vya Ushirika wa Kuweka na Kukopa kwa lengo la kuwapatia wanawake mitaji ya kuwaongezea uwezo kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kulinda haki na ustawi wa mtoto, Serikali imeridhia Mikataba ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika kuhusu haki za mtoto. Katika kutekeleza hilo, Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali imetekeleza Mpango wa Muda Maalum wa kukomesha utumikishwaji watoto katika kazi za hatari katika Wilaya 11 za Ilala, Temeke, Kinondoni, Mufindi, Iringa Vijijini, Urambo, Iramba, Kondo, Arumeru, Simanjiro na Manispaa ya Arusha.

Katika Awamu ya Kwanza iliyoanza mwaka 2000 na kuishia 2004, Wilaya hizo zimefanikiwa kuwaondoa watoto zaidi ya 32,000 waliokuwa wanatumikishwa kwenye migodi, mashamba ya mazao ya biashara, majumbani na biashara ya ngono. Aidha, zipo

juhudi kubwa zinazofanywa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Madhehebu ya Dini na watu binafsi za kuwahudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Nawapongeza sana wote kwa juhudi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu ilipoingia madarakani iliweka wazi dhamira yake ya kupambana na rushwa. Rais Benjamin William Mkapa, aliunda Tume chini ya uongozi wa Jaji Joseph Sinde Warioba kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu namna ya kushughulikia tatizo la rushwa nchini. Matokeo ya kazi ya Tume hiyo yameleta mabadiliko makubwa katika sheria, sera na miundo ya Taasisi Serikalini.

Baadhi ya sheria zilitungwa na nyingine kufanyiwa marekebisho ili kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya rushwa. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002; Sheria ya Maadili ya Viongozi Na. 5 ya mwaka 2001; Sheria ya Ununuzi wa Vifaa vya Serikali Na. 3 ya mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake; Sheria ya Fedha za Serikali Na. 6 ya mwaka 2001; Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999.

Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa ulianzishwa kwa kushirikisha vyombo mbalimbali vya Serikali kwa lengo la kuongeza tija, kuboresha mazingira ya Taasisi za Umma, kuainisha mianya ya rushwa na kuangalia namna bora ya kuziba mianya hiyo. Katika kipindi cha Januari, 2002 hadi Juni, 2004 watumishi wa Serikali 456 waliobainika kuhusika na rushwa walipewa barua za onyo au karipio; 362 walisimamishwa kazi na 403 walifukuzwa kazi au kustaafishwa kwa manufaa ya Umma.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua za kuimarisha Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) kimafunzo, kivifaa na kifedha. Vilevile, imeongeza bajeti ya Taasisi kutoka Shilingi milioni 15 mwaka 1996/1997 hadi Shilingi bilioni tisa mwaka 2004/2005. Idadi ya watumishi imeongezeka kutoka 185 hadi 700. Ofisi za TAKURU sasa zimeanzishwa katika Mikoa na Wilaya zote nchini ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

Serikali vilevile imeongeza kasi ya kuelimisha Umma kuhusu vita dhidi ya rushwa kwa njia ya radio, mikutano ya hadhara, Semina, vijarida, vipeperushi, magazeti, televisheni, kalenda na michezo ya kuigiza. Katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendeleza vita dhidi ya rushwa kwa kuelimisha Umma na kuimarisha Taasisi ya Kuzuia Rushwa ili iweze kutimiza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na majanga na maafa ya aina mbalimbali hapa nchini, Serikali imekamilisha Sera ya Taifa ya Maafa ya mwaka 2004. Sera hiyo ndiyo inayoongoza na kuratibu shughuli zote zinazotekelezwa na Sekta mbalimbali katika kudhibiti maafa yanayotokea hapa nchini. Sera hiyo inalenga kuijengea jamii uwezo wa uratibu na ushirikiano katika kukabiliana na maafa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuratibu na kufanya tathmini ya hali halisi ya udhibiti wa maafa nchini kwa kushirikiana na wadau wengine. Lengo la zoezi hilo ni kubaini uwezo na mapungufu ya kisheria yaliyopo ili marekebisho na maandalizi

ya mitaala ya kufundishia masuala ya menejimenti ya maafa yaweze kufanyika. Aidha, utafiti wa kutambua aina za maafa yanayotokea katika maeneo mbalimbali nchini umefanyika. Serikali iliandaa mwongozo wa kukabiliana na maafa na kuusambaza kwa wadau mbalimbali. Mwongozo huo unaonyesha mgawanyo wa majukumu ya wadau katika udhibiti wa maafa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mtandao wa mawasiliano wa *Radio Call* unaunganisha Ofisi ya Waziri Mkuu na Mikoa yote 21 ya Tanzania Bara, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Afya na Hospitali za Rufaa nchini. Mtandao huo una madhumuni ya kurahisisha mawasiliano hasa wakati wa dharura au maafa.

Mafunzo ya Menejimenti ya Maafa kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu wa Majengo yametolewa kwa Maafisa wa Mikoa na Wizara, Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya, Maafisa Mipango wa Wilaya na Kamati za Maafa. Ili kukabiliana na majanga ya moto, Jeshi la Zimamoto limeimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi. Halmashauri za Manispaa na Miji, viwanja vya ndege na bandari zina jumla ya magari 53 ya kuzima moto. Aidha, jeshi hilo linashirikiana vyema na Kampuni binafsi mara majanga ya moto yanapotokea. Serikali pia inatoa elimu ya maafa kupitia Vyombo vya Habari na machapisho mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa UKIMWI ni tatizo la kijamii linalogusa Sekta zote, Serikali iliunda Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Aidha, Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ilipitishwa mwaka 2001 na Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI mwaka 2003. Utekelezaji wa sera na mkakati huo umewezesha elimu kuwafikia wananchi wengi na hivyo UKIMWI kuanza kuzungumzwa kwa uwazi zaidi. Sekta zote za Umma na zisizokuwa za Umma zina mipango ya kudhibiti UKIMWI inayolenga kuzuia maambukizo mapya, kutoa huduma na matibabu kwa waishio na virusi vya UKIMWI na kusaidia yatima na familia zilizoathiriwa na UKIMWI.

Serikali imeongeza bajeti ya kudhibiti UKIMWI kutoka Shilingi bilioni 17 mwaka 2001/2002 mpaka Shilingi bilioni 92.5 mwaka 2004/2005. Katika fedha hizo, msaada kutoka kwa wabia wa maendeleo umeongezeka kutoka Shilingi bilioni 12 mwaka 2001/2002 hadi Shilingi bilioni 78 mwaka 2004/2005. Aidha, ushirikiano wetu na nchi jirani za Maziwa Makuu na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kukabiliana na janga la UKIMWI kwa sasa umeongezeka sana.

Mheshimiwa Spika, moja ya hatua muhimu zilizochukuliwa na Serikali katika kuwahudumia wananchi walioathirika na UKIMWI ni kuanzisha mpango wa huduma na matibabu. Mpango huo unalenga kutoa dawa bila malipo kwa watu waishio na virusi vya UKIMWI wapatao 400,000 katika kipindi cha miaka mitano. Hivi sasa watu 4,200 wanafaidika na huduma hiyo.

Serikali imenunua dawa za kutosha wagonjwa 17,000 na zimesambazwa katika hospitali 64. Idadi ya wagonjwa wanaopata dawa hizo za kurefusha maisha itaongezeka kulingana na kuongezeka kwa idadi ya Vituo vitakavyokuwa na uwezo wa kitaalamu na

miundombinu inayohitajika katika kutoa dawa hizo. Inatarajiwa kuwa wagonjwa wapatao 100,000 watakuwa wanapata dawa hizo ifikapo Desemba, 2006. Lengo la Serikali ni kuwezesha hospitali zote za Serikali na zisizo za Serikali nchini kutoa dawa hizo ili walengwa waweze kuzipata kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kudhibiti uingizaji na utumiaji wa dawa za kulevya nchini. Hatua hizo ni pamoja na kutungwa kwa sheria ya kudhibiti uingizaji na utumiaji wa dawa za kulevya nchini na kuanzishwa kwa Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya ya mwaka 1997. Vilevile, hatua zimechukuliwa kuanzisha Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Dawa za Kulevya. Lengo la mpango huo ni kuelimisha jamii kuhusu madhara na athari zinazoweza kusababishwa na utumiaji wa dawa za kulevya na kujenga uwezo wa jamii wa kudhibiti dawa za kulevya kwa kutoa mafunzo kwa viongozi wa Serikali za Mitaa na Taasisi zisizo za kiserikali.

Vilevile, mafunzo yametolewa kwa Watendaji wa Wakala na Idara za Serikali za Forodha, Uhamiaji na Polisi kwa madhumuni ya kujenga uwezo katika kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya nchini kupitia mipakani, viwanja vya ndege na bandarini. Kutokana na hatua hizo, kati ya mwaka 1997 na 2004, jumla la kilo 3,146 za madawa ya viwandani, kilo 2,057,868 za bangi na kilo 22,866 za mirungi zilikamatwa na wahusika walitiwa hatiani. Aidha, jumla ya ekari 282.5 za mashamba ya bangi ziliteketezwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itahakikisha kanuni za maadili ya Vyama vya Siasa ambazo zilitungwa kwa kushirikisha Vyama vyote vya Siasa vyenye usajili wa kudumu, zinaanza kutumika ili kuendelea kujenga misingi imara ya siasa za kistaarabu.

Aidha, Ofisi ya Bunge itaendelea kuratibu na kuimarisha shughuli zake. Hii ni pamoja na kuratibu Mikutano yote ya Bunge na Vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge. Serikali itaendelea kushirikiana kwa karibu zaidi na Ofisi ya Bunge katika kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Bunge inatekelezwa kwa mafanikio makubwa na kukamilishwa kwa wakati. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa ukumbi mpya wa Bunge na upanuzi na ukarabati wa Ofisi za Bunge Dar es Salaam na Zanzibar.

Serikali itaendelea kuhamasisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya Muungano na umuhimu wa kila mwananchi kushiriki katika kuenzi na kuulinda. Aidha, Sekretarieti ya Muungano itaongezewa uwezo wa kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, maandalizi yanayohusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 yakiwemo ya ununuzi wa vifaa vya uchaguzi, mafunzo kwa Watendaji na elimu kwa Wapigakura yanaendelea. Tume imetangaza ratiba ya hatua mbalimbali za uchaguzi. Kwa mujibu wa ratiba hiyo, uchukuaji wa fomu za kugombea Urais unaanza tarehe 11 Julai, 2005 na ule wa kugombea Ubunge na Udiwani unaanza tarehe 1 Agosti, 2005.

Mheshimiwa Spika, uteuzi utafanyika tarehe 20 Agosti, 2005, kampeni za uchaguzi zitaanza rasmi tarehe 21 Agosti, 2005 hadi tarehe 29 Oktoba, 2005 na siku ya uchaguzi itakuwa tarehe 30 Oktoba, 2005. Wadau wote hususan Vyama vya Siasa,

Vyombo vya Habari, Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na Asasi Zisizo za Kiserikali, wanaendelea kushirikishwa ili kuhakikisha kwamba Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu unafanyika vizuri, kwa uhuru na haki.

Natoa wito kwa wananchi wote waliojiandikisha kutunza vitambulisho vyao vya kupigia kura ili waweze kushiriki kikamilifu katika zoezi hilo mara muda utakapofika. Aidha, ni vyema wananchi wote wakatambua kuwa wale ambao hawatakuwa na vitambulisho vya kupigia kura hawataweza kupiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea kutumia mfumo mpya wa utendaji kazi katika utumishi wa Umma pamoja na utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 na Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Mfumo wa upimaji wa wazi wa utendaji kazi katika utumishi wa umma, utaendelea kuanzishwa ndani ya Wizara na Idara za Serikali pamoja na uundwaji wa Bodi na Kamati maalum za Ajira kwa kila mwajiri. Aidha, zoezi la kuanzisha mfumo wa uboreshaji utendaji kazi katika Mikoa yote Tanzania Bara nalo litaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuziimarisha Serikali za Mitaa, Serikali ilikamilisha maandalizi ya mradi mpya unaoziwezesha Serikali hizo kupata fedha zaidi kwa matumizi ya shughuli za maendeleo. Mradi huo utagharimiwa kwa pamoja na fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia, mchango wa Serikali Kuu, pamoja na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kujiunga na mradi huo, kila Halmashauri italazimika kutimiza masharti yaliyokubalika ikiwa ni pamoja na utunzaji mzuri wa kumbukumbu za kimahesabu na usimamizi wa fedha; kupata hati safi za ukaguzi wa hesabu; kuwa na wafanyakazi wenye sifa na uwezo unaotakiwa kwenye ngazi mbalimbali; kuonyesha uwazi katika maamuzi na utendaji wa Halmashauri; kuwa na uwezo wa kifedha wa kuchangia asilimia tano ya gharama za shughuli za maendeleo na uwezo wa kupanga na kutekeleza mipango shirikishi kuhusu maendeleo ya Halmashauri.

Napenda kutoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuboresha hali ya utendaji wao wa kazi ili ziweze kutimiza masharti ya kuingizwa katika mpango huo wenye lengo la kuziongezea uwezo wa kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Serikali imeandaa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA). Mkakati huo umelenga kuhakikisha kuwa uchumi wetu unaendelea kukua kwa kasi zaidi na hivyo kuiwezesha Tanzania kufikia malengo yaliyobainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Mkakati huo utatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali kuanzia mwaka 2005/2006 hadi mwaka 2009/2010 na Serikali imetenga zaidi ya asilimia hamsini ya bajeti ya mwaka 2005/2006 kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati huo.

Maeneo ya kipaumbele yaliyobainishwa katika MKUKUTA ni pamoja na kupunguza umaskini wa kipato kwa kuongeza ukuaji wa uchumi unaolenga jamii maskini, kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii na kuimarisha utawala bora na uwajibikaji. Sekta binafsi nayo itahamasishwa kuelekeza rasilimali zake katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha wananchi wanashiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi, Serikali itaongeza kasi ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezesaji wa Wananchi Kiuchumi pamoja na Sheria ya Uwezesaji. Hatua zitakazochukuliwa zitalenga katika kuhakikisha kwamba sera mbalimbali za Serikali na sheria zinasaidia katika kuwafanya wananchi wa Tanzania kuwa na kauli na ushiriki wa kutosha katika shughuli mbalimbali za kiuchumi katika sekta zote.

Aidha, wananchi watawezesha na kusaidiwa kuwa na miradi mizuri inayokopesheka na kuwepo kwa utaratibu wa mifuko ya dhamana na mitaji ili Watanzania wasiendeleo kubaki nyuma na shughuli za uchumi kushikwa na kuendeshwa zaidi na watu wa nje.

Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) umeanzishwa kama moja ya njia za kuwawezesha wananchi kupata hatimiliki ya mali zao kama vile ardhi, nyumba na biashara nyinginezo ili kuwasaidia wananchi kulinda mali zao ambazo wanaweza kuzitumia kama dhamana katika kupata mikopo kwa ajili ya shughuli zao za kujiongezea mapato. Natoa rai kwa wananchi kushirikiana na Serikali kufanikisha mipango hiyo ya uwezesaji wa wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, zoezi la urekebishaji na ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma linakaribia kumalizika. Serikali imekamilisha taratibu zote muhimu kwa ajili ya kuanzisha mpango wa pamoja wa kuwekeza chini ya Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania. Ili kufanikisha malengo ya mfuko, Serikali imetoa asilimia mbili ya hisa zake katika Kampuni ya Bia Tanzania na asilimia moja katika Kampuni ya Sigara, zote zikiwa na thamani ya Shilingi bilioni 10.9 ili zianze kutumika kama mbegu ya mtaji kwa mipango mbalimbali ya uwekezaji wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huo umeanza kuuza vipande kwa wananchi tangu mwezi Mei, 2005 ambapo katika kila kipande kinachouzwa Shilingi 100, mwananchi atatakiwa kukinunua kwa Sh.70/= na Serikali itamwongezea Sh.30/=. Hatua hiyo imechukuliwa ili kuwawezesha wananchi wengi kununua hisa, kumiliki dhamana na kunufaika na mfuko huo wa umoja.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji katika kilimo unategemea sana matumizi ya pembejeo ya mbolea. Katika mwaka 2005/2006, Serikali imetenga Shilingi bilioni 8.0 zitakazotumika kufidia gharama za usafirishaji wa tani 75,000 za mbolea za aina mbalimbali. Viongozi na Watendaji katika Mikoa na Wilaya wasimamie na kuratibu utekelezaji wa mpango huo ili kuhakikisha kuwa mbolea inawafikia wakulima kama ilivyopangwa.

Kuhusu kilimo cha umwagiliaji, mkazo utawekwa kwenye kusimamia skimu zote za umwagiliaji ili kuhakikisha kwamba malengo yaliyowekwa ya kuongeza tija na uzalishaji yanafikiwa. Aidha, Serikali itaandaa mfumo wa matumizi ya takwimu zilizotayarishwa na Mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji Mashambani ili ziweze kutumiwa na Wilaya kama mwongozo wa kitaalamu katika utayarishaji wa mipango ya kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo katika nyanja za tiba, kinga, usambazaji maji na uboreshaji wa malisho. Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana na Asasi mbalimbali kama vile *Heifer Project International*, *Caritas*, *Regional Integrated Programme* na Wadau wengine ili kuongeza kasi ya uendelezaji mifugo katika Mikoa ya Kusini mwa nchi yetu.

Juhudi zitaelekezwa katika kuongeza uzalishaji wa nyama na maziwa, upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo, ukusanyaji wa maziwa Vijijini, usindikaji na kupanua wigo wa masoko mapya yanayonunua nyama bora na maziwa hasa maduka makubwa. Aidha, Serikali itaweka msukumo zaidi katika kuuza ngozi zilizosindikwa kwa kufufua viwanda vya ngozi na kuanzisha vipya.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuweka mkazo katika uzalishaji wa mazao ya kilimo, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu, mwenendo, ufanisi na mifumo ya masoko ya mazao ya kilimo ili hatimaye iwezeshe upatikanaji wa soko la mazao ya kilimo la uhakika ambalo litainua hali ya maisha ya wananchi. Kazi hiyo itatekelezwa chini ya Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo. Mafanikio mbalimbali yameanza kuonekana hasa kwa vikundi vinavyoshiriki katika shughuli za Programu. Kutokana na mafunzo mbalimbali yanayotolewa, baadhi ya vikundi vimeanza kuuza bidhaa zao kwa faida baada ya kuelewa umuhimu wa kutafuta taarifa za masoko na pia kuwa na uwezo wa kujadiliana bei na wanunuzi. Pia, vikundi hivyo vinajijengea uwezo wa kifedha ili viweze kujiendesha kibiashara na pia kuwawezesha wanachama wake kumudu gharama za uzalishaji badala ya kutegemea mikopo isiyo rasmi kutoka kwa walanguzi. Serikali itakamilisha Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo.

Sera hiyo itasimamia uendeshaji wa masoko ya mazao ya kilimo kwa kuzingatia taratibu na kanuni na pia itaweka mazingira bora na mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za masoko ya mazao ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, ili tuwe na ushirika imara, hatuna budi kupeleka madaraka ya udhibiti na usimamizi wa Vyama vya Ushirika karibu na Vyama hivyo na kuendelea kuwahamasisha wananchi umuhimu wa kuwa na Viongozi wa Vyama vya Ushirika waaminifu na wanaowajibika kwa wananchi na ambao ni wabunifu kibiashara. Katika mwaka 2005/2006, Serikali itaimarisha uongozi wa Vyama vya Ushirika kwa kuweka taratibu za kusimamia uchujaji wa wanaogombea uongozi.

Aidha, itaendelea kuhamasisha wananchi kuhusu uanzishaji wa Vyama vya akiba na mikopo kwa wingi, kuandaa miongozo na kanuni maalum kwa madhumuni ya

kuboresha utendaji na kuhakikisha usalama wa akiba za wanachama. Uchambuzi maalum utafanywa kwa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania na Muungano wa Vyama vya Akiba na Mikopo ili kuainisha upya majukumu na muundo wao kwa lengo la kuwa na muundo unaokidhi mahitaji ya wanachama na usio na gharama kubwa za uendeshaji.

Hatua nyingine ni kuhamasisha wakulima kuzalisha kulingana na mahitaji ya soko na kuwawezesha kushiriki katika maonyesho ya kilimo ya ndani na nje ya nchi ili kuweza kupata masoko ya uhakika zaidi.

Mheshimiwa Spika, Sekta za Uvuvi na Utalii zimeendelea kutoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa. Kwa kutambua mchango huo, katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea kulinda rasilimali za uvuvi dhidi ya uvuvi usio endelevu kwa kuimarisha doria za majini na nchi kavu, kushirikisha jamii katika kusimamia rasilimali hiyo na kuelimisha jamii juu ya ufugaji wa samaki. Aidha, wananchi watahimizwa kuanzisha vikundi vya uvuvi na ujenzi wa mabwawa ya samaki ikiwa ni pamoja na kupewa mikopo kwa shughuli hiyo. Kwa upande wa utalii, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu katika maeneo ya kitalii, kubaini vivutio vipya kwa watalii na kutangaza zaidi vivutio tulivyonavyo ndani na nje ya nchi ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa bidhaa katika viwanda umeendelea kuwa mzuri na bidhaa za viwandani zimesambazwa nchini kwa wingi kukidhi mahitaji ya wananchi. Hivi sasa, bidhaa nyingi zinazozalishwa na viwanda vyetu zinaonekana katika maduka mbalimbali zikishindana na zile zinazotoka nje ya nchi. Jambo hilo linaashiria kuimarika kwa Sekta ya Viwanda na mwelekeo mzuri wenye matumaini katika uchumi wa Taifa.

Katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea kuhamasisha, kuwezesha na kuelekeza wawekezaji binafsi katika kujenga viwanda vya usindikaji mazao ya kilimo, kuimarisha Sekta ya Ngozi na Viwanda vya Ngozi na kutekeleza programu na sera ya viwanda vidogo na biashara. Aidha, zoezi la ubinafsishaji litaendelezwa ili kufufua uzalishaji, kufuatilia uwekezaji katika maeneo ya Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara, ikiwa ni pamoja na miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na chuma cha Liganga na kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kuuza bidhaa nje ili Tanzania ifaidike na masoko nafuu ya Amerika ya Kaskazini, Ulaya na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika ya Mashariki ulianza rasmi tarehe 1 Januari, 2005. Itifaki hiyo inalegeza masharti ya kibiashara na kuweka wigo wa pamoja wa ushuru wa forodha miongoni mwa nchi wanachama kama nyenzo ya kukuza na kuendeleza biashara, uzalishaji na uwekezaji. Kwa hiyo, changamoto iliyoko kwa wafanyabiashara na Watanzania wote ni jinsi ya kutumia fursa zaidi za masoko zilizopo katika nchi za Afrika Mashariki.

Kadhalika Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizosaini Itifaki ya Mkataba wa Biashara katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ambapo sasa nchi za Jumuiya hiyo ni Eneo Huru la Biashara. Ili tuweze kutumia vizuri fursa hizo, hatuna budi kuuza

bidhaa nyingi, bora na za aina mbalimbali zikiwemo za viwandani, mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na Misitu katika masoko hayo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ardhi ni moja ya sekta muhimu katika kutoa huduma za kiuchumi. Hata hivyo, ili kuwawezesha wananchi kuitumia ardhi yao vizuri, hatuna budi kutoa elimu kuhusu sera, sheria za ardhi na kanuni zake katika Mikoa na Wilaya mbalimbali nchini. Katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendeleza zoezi la kutambua miliki katika maeneo yaliyojengwa kiholela katika Miji mbalimbali nchini kwa kutoa leseni za makazi zinazotambulika kisheria. Utambuzi huu hautahusu maeneo yaliyo ya hatari au yasiyoruhusiwa kwa makazi.

Kwa upande wa upimaji wa ardhi Vijijini na Mijini, Serikali itaendelea kutekeleza zoezi hilo kote nchini, kuimarisha kwa makusanyo ya kodi ya pango la ardhi kwa kujenga mazingira mazuri ya kuwatambua walipakodi na kuandaa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi katika ngazi za Vijiji, Wilaya, Kanda na Taifa. Vile vile, itaanzisha mfumo wa jumla wa utayarishaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi itakayowezesha mipango ya Sekta nyingine kuandaliwa na hivyo kuwezesha ushirikiano mzuri baina ya Sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuchukua hatua zenye lengo la kuwa na utaratibu endelevu wa kupeleka umeme Vijijini. Aidha, katika kuharakisha upatikanaji wa nishati hiyo Vijijini, Serikali itaweka vivutio muhimu katika vyombo au mitambo itakayotoa nishati mbadala kwa mfano nguvu ya mionzi ya jua na upepo. Hivi sasa, ipo sheria ya kuanzisha Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini wenye lengo la kutuwezesha kuwa na chombo cha kusimamia na kuratibu mpango wa kusambaza nishati Vijijini. Maandalizi yanaendelea ili Wakala huo uanze kazi mwaka 2005/2006.

Mradi wa gesi wa *Mnazi Bay* utaendelezwa ili uweze kukamilishwa na hivyo kutoa umeme kwa wananchi wa Mikoa ya Mtwara na Lindi. Aidha, matumizi ya gesi ya Songosongo yataendelea kupanuliwa ili kuongeza idadi ya viwanda Jijini Dar es Salaam vinavyotumia gesi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ujenzi bado ni sekta muhimu yenye mchango mkubwa katika kufanikisha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali katika mwaka 2005/2006, itatekeleza miradi ya ukarabati, ujenzi wa barabara kuu na za Vijiji na ujenzi wa madaraja. Vile vile, Sekta binafsi itashirikishwa katika ujenzi wa barabara kwa kufuata utaratibu wa Jenga-Endesha-Kabidhi.

Chini ya Mradi Maalumu wa Barabara Kuu, Serikali inaendelea kujenga barabara za Dodoma-Manyoni yenye urefu wa Kilometa 127, Manyoni-Singida Kilometa 119, Nangurukuru-Mbwemkulu Kilometa 95 na Mbwemkulu-Mingoyo Kilometa 95. Miradi hiyo yote iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma zake katika maeneo mbalimbali nchini. Huduma za simu zimepanuka zaidi

baada ya Sekta binafsi kuanza kutoa huduma hizo. Hivi sasa huduma za simu za mikononi zinapatikana karibu katika Wilaya zote na katika Vituo vya biashara nchini.

Serikali imepanga gharama zinazokubalika za maingiliano ya mawasiliano ya simu katika kipindi cha miaka minne ijayo baada ya kukamilika kwa uchunguzi wa gharama halisi za mawasiliano nchini. Katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendeleza mafanikio yaliyopatikana katika Sekta hiyo na itashirikiana na wadau wote wa Sekta hiyo ili kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika na mabadiliko makubwa ya kiteknolojia yanayotokea katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma za uchukuzi kwa kurekebisha na kubinafsisha Mashirika mbalimbali. Taratibu zinaendelea ili kulikodisha Shirika la Reli nchini. Aidha, mawasiliano yanaendelea kati ya Serikali za Tanzania, Zambia na ya Jamhuri ya Watu wa China kwa lengo la kupata utaratibu bora wa kuiendesha reli ya *TAZARA*. (*Makofi*)

Mkakati umeandaliwa ili Mamlaka ya Bandari za Tanzania imiliki na kuendesha Bandari zote nchini zikiwemo zile za maziwa. Ili kuimarisha usafiri kwa njia ya reli, Serikali inashirikiana na wadau mbalimbali, zikiwemo nchi jirani ili kuendeleza Ukanda wa Kati wa Maendeleo na hivyo kuwezesha reli ya kati kutoa mchango mkubwa zaidi kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuvihudumia viwanja vya ndege vilivyopo kwa kuzingatia sera na mwelekeo wa sasa wa kuviwezesha viwanja hivyo kujiendesha kibiashara. Serikali imekamilisha mradi mkubwa wa ukarabati wa umeme katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam na kuendelea na matengenezo ya viwanja vingine nchini. Ili kupanua na kuendeleza usafiri wa anga, Serikali itaendelea kushirikiana na nchi mbalimbali ili kuiwezesha sekta hiyo kukua na kutoa mchango mkubwa zaidi katika ujenzi wa uchumi wetu.

Kwa vile suala la usalama wa abiria, vyombo vya usafiri na viwanja vya ndege linapewa kipaumbele kimataifa, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha usalama kwenye viwanja hivyo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEM) unaendelea vizuri. Serikali itaendelea kuwahamasisha wananchi ili watambue kuwa MEM ni mpango endelevu wenye lengo la kuhakikisha kuwa tunatoa Elimu ya Msingi iliyo bora na inayokidhi matarajio ya mazingira ya sasa na ya wakati ujao. Sambamba na MEM, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MES) ulianza Januari 2005.

Mpango huo wa miaka mitano unalenga kupanua, kuboresha na kuleta usawa katika Elimu ya Sekondari na pia kuimarisha uongozi. Ili mpango wa MES uweze kufanikiwa, hatuna budi kushirikisha kwa kuhamasisha na kuelimisha wananchi kwa lengo la kuwawezesha kutoa michango yao ya hali na mali katika ujenzi wa Shule za Sekondari. Tusipofanya hivyo hivi sasa, tutashindwa kukabiliana na ukubwa wa tatizo.

Kwa mfano, katika mwaka huu wa 2005, idadi ya wanafunzi wanaosoma Darasa la Nne ni 1,427,398. Baada ya miaka mitatu wanafunzi hao watakuwa wamehitimu Darasa la Saba. Ni wazi kuwa idadi ya watakaofaulu itakuwa kubwa kuliko hali ilivyo hivi sasa. Kwa hiyo, tunao wajibu wa kuusimamia mpango wa MMES kikamilifu ili angalau kila Kata nchini iwe na Shule ya Sekondari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Elimu ya Juu, yapo mabadiliko makubwa yanayotokea baada ya Serikali kuweka mazingira ya kuwezesha Sekta binafsi na Mashirika ya Dini kuanzisha Vyuo vya Elimu ya Juu. Ili kujenga uwezo wa kugharimia Elimu ya Juu, Serikali imeanzisha Bodi ya Mikopo ambayo itahusika katika utoaji wa mikopo na matumizi yake. Bodi hiyo vilevile itakuwa na majukumu ya kuwatambua wakopaji wenye kuhitaji zaidi kusaidiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwajengea watoto wa kike mazingira ya kuwawezesha kujiunga na Sekta ya Ufundi na Uhandisi, Serikali imechukua hatua za kutoa tuzo kwa wanafunzi wa kike wanaohitimu na kufaulu Kidato cha Sita katika fani za sayansi kama motisha wa kujiunga kwa wingi zaidi na masomo ya Ufundi na Uhandisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Mpango wa Mabadiliko katika Sekta ya Afya kwa lengo la kuboresha huduma zitolewazo na kuondoa kero kwa wananchi, hususan akina mama na watoto ambao ni watumiaji wakuu wa huduma za afya. Uelimishaji na uhamasishaji wa wananchi kuhusu mabadiliko hayo na uundaji wa vyombo vya uwakilishi wa wananchi umeendelea katika Halmashauri 33 zilizokuwa hazijatekeleza zoezi hilo.

Hivi sasa, Bodi za Huduma za Afya 61 zimeanza kazi. Utaratibu wa kuanzisha Mfuko wa Afya ya Jamii katika Sekta isiyo rasmi kwa Halmashauri za Mijini unaojulikana kama Tiba kwa Kadi (TIKA) nao umeanza kutekelezwa. Halmashauri za Miji ya Moshi, Mtwara, Mwanza na Iringa zinataraajia kuanzisha Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea kuimarisha Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa ili iweze kuwa na uwezo wa kutoa huduma zake kwa wananchi kwa ufanisi na gharama nafuu. Aidha, itaendelea kuihamasisha jamii kusimamia hifadhi na utunzaji wa rasilimali za maji katika maeneo yote nchini, kupanua miradi mipya na kuendeleza kazi ya uchimbaji visima. Ni wajibu wetu sote kama Taifa kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji na kuhakikisha kuwa wale wote wanaoendesha shughuli ambazo zinaathiri vyanzo hivyo wanaondolewa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mafanikio ya Awamu ya Kwanza ya *TASAF* katika Wilaya 40 za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, Serikali imeamua kuwa na Awamu ya Pili ambayo itatekelezwa katika Halmashauri zote za Wilaya, Miji na Manispaa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2005. Madhumuni ya Awamu hiyo ya Pili iliyozinduliwa na Mheshimiwa Rais, Benjamin William Mkapa, tarehe 23 Mei 2005, ni kujenga uwezo wa jamii katika kuanzisha miradi inayoweza kuchangia kuinua hali ya

maisha kwa kuzingatia malengo ya Maendeleo ya Milenia kama ilivyoainishwa kwenye MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, katika awamu hiyo, miradi pekee ambayo itachangiwa na *TASAF* ni ile iliyoainishwa na Sekta husika za Afya, Elimu, Maji, Ustawi wa Jamii, Uvuvi, Chakula na Ushirika. Sekta nyingine ni Barabara, Misitu, Madini, Benki na Masoko. Natoa wito kwa Viongozi wa Serikali za Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Halmashauri za Miji na Manispaa na Asasi mbalimbali za maendeleo kutumia nafasi hiyo na kuwaongoza vizuri wananchi Katika kutekeleza miradi itakayowaletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Serikali itaanza kutekeleza Awamu ya Pili ya Mpango Maalumu wa Kukomesha Utumikishwaji Watoto. Katika awamu hiyo, Sekta zote za uzalishaji na huduma zitahusishwa kwenye mpango huo kama ilivyoainishwa kwenye MKUKUTA. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na wadau itakamilisha taarifa ya pili ya utekelezaji wa Mkataba wa Afrika Kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto ambayo itawasilishwa Umoja wa Afrika. Natoa wito kwa Watanzania tuendeleo kuchukua hatua madhubuti zenye lengo la kupambana na matatizo mbalimbali yanayowakabili watoto.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji kwa kuimarisha utoaji wa habari na kukamilisha Muswada wa Sheria ya Uhuru wa Habari. Aidha, Serikali itaendelea kupanua na kusambaza huduma za Televisheni ya Taifa na Radio Tanzania kwa kukamilisha ujenzi wa minara katika Vituo vya Tabora, Kigoma, Bukoba, Musoma, Lindi, Mbeya na Tanga itakayowezesha matangazo ya Vituo hivyo kupatikana katika eneo kubwa zaidi nchini. Kukamilika kwa Vituo hivyo kutawezesha Serikali kuanza ujenzi wa Vituo kwa Mikoa mingine iliyosalia.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwa na mawasiliano ya mara kwa mara na kuwa na Vikao vya pamoja na wamiliki na Wahariri wa Vyombo vya Habari kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba utendaji wa vyombo hivyo hauathiri maslahi ya Taifa hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu.

Napenda kutoa wito kwa vyombo vyote vya habari kuelewa kuwa vina wajibu mkubwa kuhakikisha kuwa demokrasia inadumishwa na kuendelezwa. Hivyo, ni muhimu kwa vyombo hivyo kuchapisha na kutangaza habari zao kwa uwiano mzuri na kuepuka ushabiki, uchochezi, kashfa na matusi, mambo ambayo yanaweza kuathiri misingi imara iliyopo ya umoja, amani na mshikamano wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hali ya UKIMWI bado ni mbaya katika nchi yetu na kama nilivyoeleza, tutaendelea na hali ya kukabiliana na tatizo la UKIMWI. Utafiti wa hivi karibuni unaonyesha kwamba wastani wa asilimia saba ya Watanzania wana virusi vya UKIMWI. Kiwango hicho kinaweza kuongezeka kwa kasi na kuangamiza Taifa. Kwa hiyo, kama inavyosisitizwa kwenye Sera na Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, udhibiti wa ugonjwa huo miongoni mwa jamii yetu ni eneo linalostahili kupewa

kipaumbele. Wizara zote zina mipango na bajeti ya kutekeleza shughuli za kudhibiti UKIMWI.

Kamati shirikishi zilizoundwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe, zinatarajiwa kushirikisha na kuhamasisha wananchi katika maeneo yao, hususan katika kutambua athari za UKIMWI na kujiepusha na maambukizo. Tume ya Kudhibiti UKIMWI imeteua Wakala watakaosaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kushirikisha Sekta mbalimbali, Asasi zisizo za kiserikali na Sekta binafsi katika kuimarisha mwitikio wa wananchi dhidi ya UKIMWI.

Ni muhimu tukatambua kwamba matokeo mabaya ya UKIMWI tunayoyaona hivi sasa ni kielelezo kwamba jamii yetu haijawa makini ipasavyo katika kudhibiti UKIMWI, hasa katika kuzuia maambukizo mapya. Hivyo, ninatoa wito kwa viongozi wote kushirikiana kuhimiza utekelezaji wa harakati za kudhibiti UKIMWI na kuhamasisha zaidi wananchi katika maeneo yao hususan katika kipindi cha kampeni za Uchaguzi zitakazoanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeridhia na inatekeleza mikataba na itifaki zinazohusiana na udhibiti wa dawa za kulevya. Aidha, upo mwongozo wa utoaji matibabu, mafunzo ya ushauri nasaha kwa Watendaji na kuwaelekeza Waathirika sehemu ya kwenda kupata matibabu. Nchi yetu inashirikiana na nchi nyingine na Taasisi za Kimataifa zinazoratibu udhibiti wa dawa za kulevya ili kujifunza mbinu za kisasa za kudhibiti uingizaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

Katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya na kutoa elimu kwa Umma kuhusu madhara yanayosababishwa na dawa hizo. Serikali itaendelea kupambana na uingizaji wa dawa za kulevya nchini kwa kuongeza uwezo wa Idara na Wakala wa Serikali katika kusimamia mipaka, Bandari na viwanja vya Ndege.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha takriban miaka kumi, Serikali imefanya kazi kubwa ya kujenga uchumi unaokua. Pamoja na mafanikio yanayoonekana, bado ukuaji huo hautuwezeshi kupambana kikamilifu na umaskini. Mahitaji ya wananchi yanaongezeka kutokana na ongezeko la idadi ya watu ambalo sasa ni asilimia 2.9 kwa mwaka. Kwa msingi huo, bado tuna kazi kubwa mbele yetu. Tunachoweza kujivunia hivi sasa ni kuwa tumeweka misingi imara ya ukuaji wa uchumi tulivu na endelevu na tunao mwelekeo wenye matumaini makubwa.

Wito wangu kwa Watanzania ni kuwataka watambue kuwa suala la kujenga uchumi imara halina njia ya mkato. Tunahitaji kuongeza tija katika sehemu zetu za kazi hususan kwenye Sekta za Uzalishaji na vilevile kuendeleza utekelezaji wa hatua zote zitakazotuwzesha kukuza uchumi kwa viwango vikubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, utandawazi na mabadiliko ya teknolojia yanasababisha masuala ya uwekezaji, biashara na ajira kuvuka mipaka ya nchi na nchi. Pamoja na

ongezeko kubwa la uwekezaji na shughuli za biashara nchini ambalo limewawezesha Watanzania wengi zaidi kupata ajira katika Sekta rasmi. Bado Watanzania tunakabiliwa na changamoto ya kuhakikisha kuwa tunaweza kushindana kwenye soko la ajira. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, pamoja na kuwa na sifa za elimu au hata uzoefu, tunao wajibu wa kuwa na nidhamu katika kazi.

Wawekezaji wanawekeza wakitegemea kupata faida na hivyo kurudisha gharama zao. Ili malengo yao hayo yafikiwe, wanategemea waajiriwa wao waonyeshe uwezo, ujuzi na nidhamu katika kazi. Kwa vile, soko la ajira Afrika Mashariki linaelekea kuwa moja, Watanzania hatuna budi kuongeza jitihada ili tusinyang'anywe nafasi za ajira na wenzetu wa nchi nyingine za Afrika Mashariki. Wale wenye sifa na uwezo wawe wajasiri kutafuta ajira katika masoko ya nje hususan nchi za jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kilimo bado kitaendelea kuwa mhimili wa uchumi wa familia nyingi nchini. Serikali imechukua hatua za kuongeza bajeti katika Sekta hiyo kwa lengo la kuwawezesha wakulima kutumia fursa zinazojitokeza kupanua na kuboresha kilimo chao na hivyo kujiongezea kipato. Tunazo programu mbalimbali zinazotekelezwa zinazolenga kuongeza tija katika uzalishaji, huduma za ugani na huduma za masoko.

Kwa msingi huo, Wataalamu wa Kilimo na Viongozi katika ngazi za Vijiji, Kata, Tarafa na Wilaya wanao wajibu wa kuwafikia wakulima ili kuwawezesha kunufaika na hatua hizo za Serikali. Pamoja na hatua hizo, tunao wajibu vilevile wa kuongeza nguvu zaidi katika usindikaji wa mazao ya kilimo kama njia ya kuongeza thamani ya mazao na hivyo kuwawezesha wakulima kupata mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikiwa katika kilimo, eneo ambalo hatuna budi kulipa msukumo mkubwa ni lile la usindikaji wa mazao. Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo limetoa mafunzo kwa wajasiriamali katika maeneo mbalimbali nchini katika teknolojia ya usindikaji wa mazao. Tumeshuhudia katika maonyesho mbalimbali ya wasindikaji wa mazao ya kilimo, jinsi ubora wa bidhaa hizo unavyoongezeka.

Ni wajibu wa viongozi na wataalamu kuwasaidia na kuwapa moyo wale wote wanaothubutu kuwekeza katika eneo hilo na maeneo mengine yenye lengo la kubadili kilimo chetu. Jukumu la Serikali ni kuweka mazingira yatakayowezesha kuondolewa kwa vikwazo vinavyowazuia wajasiriamali wengi zaidi kujitokeza, hasa wenye uwezo wa kujenga na kuendesha viwanda vikubwa vya usindikaji.

Mheshimiwa Spika, Soko la Afrika Mashariki hivi sasa ni moja. Vilevile, eneo la nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika nalo ni eneo huru la biashara. Zipo pia fursa kwa Watanzania kupenya katika masoko ya Ulaya na Marekani Kaskazini kutokana na mazingira ya masharti nafuu yaliyowekwa na nchi hizo kuwezesha bidhaa za nchi zinazoendelea kupenya kwenye masoko yao. Pamoja na kuwepo kwa fursa hizo, bado Watanzania hatujazitumia kikamilifu. Kwa jumla bado ni Watanzania wachache sana wamethubutu kujiingiza katika uwekezaji wenye lengo la kuingia kwenye masoko hayo.

Mazingira ya kiuchumi yaliyopo nchini hivi sasa yanatoa fursa kwa Watanzania kujifunza na hivyo kujiandaa kuwekeza katika Sekta mbalimbali. Aidha, ongezeko la Taasisi za fedha linatoa fursa ya kupatikana kwa mikopo ya kuwawezesha wajasiriamali kujenga uwezo wao. Wito wangu kwa Watanzania ni kuwa tubadilike sasa na tuwekeze katika maeneo yatakayotuwzesha kupenya kwenye masoko ya nje.

Bila kuongeza uwezo wetu wa kuuza bidhaa nje, hatuwezi kuongeza utajiri nchini. Serikali ni mdau muhimu sana katika jambo hili, lakini wadau wengine muhimu zaidi ni wazalishaji na wafanyabiashara wa kuuza nje. Tusiogope kutumia rasilimali tulizonazo kwa utaratibu endelevu na unaozingatia maslahi ya Taifa ya sasa na ya vizazi vijavyo. Ni wajibu wetu kutambua kuwa rasilimali hizo zikitumika vyema ni kichocheo kikubwa cha kutuwzesha kupambana na umaskini na hivyo kuwa nchi tajiri. Kwa hiyo, tutumie utaalamu na teknolojia kutoka nje kama nyenzo za kutuwzesha kufikia malengo yetu ya kuzalisha kwa wingi na kuuza katika masoko ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amani na utulivu wetu ni kigezo na nguzo muhimu sana ya maendeleo tunayoyategemea. Uchumi wetu unakua vizuri na wawekezaji wa nje na ndani wanawekeza kwa sababu kuna amani. Utawala bora unakuwepo kwa sababu kuna amani. Hivyo, tahadhari yangu kwa Watanzania ni kuwa, kama tunataka mafanikio yote tunayoyaona yayeyuke, tuchezee amani yetu. Amani yetu ni mali ya Watanzania na siyo mali yetu Viongozi wala mtu yeyote. Aidha, Muungano wetu ni mhimili mkubwa wa amani yetu. Hivyo ni muhimu kudumisha Muungano ili amani idumu nchini.

Mwaka huu tuna uchaguzi kama nilivyokwishaelezea awali. Shughuli za uchaguzi huwa zinaweza kuwa chanzo cha kuvuruga amani na utulivu kama Viongozi wa Vyama vya Siasa na mashabiki wao wasipokuwa waangalifu. Naomba Vyama vyote vya Siasa tuwe wadau wakubwa wa kulinda amani na utulivu hasa wakati huu wa uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapokaribia mwisho wa kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu, Watendaji Serikalini wanao wajibu wa kufanya maandalizi yote muhimu yatakayowezesha makabidhiano ya Serikali kufanyika kwa ufanisi mkubwa. Nchi yetu inao uzoefu wa kutosha wa makabidhiano ya uongozi wa nchi. Wakati viongozi wa kisiasa watakapokuwa kwenye harakati za kuomba ridhaa ya kuongoza kutoka kwa wananchi, Watendaji wa Serikali wataendelea kutekeleza majukumu yao kikamilifu ili kuiwzesha Serikali ijayo kuanza kazi vizuri bila kuonekana pengo lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu imepata mafanikio makubwa na ya kujivunia katika utekelezaji wa sera na mipango mbalimbali. Mafanikio hayo ni matunda ya uongozi thabiti wa Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, pamoja na mshikamano na Uongozi wa pamoja wa Viongozi na watumishi wote wa Umma.

Napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kutuongoza, kutoa dira sahihi na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa majukumu yote ya Serikali yake. Ninawashukuru vilevile Mawaziri na Naibu Mawaziri, kwa kutekeleza majukumu yao

kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kunipa ushirikiano mkubwa. Nawashukuru Wakuu wa Mikoa na Wilaya na Makatibu Tawala wao na Wakurugenzi Watendaji wote kwa kusimamia shughuli za maendeleo katika maeneo yao ya utawala. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na Taasisi zake chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi, Mheshimiwa Martin Lumbanga pamoja na vyombo vyote vya dola kwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Napenda pia kuwashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na Taasisi zake kwa kuiwezesha Serikali kila mwaka kukamilisha maandalizi yote ya bajeti za Serikali kwa wakati pamoja na makadirio ya matumizi ya fedha za kila Wizara, Mikoa, Asasi na Idara zinazojitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nimekuwa Waziri Mkuu kwa vipindi vyote viwili vya Serikali ya Awamu ya Tatu. Hivi sasa tunafikia mwisho wa awamu hiyo iliyoongozwa kwa umakini mkubwa na Rais Benjamin William Mkapa. Kwa vyovyote vile, huu ni Mkutano wangu wa mwisho na hii ni bajeti yangu ya mwisho kuiwasilisha kama Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa Waziri Mkuu, lazima uwe Mbunge wa Jimbo. Hivyo, ninapenda kuwashukuru sana kwa dhati wapigakura wangu wa Jimbo la Hanang ambao wamenichagua kwa vipindi vinne mfululizo. Lakini pia huwezi kuwa Waziri Mkuu mpaka Rais akuteue na Wabunge wathibitisha uteuzi huo. Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa imani kubwa aliyonayo kwangu na hivyo kuiteua mara zote mbili kuwa Waziri Mkuu. Ninamshukuru pia kwa jinsi alivyoniipa fursa ya kufanya kazi naye kwa karibu na hivyo kuniwezesha kujifunza mengi kutoka kwake. *(Makofi)*

Vile vile ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuidhinisha uteuzi wa Rais mara zote mbili kwa kunipigia kura nyingi sana za “Ndiyo”. Mwaka 2000 nilipata kura zote isipokuwa kura tatu tu. Nawashukuru sana. Hiyo ni heshima kubwa sana kwangu. Zaidi ya kuthibitisha uteuzi wa Rais, Waheshimiwa Wabunge, mmenipa ushirikiano mkubwa sana katika kipindi chote nikiwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Nasema ahsanteni sana.

Niwashukuru kipekee Waheshimiwa Wabunge wa CCM ambao walinipa ushirikiano mkubwa hasa katika Vikao vya Wabunge wa CCM kama Kamati Maalumu ya Chama. Nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kutokana na ushirikiano mkubwa uliopo kati ya uongozi na wafanyakazi wote. Kwa namna ya pekee, napenda niwashukuru Mawaziri wote na Makatibu Wakuu ambao waliwahi kukabidhiwa majukumu katika Ofisi ya Waziri Mkuu, katika kipindi hicho cha miaka kumi. Tunaithamini sana michango yao kwani imesaidia katika kuiwezesha Ofisi ya Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Kwa namna ya pekee, ninawashukuru Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Habari na

Siasa kwa ushauri na msaada mkubwa walioutoa kwangu katika utekelezaji wa majukumu ya kazi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Namshukuru sana Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Bibi Rose Lugembe na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Asasi zilizo chini yake kwa ushauri wao wa kitaalamu ambao umeniwezesha mimi binafsi na Mawaziri wa Nchi, kutekeleza kazi zetu bila matatizo. Ninawashukuru vilevile kwa kukamilisha maandalizi yote ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mwaka 2005/2006. Namshukuru Mpiga Chapa wa Serikali kwa kuichapa hotuba hii kwa unadhifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepiga hatua kubwa ya maendeleo katika sekta na nyanja mbalimbali kutokana na mchango mkubwa wa misaada na mikopo kutoka kwa Wahisani mbalimbali. Wahisani hao ni Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Taasisi za Fedha za Kimataifa, nchi rafiki, nchi fadhili, Mifuko mbalimbali, Madhehebu ya Dini na Asasi Zisizo za Kiserikali. Wote hao ni mashahidi wa jinsi tulivyotumia misaada na mikopo yao vizuri kuleta mabadiliko makubwa katika sekta na nyanja mbalimbali. Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wote kwa dhati na kuwahakikishia kuwa Watanzania tunathamini sana mikopo na misaada yao. *(Makofi)*

Aidha, kwa niaba ya Watanzania wote, ninapenda kuwathibitishia kuwa tutaendelea kushirikiana nao katika harakati zetu za kupiga vita umaskini na kujenga uchumi imara na endelevu. Napenda kushukuru kundi G8 ambalo hivi karibuni pia limesamehe madeni kwa nchi maskini 18 na nchi yetu Tanzania ikiwa mmojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2005/2006, Ofisi ya Waziri Mkuu na Asasi zake pamoja na Ofisi ya Bunge, inaomba jumla ya Sh. 95,446,396,900/= kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo. Kati ya fedha hizo, Ofisi ya Waziri Mkuu na Asasi zake inaomba jumla ya Sh. 65,806,519,700/= na Ofisi ya Bunge inaomba jumla ya Sh.29,639,877,200/=.

Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu na Asasi zake inaomba jumla ya Sh.45,426,197,100/= kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, Sh.2,000,000,000/= ni fedha za hapa nchini na Sh.43,426,197,100/= ni fedha za nje. Ofisi ya Bunge inaomba jumla ya Sh.950,000,000/= fedha za hapa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imechukua muda mrefu kwa sababu imejumuisha mambo yote ya miaka kumi. Baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Orodha ya Waheshimiwa Wabunge walioomba kupewa nafasi ya kuchangia imeshawekwa kwenye ubao wetu wa matangazo. Niseme tu kwamba, kwa sababu hata hoja ya Waziri Mkuu inazungumzia Serikali kwa ujumla, ni sawa sawa na Bajeti. Kwa hiyo, anayechangia hawezi kuambiwa zungumzia hoja iliyoko mbele yetu. Kwa chochote utakachozungumza kiko ndani ya hoja.

Kwa ajili hiyo, basi tutawapa nafasi wale ambao hawakuchangia kwenye Bajeti yenyewe. Kwa hiyo, ndiyo wanaoorodheshwa kwanza na kama nafasi itabaki waliochangia kwenye Bajeti wanaweza na wao wakapewa nafasi. Hii ni kwa utaratibu wetu wa kuwezesha Wabunge wengi kadri inavyowezekana waweze kupata nafasi ya kuishauri Serikali. Sasa namwita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala atoe maoni ya Kamati. *(Makofi)*

MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, Kamati yangu haikuwahi kupata fursa ya mapitio ya miaka kumi ya utekelezaji katika Awamu ya Tatu kama yalivyowasilisha na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, maoni ya Kamati yatakuwa yamezingatia zaidi mapitio ya mwaka 2004/2005 na Bajeti ya mwaka 2005/2006.

Lakini niseme kwamba nimemsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli Serikali inastahili kupongezwa sana kwa kazi nzuri iliyofanya katika kipindi hiki cha miaka kumi. Nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuweza kuhimili kuiwasilisha hoja yake kwa muda wa karibu masaa mawili na robo bila ya kutetereka. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yale aliyoyaeleza ni dhahiri kabisa kwamba yatawaziba midomo wale ambao wanajaribu sana kutoa dosari ya utekelezaji wa Serikali. Kama alivyosema mwenyewe katika hitimisho lake kwamba tunao mwelekeo wenye matumaini makubwa ambao Ndugu yangu Mramba aliita mdundiko, kwa hiyo, wale ambao wamavamia mdundiko bila kujua harusi ni ya nani, sasa nadhani watajua kwamba harusi hii ni ya nani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, sasa naomba kuwasilisha Taarifa na Maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Utekelezaji wa kazi katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa Fedha wa 2004/2005 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2005/2006 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya majukumu ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ni kushughulikia bajeti za Wizara kama ilivyoainishwa katika Kanuni Na. 93, Kanuni za Bunge, Toleo la 2004. Kwa mujibu wa Kanuni hiyo, Kamati imepewa jukumu la kushughulikia Bajeti za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hili, tarehe 23 - 26 Mei, 2005, Kamati ilipata fursa ya kuchambua utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2004/2005 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa Fedha 2005/2006. Katika Vikao hivyo, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib - Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Habari na Siasa), akishirikiana na Mheshimiwa William Lukuvi - Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera).

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu inahusisha Mafungu yafuatayo:-

Fungu 25 - Ofisi ya Waziri Mkuu mwenyewe, Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 42 - Ofisi ya Bunge, Fungu - 61 Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Fungu 91 - Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawu za Kulevya na Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.

Mheshimiwa Spika, dira na majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu yameainishwa katika kitabu cha Muhtasari wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mafungu yaliyotajwa hapo juu kilichowasilishwa mbele ya Kamati. Kwa muhtasari Dira ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ni kuwa na mamlaka yenye ufanisi mkubwa katika kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali katika sekta zote.

Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake ina majukumu kadhaa yakiwemo, kuratibu na kusimamia kwa makini na ufanisi shughuli zote za Serikali katika Sekta zote na ndani ya Bunge, kuelimisha, kuziunganisha na kuziwezesha Taasisi mbalimbali kitaifa kuchukua tahadhari na kinga dhidi ya maafa, kuratibu utekelezaji wa miradi inayogusa Sekta nyingi, kuwa kiungo kati ya Serikali na Vyama vya Siasa, kuratibu shughuli za kudhibiti UKIMWI kitaifa na akadhalika na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa ameeleza hapa amegusa maeneo hayo yote.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa maagizo ya Kamati kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005. Wakati wa kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa Fedha wa 2004/05, Kamati kwa niaba ya Bunge ilitoa jumla ya maagizo nane. Nayo yalihusu, Mpango wa Kuhamia Makao Makuu Dodoma, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Kitengo cha Maafa, Televisheni ya Taifa, Redio Tanzania, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Ofisi ya Spika na Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawu za Kulevya.

Ufafanuzi wa kina wa utekelezaji wa maagizo haya umo katika kurasa 15 hadi 22 za kitabu cha Muhtasari wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu nilichokitaja awali.

Mheshimiwa Spika, kwa jumla, maagizo yetu mengi yametekelezwa ipasavyo isipokuwa agizo moja tu la Mpango wa Kuhamia Makao Makuu Dodoma ambao nafurahi kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliuzungumzia tena katika hoja yake ya mwaka huu. Kwa taarifa ni kwamba, katika mwaka wa Fedha uliopita, Kamati iliagiza kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu iwe na ratiba ya utekelezaji. Narudia. Iwe na ratiba ya utekelezaji wa

shughuli zote za kuhamia Dodoma awamu kwa wamu na ratiba hiyo iwe wazi ikionyesha muda wa Wizara na Taasisi kuhamia Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi Serikali ilijibu kama ifuatavyo:- Nanukuu. “Nia ya Serikali ya kuhamia Makao Makuu Dodoma ipo pale pale haijabadilika. Tatizo lililopo ni uwezo mdogo wa Serikali kifedha kutekeleza azma hiyo mara moja. Pamoja na hali hiyo, azma ya kuhamia Dodoma inaendelea awamu kwa awamu”.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona kuwa majibu haya hayakujielekeza kwenye agizo la msingi ambalo ni kutoa ratiba ya Serikali kuhamia Dodoma. Kutokana na upungufu huo, Kamati bado kwa niaba ya Bunge, inaiagiza Serikali itekeleze agizo hili kikamilifu, kwani kwa kufanya hivyo, Kamati inaamini kuwa wote tutafahamu ni lini na Wizara zipi zinahamia Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka wa Fedha 2005/2006 katika mwaka huu wa fedha, Kamati yangu ilielezwa kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu imepanga kufanya kazi zifuatazo: -

Uhamasishaji wa shughuli za maendeleo ya wananchi Mijini na Vijijini, Uratibu wa shughuli zote za Serikali katika Sekta zote na ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kusimamia mapambano ya vita dhidi ya UKIMWI, rushwa na dawa za kulevya; kuendeleza ujenzi wa vituo vya kurushia matangazo ya *TVT* na uimarishaji wa mitambo ya *RTD*.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine ni kuratibu na kusimamia miradi mbalimbali iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kuimarisha uwezo wa kukabili maafa, kusimamia shughuli za uchaguzi nchini, kuendelea na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2005, kuimarisha Idara ya Kupiga Chapa ya Serikali; Kuimarisha Huduma za Bunge ikiwa ni pamoja na kuendeleza ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi ya Dar es Salaam na Zanzibar na kuweka samani na kusimamia, kuratibu na kuwa kiungo kati ya Serikali na Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2005/2006, Kamati ilielezwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, imelenga kutekeleza majukumu ya kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali, zikiwemo: kuandaa mazingira mazuri yatakayosaidia ustawi na uendeshaji wa Vyombo vya Habari vya Umma, kuboresha mandhari na miundombinu ya Makao Makuu Dodoma, kukamilisha ukarabati wa Ofisi ya Bunge Dar es Salaam na ujenzi wa Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar na uwekaji wa samani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake iliomba Kamati iidhinishie jumla ya Sh.141,882,594,250/=. Kati ya fedha hizo Sh. 95,446,397,100/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.46,376,197,150/= ni kwa ajili ya mpango wa maendeleo. Kwa jumla Kamati yangu baada ya uchambuzi wa kina wa mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake imeridhika na

maelezo yaliyotolewa, lakini pamoja na kuridhika huko bado Kamati imelazimika kutoa maagizo mapya kwa niaba ya Bunge kwa mwaka 2005/2006 katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza mpango wa kuhamia Makao Makuu Dodoma, Kamati imeagiza kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu iweke ratiba inayoeleweka ya kuhamia Makao Makuu Dodoma kama ilivyoagizwa mwaka 2004/2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, katika Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevywa kuna maagizo mawili. La kwanza katika eneo hili Kamati imeagiza kuwa:-

- (i) Elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi kuhusu madhara ya dawa za kulevywa;
- (ii) Serikali izifanyie marekebisho sheria zilizopitwa na wakati zinazotoa mwanya wa kuzidisha kasi ya matumizi ya dawa za kulevywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha niliyoyasema, ndiyo maelezo ya uchambuzi wa Kamati yangu kwa muhtasari. Kama yapo maeneo mengine ambayo sikuweza kuyagusia, natumaini Wajumbe wa Kamati hii watakapata nafasi ya kuweza kuchangia, watajazia pale ambapo mimi nimeachia.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii kuwasilisha maoni ya Kamati katika kipindi hiki cha mwisho wa uhai wa Bunge. Napenda kukupongeza kwa dhiti kabisa kwa kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu katika kipindi chote hiki. Aidha, napenda nimpongeze Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti - Mbunge na Naibu Spika, kwa kazi nzuri aliyoiyonyesha ya kuliongoza Bunge wakati wote ulipomwachia madaraka ya kufanya hivyo. Vilevile nawapongeza, Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa na Mheshimiwa Anne S. Makinda, kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao ulipowaachia kuongoza Vikao vya Bunge. *(Makofi)*

Pili, napenda niwashukuru, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib - Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu mwenye jukumu la Habari na Siasa na Mheshimiwa William Lukuvi - Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu mwenye jukumu la Sera na wataalamu wao kwa kushirikiana vyema na Kamati walipowasilisha Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa michango yao ya kina wakati wa kuichambua bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake na kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge, tulipopewa dhamana ya kuishughulikia bajeti ya Ofisi hii. Naomba niwatambue kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Athumani S.M. Janguo, anayesoma hotuba hii, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru - Mjumbe, Mheshimiwa Grace Kiwelu - Mjumbe, Mheshimiwa Rosemary Nyerere -

Mjumbe, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis - Mjumbe, Mheshimiwa Khamis Salum Ali - Mjumbe, Mheshimiwa Ramadhani H. Khalfan - Mjumbe, Mheshimiwa Juma S. N'hunga - Mjumbe, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri - Mjumbe, Mheshimiwa Paschal Degera - Mjumbe, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte - Mjumbe, Mheshimiwa Chifu Abdallah S. Fundikira - Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa - Mjumbe, Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mjumbe, Mheshimiwa Mwanne Mchemba - Mjumbe, Mheshimiwa George F. Mlawa - Mjumbe, Mheshimiwa Raynald Mrope - Mjumbe, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma - Mjumbe, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe - Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Nimrod Mkono - Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai - Mjumbe na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare - Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda niwashukuru Ndugu Athumani Hussein, Charles Mloka na Ernest Zulu, Makatibu wa Kamati hii chini ya Uongozi wa Bwana Damian Foka, Katibu wa Bunge, kwa kuihudumia Kamati vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda nikutakie kila la heri katika mwaka huu wa fedha, nawatakia kila la kheri pia Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kinyang'anyiro kijacho cha uchaguzi. Mungu atujalie tukutane tena Novemba, mosi mwaka huu. Kwa walioamua kung'atuka, nawatakia kila la kheri huko waendako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia na ninaomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. WILFRED M. LWAKATARE - KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI - OFISI YA WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kufuatana na hotuba ya bajeti iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nitoe maoni na mtazamo wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga na wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kuondokewa na mpendwa Mbunge wao.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Ibrahim Lipumba, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, Mheshimiwa Juma Duni, Mheshimiwa Agustino Lyatonga Mrema, Mheshimiwa Rukia Kiota, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Amani Abeid Karume na Mheshimiwa Dr. Shein kwa kuteuliwa na Vyama vyao kugombea Ofisi kubwa za utawala wa nchi. *(Makofi)*

Pia, nawapongeza wale wote ambao tayari wamebahatika kushinda kura za maoni kupitia Vyama vyao, nikiwemo mimi mwenyewe kugombea nafasi za Ubunge, Uwakilishi na Udiwani. Pia niwashukuru wananchi wa Bukoba Mjini na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama kwa kuiteua na kuniamini kukiwakilisha Chama katika kinyang'anyiro kinachokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napongeza hotuba zote ambazo zimetangulia kuwasilishwa hapa Bungeni, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Waziri wa Fedha na hii iliyotolewa hivi punde ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na hususan hotuba ya Waziri wangu Kivuli kwa Wizara ya Mipango na Ubinafishaji na Wizara ya Fedha, Mhe. Hamad Rashid Mohamed. *(Makofi)*

Hotuba iliyowasilishwa na Mheshimiwa Hamad Rashid, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, imetoa mtizamo halisi wa jumla wa Kambi dhidi ya Mipango ya Bajeti ya Serikali kama ilivyowasilishwa na Mawaziri husika na zaidi ya yote, hotuba hiyo imekata kiu ya wale ambao huwa wanafikiria Upinzani hauna Sera, hauna jipya, hauna Ilani za Uchaguzi, hauna mipango thabiti, hauwezi kuongoza Serikali na kadhalika.

Hotuba yetu ya Upinzani, zaidi ya kuikosoa na kuishauri Serikali, imeeleza nini tunatarajia kufanya tukikamata madaraka mwezi Novemba mwaka huu na hivyo sitakuwa na haja kuyarudia. Nzuri zaidi, kama ambavyo imejithibitisha katika michango mbalimbali iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, hayupo aliyethubutu ku-*challenge* hoja zilizowasilishwa na Wapinzani zaidi ya baadhi tena wachache kutoa kejeli za jumla za kwamba Wapinzani wamechanjia ubishi, ni wapotoshaji, malofa na kadhalika. Tunaomba wananchi watupe kura zao tarehe 30 Oktoba, 2005 tuyaweke yale yote tuliyoaeleza katika vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumewahi kueleza katika hotuba zetu za miaka iliyopita, hotuba yetu ya mwaka 2003/2004 tulisema, kupongezana kwamba bajeti hii ni nzuri, ni jambo moja na kutekelezeka kwa bajeti hiyo ni jambo lingine” Inasikitisha hadi hivi leo Mtanzania anapojivunia kuwemo ndani ya nchi yake huru kwa miaka 43 tangu Mkoloni aondoke, wengi bado wamegubikwa na dimbwi la umaskini. Watu wachache wanafaidi wakati walio wengi hawana uhakika wa hata mlo mmoja au tiba pindi wanapougua au kuuguliwa. Pato la Mtanzania limeendelea kushuka mwaka hadi mwaka toka Dola 85.2 mwaka 1995 mpaka Dola 57.2 mwaka 2002. Jambo la kujiuliza ni kwamba hizi bajeti tunazoambiwa ni za kuwakomboa Watanzania mwaka hadi mwaka, mbona hazibadili hali za Watanzania walio wengi? Mbona zinaonekana kwenye makaratasi na wengi kuishia kunawa tu. Mbona Watanzania zaidi ya asilimia 90 bado wanausikia umeme kwenye redio?

Mheshimiwa Spika, imefika wakati Watanzania watayarishiwe bajeti ya kweli itakayowawezesha kupambana na umaskini wa kipato. Watu wamechoka na misamiati mipya ya kila kukicha; mara MKUKUTA, mara MKURABITA, mara *TASAF*, mara *BEST* na kadhalika. Watanzania wanataka pesa mifukoni, sio lugha zinazobadilika badilika kila siku lakini umaskini na ufukara vinazidi kutawala kwa watu wengi. Pamoja na Serikali kupenda kutumia tulichonacho (*cash budget*) lakini ni wazi utaratibu huo

unafanya bajeti iliyopitishwa na Bunge kutokuwa na dira madhubuti ya matumizi ya Serikali. Huenda Hazina wanapendelea kuendelea na utaratibu huu kwani unawapa madaraka zaidi ya kugawa fedha baada ya bajeti kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inampongeza Rais Mkapa na Serikali yake kwa jitihada walizoweza kuzifanya kwa kuyafanya hayo waliyoweza kuyafanya kwa miaka 10. Lakini ukimsifia sana mgema, tembo hilitia maji. Ni vyema kama kweli tunataka kuwasaidia Viongozi wetu na tunawapenda bila unafiki au kujifagilia kwa nia fulani fulani na vile vile kama tunataka kujenga misingi mizuri ya utawala endelevu, pale ambapo Viongozi wetu wanahitaji kukosolewa, ni vyema tukawaeleza. Penye kasoro tupataje, walipovurunda tupabainishe na hiyo itakuwa njia nzuri ya kurekebisha mambo na wananchi kunufaika.

Vile vile, itakuwa njia bora ya kuwafanya Viongozi walioko madarakani au wajao kujirekebisha. Vinginevyo sifa za jumla jumla tu tunazozitoa, zilizojaa mazuri kemkem, zitatufikisha mahali ambapo jamii fulani katika nchi fulani kutokana na kumwogopa sana mtawala wao na hivyo kutokuwa tayari kumweleza ukweli, walifikia mahali pa kumsifia kwamba nguo aliyovaa imemkaa vizuri sana na inampendezesha, kumbe katika hali halisi alikuwa yuko uchi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema “Hatuwezi kusema kwamba sisi hali yetu ni nzuri kwa sababu ya kujifaninisha na wagonjwa.” Kuna mambo hivi sasa tunajisifia kwamba tumefanya vizuri sana kwa sababu huko nyuma sisi wenyewe tulishazoea kutofanya kabisa. Lakini kwa sababu hivi sasa tunapofanya hako kadogo tena kwa sababu ya kusukumwa na Wapinzani ili tusinyang’anywe tonge la ugali, basi kujisifia kunazidi mno.

Niliwahi kusema humu Bungeni katika hotuba yangu ya mwaka 2004/2005 na nanukuu: “Kambi ya Upinzani inapongeza na inayaona yale yote mazuri yanayofanywa na Serikali ya CCM, lakini ukweli ni kwamba mnafanya mazuri machache mno kuliko yale mazuri mengi mno ambayo yangefanywa na Serikali iliyo makini na iliyojipanga vizuri.” Wabunge ni Viongozi wanaosafiri mno nje ya nchi: Je, nchi nyingi mnazotembelea zina hali sawa na nchi yetu? Je, maajabu mnayoyakuta huko yanatengenezwa kwa uchawi au binadamu kama sisi?

Mheshimiwa Spika, tunaomba wenzetu kwa uungwana wakubali kwamba, “jambo usilolijua ni sawa na usiku wa giza”. Tufike mahali pa kukubaliana sisi sote kama Watanzania kwamba kila mmoja wetu ana wajibu wa kutoa mawazo yatakayonusuru nchi yetu na janga la umaskini, ujinga na maradhi bila kupuuzwa kwa sababu za kiitikadi, kikabila au kiuwezo. Umefika wakati wa kuainisha na kukubaliana juu ya sera za Kitaifa ambazo sisi wote inabidi tuzilinde na kuzisimamia. Masuala ya ulinzi, ardhi, elimu, mambo ya nje, ni mambo yanayopaswa kupangiwa mipango isiyobadilika wala kuyumba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri zilizofanywa na Serikali zetu za Awamu ya Tatu kwa Serikali ya Muungano na ya sita (6), kwa Zanzibar, yafuatayo lazima yawekwe bayana kwa faida ya awamu zijazo na kuweka kumbukumbu sawa.

Pamoja na Rais wetu kuwa mstari wa mbele kuwasisitiza Viongozi wenzake wa *SADC* kuwa Serikali zitenge angalau asilimia kumi ya bajeti kwa Sekta ya Kilimo katika wakati wake wote kama Rais, Serikali imetenga chini ya asilimia tano ya bajeti yake katika Sekta ya kilimo.

Serikali ya CCM inaendelea kutoa msisitizo wa kukaribisha wakulima wakubwa kutoka nje wapewe mapande ya ardhi kukuza kilimo, lakini mkulima mdogo amesahauliwa. Serikali inaeleza kuwa inatoa ruzuku kwa pembejeo ili bei ziwe nafuu. Hivi sasa bei ya mbolea Mkoani Iringa ni Shs.20,000/- kwa mfuko mmoja. Utaratibu wa mikopo ili wakulima wainunue haupo. Matokeo yake wengi hawatumii mbolea na mavuno yao ni madogo na wanakabiliwa na njaa na umaskini. Kilimo cha umwagiliaji kimeendelea kuonekana kwenye vitabu na takwimu kuliko hali halisi.

Pamoja na kujisifu sana kuwa tumefanikiwa katika kukusanya kodi, mapato ya kodi yote bado ni chini ya asilimia 14 ya pato la Taifa. Bado bajeti yetu inategemea misaada kwa zaidi ya asilimia 40. Lazima tukubali ukweli kwamba bado Watanzania hatujanufaika ipasavyo na madini yetu japo yanaendelea kupungua. Ripoti ya Tume ya Serikali chini ya Uenyekiti wa Dr. Kipokola iliyokabidhiwa kwa Waziri Mkuu bado imebaki Siri ya Serikali na wala hotuba ya bajeti haigusii chochote cha kunufaika na ripoti ya Tume hiyo. Upo ukwepaji mkubwa wa kodi ambao haujafanyiwa uhakiki na Serikali na hasa unaofanyika kupitia *Tanzania Investment Centre*.

Ni kweli Serikali imeeleza kwamba imepata mafanikio makubwa katika ujenzi na ukarabati wa barabara kuu za Mikoa na Vijiji. Tunaipongeza sana Serikali, lakini inabidi tuelewe kwamba katika kipindi cha miaka tisa, ongezeko la barabara za lami ni Kilomita 957 wastani wa Kilometa 106 kwa mwaka. Mwaka 1995 Rais Mkapu alisema barabara ya lami kwenda Kusini ingekamilika kabla ya mwaka 2000. Sasa ni mwaka 2005 na anaondoka.

Hivyo, ili twende vizuri na Watanzania walio wengi wayaone maendeleo ya kimelenia, tunahitajika angalau tujenge Kilomita 300 hadi 400 za barabara za lami kwa mwaka. Hii inawezekana kabisa ili mradi kupanga mambo yetu kwa kufuata *priorities*.

Ilani ya CCM ya Mwaka 1995 ilieleza wazi kuwa Mashirika nyeti kama vile Mabenki ya biashara, Bandari, Posta na Simu, Umeme, Maji, hayatabinafsishwa. Hadi Desemba 2004, Mashirika 312 yamebinafsishwa na mali za Mashirika (*non core assets*) zipatazo 499 zimeuzwa. Hivi leo hii mtu akitaka kujua au kuona kwamba tumeuza hiki na tukapata hiki tutaonyesha nini? Ni ukweli usioplingika kwamba Serikali haipati mapato yanayostahiki kutokana na zoezi hili. Tunatapeliwa!

Mfano ni Shirika la Simu lililofanyiwa ukarabati mkubwa wa Dola milioni 250, likawa linaendeshwa kwa faida. Asilimia 35 za hisa zikauzwa Kampuni ya nje ya *MCI* kwa dola milioni 60. Serikali haikulipwa hizo fedha, pamoja na Mbunge mmojawapo wa Upinzani kutangaza humu ndani kwamba Serikali kama ingelipwa fedha angejiuzulu, badala yake Kampuni ikatumia fedha kuanzisha Kampuni ya *Celtel*. *MCI* ikadai *TTCL* inaendeshwa kwa hasara pamoja na wataalam kupitisha mahesabu ya *TTCL* kuwa ni

sahihi *MCI* wamefanikiwa kulipa Dola milioni tano tu, badala ya milioni 60. Isitoshe *MCI* haihesabu *Celstel* kuwa Kampuni tanzu ya *TTCL* bali ni Kampuni yao ya pili Tanzania. *Celstel* hivi sasa imeuzwa nje ya nchi bila Serikali kushiriki katika uamuzi huo.

Mheshimiwa Spika, hivi hatuoni kabisa kwamba Tanzania tunachezewa mchezo wa karata tatu? Ni vyema tukayaweka wazi mambo haya ili wajao wajirekebishe na wasiyarudie. Je, na haya tuyaweke katika orodha ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kati ya sifa ambayo Marehemu Mwalimu Nyerere mwaka 1995 alizunguka nchi nzima kumnadi Rais Mkapa ili achaguliwe, ilikuwa ni kuaminika kwake kwamba ni Kamanda mpambanaji wa adui rushwa. Hii leo ukitaka Mheshimiwa Rais akusute hadharani ni pale mtu atakapotamka kwamba ndani ya Serikali yake kuna rushwa iliyokomaa. Pamoja na kuwepo chombo cha kumsaidia kuchunguza, kubainisha na kupambana na rushwa (*PCB*) atakutaka ulete ushahidi badala ya kuvielekeza vyombo vyake hivyo vinavyolipwa fedha nyingi za walipa kodi visaidiane na huyo Mtanzania mwema aliyeanika hadharani vitendo hivyo vya rushwa.

Marehemu Baba wa Taifa wakati anaondoka, hakuacha hata huo msamiati wa “takrima”, ambayo kimsingi mimi naiita rushwa. Imehasisiwa na kupewa baraka zote katika Awamu hii ya Tatu. Ukishakuwa na Viongozi wanaotokana na takrima, huna Viongozi. Sio siri kwamba hivi sasa rushwa na wizi unaoimaliza nchi kuliko hata wizi wa kutumia silaha, ni wizi na rushwa inayofanyika kwa kutumia kalamu. Hii ni hatari sana na balaa zaidi na imekomaa.

Kielelezo halisi, ni ile hali ya misaada mingi na Mikataba ya mamilioni mengi ya fedha kutokubadili sura za Watanzania walio wengi wanaokopewa fedha hizo. Lazima tuelewe kwamba hicho tunachokihubiri kuhusu utandawazi ni pamoja na kuwemo ndani yake utandawizi. Tumejiingiza pia katika *network* ya *International Corruption*. Tunakubali paka ni paka, lakini pia tuelewe kuna paka mwizi (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli Awamu ya Tatu imefanya makubwa katika Sekta ya Elimu’ MMEM. MMES na kadhalika. Tunaipongeza Serikali ya CCM. Lakini lazima tukubali kwamba tuna kazi kubwa ya kufanya katika Sekta ya Elimu. Hivi sasa watoto wanaokwenda Shule za Sekondari toka Shule za Msingi, hawafiki asilimia 20% ya watoto wote wanaokuwa wamemaliza Darasa la Saba. Ripoti ya Benki ya Dunia imeonyesha hivyo. Kambi ya Upinzani inakubali kuwa mnaifanya lakini haitoshi.

Mheshimiwa Spika, katika huduma za afya, Bajeti inayotolewa katika Sekta ya Afya ni ndogo mno. Nawapongeza Waganga wa Jadi, Wakunga wa Vijijini, kwani wamekuwa kimbilio la wengi hivi sasa. Rais Mwinyi katika mwaka wake wa mwisho wa bajeti ya mwaka 1994/1995, Serikali ilitenga Shilingi billioni 28 kwa ajili ya dawa. Wakati huo Serikali yake ilikuwa inakusanya chini ya Shilingi billioni 20 kwa mwezi kama mapato ya Serikali. Hivi sasa zinakusanywa zaidi ya billioni 150 kwa mwezi, lakini fedha za dawa zimekuwa zinatengwa kidogo sana.

Kutokana na Serikali kushindwa kabisa jukumu la kujali afya ya watu wake na hasa akina mama na badala yake ikatusisitizia tujibane tule nyasi, lakini ndege na rada vinunuliwe. Tunashukuru Watanzania wameanza kutafuta njia za kujijali na kuangalia wenyewe uhai wao. Tunawashukuru na kuwapongeza Madaktari wa Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (*MEWATA*) kwa kushirikiana na *ITV* ambao wameanzisha mpango wa kuwahudumia na kuwasaidia akina mama wenye matatizo ya *cancer* za matiti kwa njia ya kuhamasisha michango ambayo imetolewa hata na watoto na wajukuu zetu, kwa kujinyima na kubana senti hamsini na Shilingi mia tunazowapa kwenda kununulia maji baridi na mahindi ya bisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Tatu imejitahidi sana kufanya ukarabati wa Ikulu katika kipindi chake chote ambapo kwa bahati mbaya inaonekana itashindwa kuacha imeukamilisha na ndiyo maana zimeombwa tena pesa. Naamini huenda Watanzania wengi hawajui bilioni inalinganaje. *PPF Tower* jengo lenye ghorofa 18 na umaridadi wake kama linavyoonekana katikati ya Jiji, limejengwa kwa billioni 20, tena baada ya aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wake Mr. Mataka kutuhumiwa na kusimamishwa kazi kwa kuvuka gharama za Mkataba wa awali wa billioni tisa.

Kwa maana hiyo, ukarabati wa Ikulu unaoendelea mpaka kiama tayari ni sawa na Jengo la *PPF Tower* tena kwa kiwango kilichodaiwa kina sura na harufu ya rushwa. Awamu ya tatu pamoja na kukusanya vizuri mapato, lakini mgawanyo, usimamizi wa mapato hayo na matumizi umekuwa na walakini.

Mheshimiwa Spika, hali za kiutumishi na haki za watumishi zimeendelea kuwa duni na za kimigogoro. Watu hawapati chao mpaka wagome au watishie kugoma. Kiwango cha mshahara na uwezo wa kimanunuzi kimepungua. Mwaka 1995 mshahara ulikuwa Sh. 45,000/= na *exchange rate* ya Dola ilikuwa Sh.560/=. Hivyo, mshahara huo ulikuwa sawa na Dola 80.35. Mwaka 2005 mshahara wa chini kwa watumishi rasmi wa Serikali ni Sh.60,000/- kwa *exchange rate* ya Sh.1,030/=. Kwa Dola ni sawa na Dola 58.25. Hiyo ina maana kwamba kipato kwa mtumishi kwa mwezi kimeanguka. Hivi mnataka watumishi hawa wale wapi kama sio ule urefu wa kamba waliyofungiwa.

Haki za wastaafu zimekuwa zikipatikana kwa mbinde na wengine kufariki bila ya kuyaona hayo mafao. Ahadi za kulipwa ambazo zimekuwa zikitolewa zimekuwa za jumla jumla na wakati mwingine kuwatia watumishi hamu na kiu ya bure kumbe malipo yenyewe hakuna au ni kiduchu. Sio siri, Ndugu zangu Walimu wanalielewa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yuko mzee mmoja mstaafu wa Morogoro aliyekwenda Hazina Dar es Salaam kuchukua mafao yake, baada ya kusikia Serikali imekubali kulipa. Alichambulia huko Hazina pamoja na kulipa nauli ya Moro-Dar-Moro, ni hundi ya Sh.10/=.

Mheshimiwa Spika, hivi kweli tunamwogopa Mungu? Au Serikali hii imesahau kwamba Mungu wa haki yupo?

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya mdundiko wa jana wa Mheshimiwa Mramba ni kweli kama alivyosema umewachukua waliomo na wasiokuwemo. Kwa suala la mafao ya watumishi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977, nathubutu kusema kwamba, Waziri jana ametumia nafasi ya Wabunge wengi kutolielewa vizuri suala hilo, kulidanganya Bunge na wananchi kwa ujumla kwa kupindisha ukweli wa jambo hilo kimakusudi. Maadam Mheshimiwa Waziri wa Fedha amefanya vizuri kwa kuanika taarifa za jambo hilo hadharani, hususani hapa Bungeni, namshukuru kwamba jambo hilo sio siri tena kama ambavyo Serikali imekuwa ikilitaka liwe kwa kulibana kwenye vikwapa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ya Rais Mkapa inaaminika kuwa ya Uwazi na Ukweli, naiomba kama sio kuitaka Serikali, kabla ya kuwasilishwa hapa Bungeni Bajeti ya Wizara ya Fedha, iwe tayari angalau siku nne kabla, imesambaza kwa Wabunge wote nyaraka zote muhimu na haswa taarifa ya Kamati ya pamoja ya majadiliano kati ya Wawakilishi wa Serikali na wadai ya mwaka 2004/2005, vinginevyo Kambi ya Upinzani kwa kushirikiana na Wasamaria wema, wapenda haki tutachapisha taarifa hizo na kuzisambaza popote pale zitakapohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Rais Mkapa kwamba katika jambo hili alifanya uungwana na alionyesha ukomavu wa Kisiasa na wingi wa busara pamoja na kwamba madai haya ameyakuta mwaka 1995. Maneno aliyoyatamka Songea yako wazi na hayana utata. Nanukuu: Alisema:-

“Ndugu wafanyakazi, hadi sasa Kamati ya Pamoja imefikia muafaka kwenye maeneo 12 ya madai. Hatujafikia muafaka kwenye maeneo manne tu, lakini naamini kuwa nayo yatapata muafaka. Kipaumbele changu hivi sasa ni kuhakikisha kuwa tunatenga fedha za kutosha itakapopita Bajeti ya mwaka 2005. Hii kama nilivyosema, tuanze kulipa japo kwa awamu kabla sijaondoka madarakani. Nisingependa mzigo huu nimrithishe Rais ajaye. Narudia, hesabu za awali zinazoendelea kuhakikiwa na kujadiliwa zinaonyesha kuwa deni ni kubwa na linaweza hata kufika Shilingi bilioni 400. Kuzilipa zote hizi kwa mkupuo ni sawa na kusema tusimamishe shughuli nyingine za Serikali. Hivyo nimeagiza kuwa baada ya madai kuhakikiwa na kukubaliwa, Kamati ya Taifa ya Kudhibiti Madeni iandae utaratibu wa malipo na kumshauri Waziri wa Fedha juu utekelezaji wake. Lakini ahadi yangu nakupeni, tutaanza kulipa kabla sijaondoka madarakani ili mradi tuafikiane na wastaafu juu ya viwango na utaratibu wa kulipa tutakaoupendekeza sisi.” Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Maneno aliyoyatamka Waziri wa Fedha hapa Bungeni kwamba ndiyo aliyoyasema Rais, sio ya kweli. Anamlishe Rais maneno yake mwenyewe ili kutaka kula vya watu, kuwadhulumu wazee, wajane na yatima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili, tunaiomba Serikali isilichukulie kama vile inatoa hisani au msaada kwa wadai, ni haki yao wanayostahili kulipwa. Ni mafao yanayotokana na jasho lao. Ni pesa ambayo Serikali ilishapewa tangu mwaka 1987

kuwalipa na pesa hiyo ikaingizwa na Serikali kwenye njia za panya na nyaraka zipo. Tunapotakiwa kulipa vya watu tusiwe na jeuri eti kwa sababu tuna Dola. Tuwe wanyenyekevu, tutumie lugha ya kiungwana ya kuwatia matumaini kama aliyoitumia Mheshimiwa Rais Mkapa na wadai watatuelewa na kutuvumilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtindo huu ambao Serikali imeanza kuutumia kama njia ya kutoroshea haki za Wadai wa “*divide and rule*” tunaomba ufe mara moja. Huu sio Utawala Bora. Mtindo huu mchafu wenye harufu ya udanganyifu na rushwa umelizonga hata tatizo la wadai wa Shirika la Mzinga na sasa unalinyemelea hata suala hili la wastaafu waliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na huenda unatumika hata katika maeneo mengine kudhulumu wastaafu.

Mheshimiwa Spika, hawa maaskari wetu wa Vyeo vya chini wanaopelekwa kwenye Opesheni Dondola na Operesheni nyinginezo kuwasulubu wanyonge wenzao, wana dhiki isiyoelezeka. Mbaya zaidi mfumo wa kinidhamu uliotengenezwa ndani ya vyombo hivi vya Kijeshi na kiusalama ni wa kuwafunga kufuli la Viro mdomoni ili wawe wanaumia kimyakimya. Kula kwao, kulala kwao ni kwa shida. Mafao yao ya uhamisho wa Vituo vya kazi wanayapata kwa ngarambe na wengine kuamriwa kwamba “Tii amri kwanza madai baadaye.” Wito wetu kwa watumishi wa Umma ni kwamba, ungeni mkono Upinzani japo kwa kimya kimya ili Wapinzani tuchukue Serikali ili hali zenu zibadilike. Vinginevyo mtaendelea kuambiwa nyinyi muijenge nchi yenu kwa moyo kumbe wanaowaambia wanaila kwa meno. (*Makofi*)

Nina wasiwasi wakati mwingine baadhi ya Taasisi za kidini ambazo sisi wote ni waumini japo tunatoka Vyama tofauti zikawa zinasukumwa na dhamira ya kutafuta uhimili toka kwa Watawala kwa mambo yashibishayo mwili na nafsi pekee badala ya mambo ya kiroho pia yatakasayo na yaneemeshayo yale ya kumpendeza Mungu na kutufanya wanawake. Kristu na Mtume Mohamed S.A.W mbona hawakubagua? Lakini baadhi ya Taasisi za kidini zimeonyesha upendeleo wa wazi na wala maovu hamyakemei? Maneno matakatifu yanasema: “*Innalillah wa Innalillah Rajiun.*” Tafsiri yake; “Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Hakika tutarejea kwake.” Hakuna kiumbe anatakayedumu milele juu ya ardhi, sote ni wafu watarajiwa. Ya duniani ni ya kupita, sisi kama binadamu tukae chini na kujipanga vizuri bila ajizi, tuangalie tutawale vipi na tugawane kile kilichopo bila kukwaruzana makucha.

Mheshimiwa Spika, katika Awamu ya Tatu, hali ya utulivu, amani na upendo kwa Watanzania imezidi kudorora. Nchi yetu ilikuwa haijawahi kuzalisha Wakimbizi, mwaka 2001 tulijionea wenyewe mauaji. Serikali kuwatesa na kuwadhulumu kwa njia za kijeuri wananchi wa Serengeti pamoja na Tume ya Haki za Binadamu ya Jaji Kisanga ambayo imeundwa na inagharamiwa na kodi zetu zaidi ya billioni mbili, kutoa maamuzi na maelekezo ya kulipwa kwa wananchi hao fidia. Hivi katika hali hiyo Tume ina kazi gazi? Kwa nini isifutiliwe mbali kuliko kuendelea kufanya kazi ya kumpigia mbuzi gitaa? Hivi tunaomwaga sifa kwa “mfalme” wetu mnayajua hayo na mnayaona?

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki tumekuwa na wahaini. Tumeshuhududia mwaka 2000 ubakaji wa masanduku ya kura huko Zanzibar. Sio siri kwamba hivi sasa Muungano wetu umewekwa katika mazingira magumu zaidi kuliko wakati wowote.

Tofauti na huko nyuma watu wameanza kuzungumzia Zanzibar *Nationalism*. Demokrasia ya mtu kuwa na haki ya kuchagua na kuchaguliwa inaanza kupotea.

Aidha, utaambiwa jitoe au wewe hutakiwi kutokana na rangi yako, asili yako au historia yako ya nyuma jambo ambalo lilishaanza kufutika vichwani mwa Watanzania na hasa wale wa kizazi kipyua. Mbaya zaidi ni pale sisi tunaowaongoza watu walioko chini tunaposhindwa kukemea hali hiyo waziwazi na badala yake kuyaona ni ya kawaida na wakati mwingine kuyashabikia.

Mheshimiwa Spika, hili ni bomu tunalolitengeneza na kulikalia sisi wenyewe. Likilipuka, tutateketea sisi wote! Nataka kutoboa siri moja kati ya nyingi nilizonazo kwamba maonevu haya na mizengwe hii ndiyo imekuwa sehemu ya kutengeneza nguvu ya *CUF* huko Zanzibar. Kwa sababu wananchi wengi hivi sasa wanaamini kwamba *CUF* ikichukua Serikali ya Zanzibar itatoa haki sawa ya Wananchi kujiamulia wanayoyapenda. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, Awamu ya Tatu iliingia madarakani kipindi cha kwanza cha uchaguzi uliohusisha mfumo wa Vyama vingi. Hivi sasa ni miaka kumi tangu uchaguzi wa kwanza ufanyike. Tulitegemea kwa nia nzuri kabisa kwamba mfumo huu ungekuwa umeendelea kukomaa. Badala yake kadri siku zinavyokwenda ndivyo njia na mbinu mbalimbali chafu zinaendelea kuandaliwa. Mbaya zaidi ni pale Rais, Amirijeshi Mkuu, anapotamka hadharani kwamba atatumia nguvu zake zote na uwezo wake wote kuhakikisha Upinzani unashindwa. Tamko hili ni hatari na ni kuvunja Katiba ambayo inaruhusu kuwepo Mfumo wa Vyama Vingi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, upo mfano mmojawapo kwamba huko nyuma Zanzibar ililazimishwa kujitua *O.I.C* ikiambiwa inavunja Katiba. Leo hii Tume ya Uchaguzi Zanzibar inavunja Katiba kwa kukiuka muda uliotajwa na Katiba ya Zanzibar Kifungu 27(3) ambacho kinataka Rais wa Zanzibar achaguliwe si chini ya siku 30. Ni wasiwasi wetu kwamba suala hili limewekwa makusudi kuvuruga Uchaguzi wa Zanzibar ili hata CCM ikishindwa, basi wajitokeze mapandikizi wapinge ushindi wa upinzani kwa misingi ya Katiba kuvunjwa.

Tunamwomba Mheshimiwa Rais Mkapa katika kujazia sifa anazoendelea kupewa, aaliangalie na hilo na aanda mazingira yatakayoweza kufanyika uchaguzi ulio huru na haki. Uwezo huo Rais Mkapa anao, labda kama hataki kwa sababu zake binafsi. Inasikitisha kuona Rais ambaye ameapa kuilinda Katiba ya nchi anapokalia Meza ya kuendesha harambee ya kuchangisha mamilioni ya fedha za kwenda kuyashughulikia maeneo yanayoongozwa na Wapinzani. Kwa nini fedha hizi zisipelekwe kwa akinamama wanaougua saratani ya matiti? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kinachotafutwa hapa, usiwe ushindi wa Kimbunga au wa Tsunami lililoua maelfu ya watu huko Asia. Utafutwe ushindi wa haki ambao aliyeshindwa na aliyeshinda watamheshimu. Ushindi wa Kishindo ulioacha maafa mwaka 2001 tulishauona. Sasa huo wa Tsunami si balaa!! (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, tunaomba wananchi walione hili na watuunge mkono tuinusu nchi yetu. Tanzania ni nchi yetu wote, hivi kuna tatizo gani sisi wote bila kujali tofauti zetu za kiitikadi tukakaa na kutafuta mustakabali wa nchi yetu? Kwa nini kusiundwe Serikali ya pamoja? Tanzania chini ya CCM kunashindikana nini? Afrika ya Kusini, Afrika ya Kati, Togo, wamefanya hivyo. Au ni kale kaugonjwa ka uchu wa madaraka?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kuwatamkia Watanzania kwamba, mwezi Oktoba tukipata ridhaa ya wananchi kuiongoza dola, tutaunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Waziri Mkuu inahudumia Bunge, kama mhimili mmojawapo wa kiutawala. Ni vyema chombo hiki kikapewa bajeti ya kutosha ili kifanye kazi yake ya kuisimamia Serikali inavyotakiwa. Kamati za Bunge ziwezeshe vya kutosha sio kuwa omba omba kwa Serikali. Vinginevyo, tutaendelea kupitisha mambo mia kwa mia bila kuelewa kasoro zilizomo kwa hayo tunayoyapitisha.

Mheshimiwa Spika, Wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge, wanafanya kazi katika mazingira magumu ikizingatiwa kwamba wao kwa mujibu wa Sheria ya Huduma ya Bunge hawawezi kuhamishiwa katika Idara nyinginezo. Gari iliyozeeka ambayo imechoka injini hata uifunge magurudumu mapya, hata uitafutie derefa aliyeshinda mbio za magari, haiwezi kuwa na nguvu mpya, kasi mpya, wala kumpa hali mpya mwendeshaji. Tatizo letu kubwa sisi tuliyobahatika kupata nafasi, tumesahau hali halisi ya watu walio wengi huko tunakotoka. Tunapeleka mambo kwa mtindo wa bora lipite, mla ni mla leo, ponda mali kufa kwaja, yajayo yana wenyewe na kadhalika. Tulio na nafasi tunakula kwa niaba ya wasiokuwa nacho.

Mheshimiwa Spika, mbegu ya kuzaa mabaya au mazuri kwa yale yajayo ni ile tunayoipanda sisi leo. Hatua za Wajumbe na wa Kamati ya Makatibu Wakuu upande wa CCM kukwepa Vikao kwa miezi sita sasa Vikao vya Muafaka bila shaka lina jambo. *CUF* pamoja na kudhulumiwa haki zake tangu uchaguzi wa mwaka 1995 imekuwa ikionyesha nia njema ya kuutekeleza muafaka. Pingamizi linakuwepo kwa Serikali ya umoja wa Kitaifa, lipo kwa CCM. *CUF* ilisharidhia kupitia Vikao vyao vya kila ngazi. Vurugu za Bagamoyo kuzihusisha na mambo ya muafaka tunaelewa fika kwamba hiyo ni janja ile ile ya fisi kumsingizia sungura eti anachafua maji ili amfanye kitoweo.

Mheshimiwa Spika, Waswahili wana usemi usemao, zege halilali. Kupitia Bunge hili, Serikali ya Rais Mkapa, iwatamkie umma Watanzania na dunia kwa ujumla kwamba muafaka basi ili wananchi wawaelewe.

Mheshimiwa Spika, namalizia maoni yetu ya Kambi ya Upinzani kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kuliendesha Bunge hili la Vyama Vingi kwa busara, umakini na uvumilivu wa hali ya juu. Aidha, mimi binafsi kama Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ndani ya Bunge, nashukuru msaada wa mara kwa mara ambao nimekuwa nikipewa kuendesha na kusimamia shughuli za Upinzani.

Nashukuru ushirikiano nilioupata toka kwa Wabunge wote wa Upinzani licha ya kutoka Vyama tofauti na misimamo tofauti. Mara nyingi nimekuwa nikijiuliza kwamba ni miujiza gani inaniwezesha kusimamia shughuli za Wabunge wanaotoka Vyama tofauti vya Kisiasa tena kwa masikilizano ya hali ya juu wakati wapo wanaoshindwa kusimamia shughuli za ndani ya Chama kimoja? Bila shaka ni msaada wa Mwenyezi Mungu na dhamira sahihi na thabiti ya wale ninaowaongoza. Aidha, nawashukuru Viongozi wote wa Vyama vya Upinzani kwa kukubali wito wa kuja kutosikiliza na kujadiliana nao kama Kambi ya Upinzani Bungeni kila tulipowaomba kukutana nao. Namshukuru Waziri Mkuu Mhe. Frederick Sumaye kwa msaada wake wa mawazo ambayo amekuwa akinipa mara kwa mara kila nilipomwendea.

Shukrani kwa Wabunge wote wa Bunge hili na Watumishi wote kwa ujumla na hususani Katibu Muhtasi wangu Bi. Salvina Mahundu kwa ushirikiano na msaada mlionipa. Tuombeana tukutane tena hapa Dodoma mwezi Novemba 2005. *(Makofi)*

Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11 jioni.

(Saa 07.00 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 Jioni Bunge lilirudia)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

MHE. MARIA D. WATONDOHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niwe mchangiaji wa kwanza katika hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Niungane na wenzangu kutoa pole zangu za dhiti kwa wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kupotelewa na Ndugu yetu Mpendwa, Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga. Naomba Mwenyezi Mungu afariji pia familia yake na ailaze roho Marehemu mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, anayetarajia kumaliza muda wake kwa kazi nzuri ya kuongoza nchi yetu. Katika kipindi chake cha miaka kumi, amekuwa nahodha hodari, ameiongoza nchi yetu katika njia sahihi hata uchumi wetu umekua na ametujengea heshima ndani na nje ya Tanzania. Ndio maana ameweza kuwa Mwenyekiti mwenza wa Tume ya Utandawazi na ameweza kuteuliwa kuwa Kamishina wa Africa *Commission* na Bwana Blair.

Haya yote ni kwa sababu CCM hutoa Viongozi makini, imara, wanaojua nini cha kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, mtu anaposimama na kubeza mafanikio ya Serikali ya CCM kwa kweli unajua kabisa kwamba huyu amechanganyikiwa na haelewi anachokizungumza. Mwenyezi Mungu ambao wote

tunamwamini ni Mungu wa upendo, Mungu anayependa amani, Mungu asiyependa mifarakano wala uchochezi. Sasa Vyama vya wenzetu ambao wanamzungumzia Mwenyezi Mungu kwamba CCM imuogope lakini wakati huo huo katika hotuba zao wanachochea kufanya vurugu, sijui ni Mungu gani wanayemzungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna dini yoyote ulimwenguni inayozungumza juu ya uchochezi. Wanapobeza na kusema wanajiandaa kuchukua utawala, ni sawa sawa na hadithi ya fisi anayemfuata binadamu nyuma anasema mikono ile itadondoka sasa hivi, mate yanamdondoka, mikono ya binadamu haidondoki yumo anamezea mate tu. Kwa hiyo hizo ni ndoto za Alinacha. *(Kicheko/Makofi)*

Natoa wito kwa wananchi wa Tanzania kuangalia mafanikio ya Serikali ya CCM na waone kwamba nchi yetu bado inahitaji nguvu ya Chama imara, chenye sera nzuri ili kutuvusha katika karne hii ya 21, wasidanganywe wala kuyumbishwa na ndoto ambazo hazieleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kupongeza Askari wa Miavuli wa Serikali ya Rais Mkapa, kwa kazi ambayo wameifanya. Mafanikio yote ambayo yameelezwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu leo, yametokana na umoja na mshikamano wa Askari hawa wa Miavuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, ninaomba nitoe ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhai wa Taifa na maendeleo ya kiuchumi yanaweza kupatikana tukiwa na barabara za uhakika maana uchumi wetu unategemea sana kilimo na kilimo kinafanyika Vijijini. Naipongeza Serikali ya CCM kwa sababu katika mpango wake wa ishirini na tano barabara nyingi Tanzania zitafunguka, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundo Mbinu na tumeona barabara nyingi sasa hivi zina wakandarasi na wanaendelea na kazi nzuri. Napongeza vilevile kwa sababu mikataba ambayo inasainiwa sasa kati ya Serikali na wakandarasi ni Mikataba makini. Lakini naomba kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, makandarasi hawa tunaowateua Serikali iwachuje kwa makini. Tumekuta mkandarasi ambaye sehemu nyingine amefanya kazi ambayo sio nzuri ilikuwa na *lifespan* ya miaka 10, lakini imeharibika chini ya miaka mitano. Sasa huyu mkandarasi huyu kazi nyingine pamoja na kwamba kiwango cha kazi aliyofanya kule ilikuwa sio nzuri.

Kwa hiyo, nashauri Serikali ichuje wakandarasi kwa makini sana. Makandarasi wengine wanaposikia kuna mkubwa anakuja kutembelea, basi wanahamishia vifaa vyote pale, lakini mkubwa akiondoka vifaa havipo, mnarudi pale pale mnaona magari mawili, trekta moja na shindilia moja. Kwa hiyo kazi haziendi vizuri. Tunaomba tuwachuje kwa makini makandarasi hawa ili kazi iweze kufanyika vizuri.

Pili, tuhakikishe makandarasi wawe na vifaa vya kutosha na viwe vifaa vya kisasa. Kamati yetu ilipotembelea katika baadhi ya maeneo tumekuta mkandarasi ana vifaa lakini karibu vyote ni vibovu. Ni kweli atafanya kazi, lakini kazi yake inaweza ikachelewa sana. Sasa tunapompa kazi mkandarasi mwenye vifaa vibovu, maana yake hata kazi ambayo unaweza kuizalisha pale ni mbaya. Naomba na hilo tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, kwa kuwa Serikali sasa imepania kuhakikisha kwamba barabara kuu za Taifa zinapitika kwa lami, zinajengwa kwa kiwango cha lami, basi Serikali itupe macho yake kwenye barabara za Mikoa. Naipongeza Serikali kwa kuanzisha *Road Fund*.

Lakini *Road Fund* barabara zinazogawiwa katika Mikoa huwa kidogo na sehemu nyingine barabara zinatengenezwa kwa kiwango cha udongo wala sio changarawe. Kwa hiyo, utakuta barabara kwa mfano inayotoka Nanganga, kwenda Rwanga mpaka Mandawa, Lindi huko au kutoka Ngongo kwenda Milola mpaka Mandawa Lindi huko au kutoka Ngongo kwenda Milola mpaka Mandawa unapotoa fedha kwa kutengeneza Kilometa tano, tano mpaka uje umalize kilometa 45, huku nyuma kumeshaharibika.

Kwa hiyo, inaonekana kana kwamba barabara haijatengenezwa lakini fedha zinatolewa. Kwa hiyo, mimi ningeshauri Serikali tuwe makini sasa tuhakikishe kwamba barabara kama hatuwezi kujenga kwa kiwango cha lami, basi zijengwe kwa kiwango cha changarawe imara ili tufunge njia za kwenda Vijijini ambako wako wananchi ambao wanajishughulisha na wazalishaji wa mazao mbalimbali. Hizi barabara nilizositaja ni maeneo ambayo ni wazalishaji wakubwa wa chakula, ndio wanaolisha Miji ya Lindi na Mtwara. Lakini barabara unakuta hazipitiki vizuri kwa kiwango kinachotakiwa ingawaje naipongeza sana Serikali kwamba barabara toka Ngongwe kuelekea Milola inatengenezwa, bado inahitaji kutengenezwa kwa kiwango cha changarawe badala ya udongo, kwa sababu kadri unavyotengeneza eneo hili la Pwani, huku nyuma kunaharibika, mbele unatengeneza, inakuwa kama hatujafanya kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia kuhusu barabara ya Dar es Salaam hadi Kibiti, nafahamu kuelekea kule wakandarasi wamepatikana isipokuwa kutoka pale tulipoishia lami ya darajani kufika Somanga, lakini hii Dar es Salaam kwenda Kibiti si parefu sana, lakini ujenzi wake unasusua mno. Kwa hali hii, tunaweza kufikia miaka thelathini hatujafika Kibiti na lengo la Serikali ni kwamba twende na *taxi* kutoka Mwanza mpaka Mtwara ifikapo mwaka 2007. (*Makofi*)

Sasa tutafikaje kama eneo hili toka Kibiti mpaka Dar es Salaam hatujafika? Maana sasa wako Mkiu pale hatujafika kokote karibu na Kibiti, na kwa mwendo wanaokwenda hatutaweza tukafika haraka. Ninaishauri Serikali *i-pull up socks* ili tuweze kwenda na wakati kukutana na mwaka 2007, ili katika mwaka huu wa 2005/2006 toka Mkiu mpaka Kibiti pawe pamekamilika. Kama hapakamiliki, basi hebu watuondolee mashimo ya lami yale, maana mashimo ya lami yanaharibu magari mno. Mtuondolee mashimo ya lami ili tuwe na barabara ya changarawe tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ningependa kuchangia ni suala la elimu, elimu wote tunafahamu ni ufunguo wa maisha na Taifa lolote ambalo wananchi wake hawana elimu hawawezi kuendelea. Kwa hiyo, nina ushauri ufuatao katika suala la elimu. Ninapongeza hatua za MEM na MMES.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jana wakati najibiwa swali la Na.65 Serikali ilisema kwamba walimu waliojiendeleza kutoka madaraja mbalimbali wamepandishwa vyeo na kurekebishiwa mishahara. Ninao ushahidi kwamba sio walimu wote wamepandishiwa vyeo na kurekebishiwa mishahara. Lakini mandhali Serikali imetoa kauli yake, basi natoa wito, wale wote ambao hawajapandishwa vyeo baada ya kujiendeleza, wapandishwe vyeo na warekebishiwe mishahara maana Serikali ilishatamka jana hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ningependa kutoa ushauri ni suala la michepuo ya Shule za Sekondari. Serikali inataka kufuta michepuo. Michepuo iliandaliwa ili kuandaa wanafunzi watoke pale waende wakajitegemee badala ya kuandaa *for white collar jobs*. Hii misingi iliwekwa na Baba wa Taifa kwa nia maalum ya kuandaa wanafunzi. Ninaishauri Serikali tusifute michepuo toka Sekondari *O-level* mpaka *A-level*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, Serikali ilitangaza mwaka jana 2004 kwamba sasa wanaomaliza Kidato cha Sita watamaliza na wakifaulu watajiunga moja kwa moja na Chuo Kikuu.

Lakini kwa masikitiko, vijana waliomaliza Kidato cha Sita mwaka huu, wanaambiwa hakuna *sponsorship* ya Serikali. Sasa vijana hawa waende wapi? Vijana hawa ni watoto wa wakulima na wafanyakazi ambao hawana uwezo wa kuwalipia, baadhi yao kama walishindwa kulipa hata ada ya Sekondari, hivyo watalipa ada ya Chuo Kikuu.

Naomba Serikali ilianganalie hili maana Bunge lako Tukufu limepitisha Mfuko wa Elimu ambao unawakopesha vijana, leo itasemaje Serikali haiwezi kuwa-*sponsor* vijana waliomaliza *Form Six* na kwamba wanachukua wa mwaka uliopita tu. Naomba Serikali ilianganalie hili na itoe tamko rasmi kabla ya Bunge lako Tukufu kuhairishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia linahusu nafasi za wanawake. Niishukuru Serikali na kuipongeza kwa msimamo wao wa kutaka kuongeza nafasi za wanawake wa Viti Maalum hadi kufikia asilimia 30 ya Wabunge wote. Maelezo hayo yako kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa katiba tulivyoirekebisha, asilimia thelathini wanawake itatokana na Wabunge wa Majimbo ambayo ni Majimbo 232, Wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi watano, Mwanasheria Mkuu mmoja, Wateuliwa wa Rais kumi ambao ni 248.

Kwa hiyo, Wabunge wa Viti Maalum wa asilimia 30 ya 248 itakuja Wabunge 75, lakini Wabunge wote kwa jumla ya Viti vyao ni 323 ukichukua na hao pamoja na hiyo na

asilimia 75 ili tupate asilimia 30 ya Viti hivi, kweli Wabunge wanawake wanatakiwa wafikie 96 na sio 75. Ninaomba Serikali iangalie hii itilafu kwenye katiba, tunatoa wapi? Ninaomba sana muiangalie hiyo, maana tukichukua asilimia 75 ni wale niliowaorodhesha tu wa Majimbo, wa Baraza la Wakilishi, Mwanasheria Mkuu na Wateuliwa. Sasa ukichukua asilimia 30 ile ukipata wote inatakiwa tufikie 323, kwa hiyo asilimia 30 iwe ya 323 na sio ya 248. Ninaomba Serikali ilianguale hili ili tupate ufafanuzi katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la ardhi. Naipongeza Serikali kwa kazi yake nzuri, lakini kwenye suala la ardhi wananchi wanalipa kodi ya viwanja mwaka hadi mwaka, lakini vilevile kuna kitu kinaitwa *property Tax* ambayo inatofautiana katika kila Halmashauri. Serikali haioni kwamba inawalipisha wananchi mara mbili kwa ardhi hiyo hiyo? Serikali haioni kwamba tunawabebesha mzigo wananchi hawa? Ni sawa sawa na kusema anayelima analipia shamba halafu alipie mazao, ni haki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii, nami nichangie katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini awali ya yote kabla sijasahau, naomba niseme kwamba naiunga mkono asilimia mia moja kwa mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokawaida na mimi naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa msiba uliotokea ambaye alikuwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mungu Mwenyezi ailaze mahali pema Peponi roho ya Mbunge mwenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi nimesikiliza hotuba ya Kiongozi wa Upinzani, ametumia maneno mengi lakini kuna neno ambalo limeandikwa mle ndani linasema: “Jambo usilolijua ni sawa na usiku wa giza.” Mimi nakubaliana naye kabisa kwamba kwa sababu yanayozungumzwa humu ndani kumbe yeye hayaelewi zaidi, kwa hiyo ndani ya miaka mitano aliyokaa Bungeni, sasa sijui tumpeleke wapi kwa sababu haelewi hata kinachozungumzwa humu ndani. (*Makofi*)

Namshangaa kama Kiongozi wa Upinzani na yeye ndiyo anayeongoza Wapinzani, ukichukua hotuba ya Waziri Mkuu ya leo imelezea mikakati, taratibu tangu mwaka 1995 mpaka mwaka 2005. Imesheheni kila kitu! Sasa binadamu huyu ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati hii anasema haelewi kinachoendelea, nawapa pole sana wananchi wake wa Jimbo la Bukoba Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anazungumzia eti tukikamata madaraka mwezi Novemba; hivi madaraka unayakamata vipi? Kwa vigezo vipi? CCM ina vigezo! Tunavyo! Naomba nivitaje vigezo vidogo tu. Ukienda kwenye matokeo ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, CCM ilizoa Viti 49,967, CUF Viti 2,000, Wenyeviti wa Vijiji CCM Viti 9,452, CUF 292, Wajumbe wa Halmashauri za vijiji CCM 1,583, CUF viti 6,000 na kadhalika. Sasa wanasema tutakapochukua madaraka, unachukua madaraka juu au

unachukua madaraka chini? Lazima uanzie chini! Nawapa pole, lakini ni vizuri wakaenda kwa wananchi kwanza ili kusudi waone jinsi gani Chama cha Mapinduzi kinavyoweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie hotuba hii. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri aliyofanya ndani ya miaka kumi. Mafanikio nafikiri Ndugu zangu tumeyaona. Lakini haya mafanikio naomba tujipongeze na sisi Waheshimiwa Wabunge, Mawaziri, miundombinu jinsi ilivyoboreka. Kwa kweli Chama cha Mapinduzi kinastahili sifa kubwa sana kwa kazi nzuri iliyofanywa na nina uhakika hata ushindi wa Novemba wa Octoba Mwaka huu utakuwa wa kishindo kikubwa kweli kweli.

Mheshimiwa mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Huduma za Jamii, lakini nizungumzie Shule. Kuhusu elimu, naomba niwapongeze sana wananchi wa Wilaya yetu ya Kwimba kwa kazi nzuri waliyofanya ya kujenga Shule za Sekondari karibu kila Kata. Tunaipongeza sana Serikali. Kwa mwaka huu peke yake tumefungua Shule za Sekondari 13. Jimbo langu la Sumve Sekondari saba, Jimbo la Kwimba kwa Mheshimiwa Sakila Shule sita, jumla Shule 13.

Lakini bado tunategemea mwakani tutafungua tena Shule tano ili kukamilisha kila Kata iwe na Shule ya Sekondari. Tunaishukuru sana Serikali, lakini tunawashukuru wananchi wa Wilaya ya Kwimba kwa kweli kwa kujitolea kuhusu suala zima la elimu. Naiomba Serikali, kuwa lipo tatizo la walimu, tunaomba sana wanafunzi hao wanaposhinda sasa tunaomba tupatiwe walimu wa kutosha ili kusudi waendane na utaratibu na masomo jinsi yatakavyokuwa yamepangwa. Hili nafikiri ni la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la pili, naomba niulize Serikali, Rais alisafiri katika ziara zake, alikwenda Vietnam. Alipokuwa kule, alizungumzia suala la pamba kwamba pamba sasa badala ya kupita kwa watu wa kati itakuwa inauzwa inapelekwa moja kwa moja Vietnam. Sasa hivi ni kimya, hakuna kinachoendelea mpaka wananchi wa Kanda ya Ziwa hasa Wilaya ya Kwimba kwa maana ya Sumve na Kwimba, si muda mrefu mwezi huu wataanza kuuza pamba yao. Lakini tunasikia bei ya pamba kwa kilo ni Sh.170/= kwa kilo moja, hivi kuna tatizo gani? Kwa mfano mwaka 2003, bei ya pamba ilikuwa ni Sh.250/= mpaka Sh.350/=, mwaka 2004. Bei ya pamba ilikuwa ni Sh.275/= mpaka Sh.300/=.

Lakini mwaka huu tunaambiwa bei ya pamba itakuwa Sh.170/= mpaka Sh.200/= . Juzi juzi nilikuwa najaribu kuzungumza na wataalam wakaniambia kwa bei ya Soko la Dunia la kilo moja ya pamba nyuzi ni *pound senti 45*. *Pound senti 45* ni sawa na Dola senti 99. Ukizidisha kwa *rate* ya sasa ni kama Sh. 1,089/= kwa kilo. Ili upate pamba nyuzi, unatakiwa uchukue kilo tatu za pamba, kwa maana hiyo utakuwa umepata pamba nyuzi kilo moja na mbegu kilo mbili. Ukigawa kwa tatu katika Sh.1,089/= utakuta kwamba unapata Sh. 363/= kwa kilo moja.

Hivi wenzetu mnaotafuta masoko, nalo hilo ni tatizo, kwa nini wananchi hawa wanaolima pamba siku zote tu ni watu wa kunyonywa hivi? Hakuna namna ya kuja

kutafuta masoko? Mheshimiwa Rais alisema kwamba jamani sasa mtakuwa mnapeleka pamba na hii aliandikwa kwenye gazeti, sikumbuki ilikuwa lini, lakini iliandikwa kwenye gazeti katika ziara yake mpeleke pamba kutoka Dar es Salaam kwenda Vietnam moja kwa moja usipitie katikati hapa kwa sababu mkipitia katikati hapa watu ni wengi gharama zinakuwa kubwa.

Sasa mpaka leo pamba wanauza, kesho kutwa watauza Sh.170/= na Sh.200/= . Hivi tukiita huu ni unyonyaji, tutakuwa tumekosea? Naiomba sana Serikali itoe majibu ya suala la ziara ya Mheshimiwa Rais, kwa nini mpaka leo Wizara inayohusika na Masoko hasa kuhusu zao la pamba wananchi wangu wa Jimbo la Sumve na Jimbo la Kwimba kwa Mheshimiwa Sakila, ni wakulima wanzuri wa pamba.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, matunda, mafanikio ya wananchi kuondoa umasikini utaondoka kwa kulima pamba, mifugo kwa Wilaya ya Kwimba na Jimbo la Sumve na Kwimba. Sasa kama hii pamba yao wataendelea kuiuza kwa Sh. 170/= tunawatakia mema? Umaskini utawaondoka lini wananchi hawa wa wilaya ya Kwimba na Kanda nzima ya Ziwa? Naoimba sana Serikali itazame hili kwa makini. Kama wenzetu wanauza kilo moja *pound cents 45*, sisi tunashindwa, kweli kufuatilia na kama hatuwezi kufuatilia hata agizo la Rais, basi kuna mapungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba sana hili litazamwe kwa makini zaidi ili kusudi wananchi wetu waweze kufaidi matunda yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kilimo kwa ujumla. Katika bajeti ya Waziri Kigoda, alisema kwamba kilimo asilimia 48.8 kinalipatia nchi yetu pato la Taifa, kilimo asilimia 66 hutoa fedha za kigeni, kilimo asilimia 70 hutoa ajira kwa Watanzania.

Sasa bado tunajiuliza, hivi kilimo chetu sisi Watanzania tumekiwekeza namna gani? Tumewekeza namna gani? Kwa sababu hakuna mahali ambapo tumewekeza, tunasema tu kwamba kilimo ni uti wa mgongo, lakini je tumewekeza kama hiki kilimo kinatoa asilimia 70 kama ni kweli na mimi najua ni kweli kwa sababu Watanzania wengi ni wakulima kinatoa asilimia 70 kwa ajira.

Hivi tumeweka mazingira gani ya kuhakikisha kwamba kilimo hiki sasa ni kilimo sio cha kizamani, ni cha kisasa? Tumeweka mazingira gani? Tumewekezaje? Lakini sio hilo tu, wananchi wetu wengi leo ukienda nchi nyingine wanapewa Semina, wanafundishwa, lakini sisi hakuna hata siku moja mkulima kupelekwa hata Semina, hakuna. Naomba sana tubadilike ili wananchi wetu nao waendane na wakati, lazima wananchi wetu wapewe Semina lakini tuwekeze. Serikali iwekeze katika suala zima la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie umeme ambao muda mwingi nimekuwa nikuzungumzia humu Bungeni. Yapo maeneo ya Sumve, Malya, Mvomero

kwa maana ya Mgeta nguzo zimeshasimikwa, upande wa Sumve, Malya nguzo ziko chini, Mgeta nguzo zimesimamishwa. Sasa naomba Serikali kupitia *TANESCO* ikamilishe zoezi la kutandaza nyaya na kuwasha umeme katika maeneo hayo, ikiwezekana mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nizungumzie Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Nashukuru sana kuwa Serikali imesema imeshaanza utaratibu kuhakikisha kwamba inaujenga, basi naomba jitihada hizo ziendelee, zisiishie njiani kwa sababu ule uwanja una manufaa makubwa kweli.

Mheshimiwa Spika, lakini pili nizungumzie simu za mkononi, Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi hili nimekuwa nikikwambia mara kwa mara, naomba sasa ulichukue kwa mara nyingine ya pili kwa sababu katika Bajeti ya mwaka jana ulisema. Nakujua wewe ni msikivu mzuri tu na unafuatilia, kama mengine unaweza kuyasimamia na yakatekelezwa sasa hili la simu za mkononi. Nilisema safari hii kwamba wananchi wangu wanasimama kwenye vichuguu, wanasimama kwenye miti, mkawa mnacheka humu ndani. Lakini mpaka leo wananchi wangu bado wanasimama kwenye vichuguu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri waambie hawa watu wa *Vodacom*, *Celtel* na *Buzz* wasimamie au waharakishe ufanikishaji wa kuweka hii mitandao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine suala la Shirika la Reli Tanzania, tunaambiwa kwamba litabinafsishwa baada ya miezi sita. Naomba Shirika hili Serikali iwe makini kidogo kwa sababu endapo tutabinafsisha bila kuangalia maslahi ya nchi basi baadaye tutakuja kupata matatizo kwa sababu ukichukua gari la abiria linalotoka Dar es Salaam kwenda Mwanza wale abiria wanaopanda kule ndani ni wengi kweli kweli. Sasa endapo ubinafsishaji hautakuwa makini basi tutakuwa tumewapa adhabu wananchi wanaotumia reli ya kati. Lakini vile vile kuna mizigo ya Serikali kama huyu mnunuzi atakuja na malengo yake bila kutupa masharti basi tutajikuta mbolea itakuwa haiendi na kile chakula cha njaa kitakuwa hakiendi kwa hiyo, naomba tuwe makini katika ubinafsishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimaliezie kwa kusema kwamba hotuba hii ni nzuri na sasa sisi Waheshimiwa Wabunge tunakwenda Majimboni tutakiane kila la kheri, twende tukachape kazi kwa kipindi kilichobaki, kwenye kura za maoni Mungu atujalie tupite wote turudi. Lakini vile vile katika Uchaguzi Mkuu ujao Chama cha Mapinduzi kiibuke kidedea ili tuje tuendeshe Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo mafupi niseme tena kwamba naunga mkono hoja asiliamia mia kwa mia. Ahsanteni. (*Makofi*)

MHE. THOMAS S. NYIMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja muhimu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza nitoe rambirambi kwa Marehemu Mbunge mwenzetu Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, natoa pole kwa familia na wananchi wa Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Amani Abeid

Karume. Hawa ni wateule wa Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi kukimbiza Bendera ya Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi unaofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiyumkiniki watapita kwa kura nyingi kwa sababu vigezo vyote vinaonyesha hivyo. Nina uhakika wanapingana na watu ambao wamekwishagombea zaidi ya mara mbili na kukataliwa na wananchi hao hao. Kwa hiyo, hawana sifa mpya ni wale wale na haiyumkiniki wananchi wanajua mapungufu mengi walionayo ambayo yanajitokeza katika utendaji wao wa kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia hotuba yako nzuri napenda niwapongeze Mawaziri wako wa Mipango na Fedha, wametoa hotuba nzuri kabla yako, Bajeti imepita kwa kura nyingi. Imepita kwa kura nyingi kwa sababu ni Bajeti iliyolenga kutoa utumishi uliotukuka kwa Watanzania kwa miaka mitano kwa mwaka ujao 2005/2006. Lakini kila Bajeti huonyesha mwelekeo wa Serikali katika utekelezaji wa maendeleo ya wananchi ndivyo Bajeti hii ilivyokuwa. Ndio maana nawapongeza sana na kwa pekee nampongeza ndugu yangu Mheshimiwa Basil Mramba, siyo tu kwa Bajeti nzuri, ila kwa uwezo wake wa kujaribu kushawishi watu waelewe na waweze kuamini ambayo kwao yeye anatenda, hongera sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu naiunga mkono hotuba yako mia kwa mia. *(Makofi)*

Kwa mantinki hiyo natumia nafasi hii kukupongeza sana kwa utumishi wako wa miaka 10. Umeweka *record* ya kwanza, kwa kumbukumbu zangu ni kwa mara ya kwanza mtu mmoja, Mtanzania mwenzetu hodari, amepewa nafasi hiyo mfululizo kwa miaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kama ilivyo ada wengi hupenda kutizama yale tu ambayo pengine kama binadamu ulipungukiwa. Lakini mengi mazuri, mengi yaliyotukuka kiutendaji haiyumkiniki CCM tukasema miaka 10 tumefanya kazi nzuri kama kwa kusema hivyo sisi pamoja na wewe Waziri Mkuu. Nakupongeza sana, nakutakia maisha marefu yaliyobaki na nakutakia uweze kuwa mshauri mzuri kwao wote watakaofuata. Ahsante sana. *(Makofi)*

Kwa pekee pia hili likiwa ni Bunge la mwisho kwa kipindi hiki napenda nimpongeze Mheshimiwa Spika, kwa kumpongeza yeye nawapongeza watendaji wa Bunge wote, kwa pekee nampongeza Ndugu yangu Damian Foka, ambaye karibuni tu ameteuliwa kujiunga na Utumishi wa Bunge hili kwa nafasi ya utendaji wa juu kabisa, Katibu wa Bunge. *(Makofi)*

Ni nafasi wengi hawaielewi, lakini ni nafasi nyeti na ni nafasi yenye heshima maana unatumikia chombo cha umma, chombo cha watu, chombo kinacholinda na kutetea maslahi ya Watanzania. Nampongeza Mheshimiwa Spika, kupitia yeye na *Commission* ya Bunge ambayo haiyumkiniki imefanya kazi nyingi kadhaa zinaonekana, kadhaa ziko kwenye mipango kwa ajili ya maendeleo ya Bunge hili kwa miaka mingi ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawajibika na ni wajibu wangu nisiendeleo kabla ya kumpongeza Mtukufu Rais wetu Benjamin William Mkapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika yote tunayoyaongea ni kwa maongozi yake, ni kwa jitihada zake amefanya kazi kubwa, amefanya kazi ambayo imetuletea heshima ndani na nje ya nchi. Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, naye namtakia maisha marefu, namwomba aendeleo kuwa mshauri mzuri kwao wote watakaopokea nafasi mbalimbali za kuongoza nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu mwaka 1992 tuliruhusu Katiba Vyama vingi vya Siasa, inasikitisha sana kwamba tangu mwaka 1992 mpaka leo hatujafanikiwa kupata vyama vya upinzani kwa mantiki ya upinzani wa kidemokrasia. Tumepata vyama ambavyo kwa sehemu kubwa vinakidhi kweli kweli kwamba hata siku moja hawafanyi jitihada kuelewa nafasi ya upinzani ipi, nafasi ya Serikali, Chama Tawala ni ipi na kukosoa yale ambayo Chama Tawala kwa sababu moja au nyingine hatukufanya vizuri. Hawa watu hawakusaidia lolote kabisa na mara nyingi wamekuwa ni kikwazo, wamekuwa wakichanganya mpaka watu wanashindwa kuelewa wanaongea nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mimi nimesikitika sana kuona wanasema, nimesoma gazeti moja haya magazeti nayo Waziri Mkuu una sehemu unafanya jitihada kuongea nao, lakini mimi nina mashaka hapo utaumia tu, kwa sababu kuongea na akili butu haisaidii chochote kile. Kuna vyuma vya aina ambavyo unaweza kutengeneza kisu ukanoa kikakata, lakini kuna aina ya chuma kama *cast iron*, ukitengeneza kisu hata unoe namna gani hakiwezi kukata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana chuma hicho siyo kwa ajili ya kuwa kisu, ni kwa ajili ya kazi nyingine. Sasa leo nimesoma gazeti la Rai, linasema Bajeti hii haisaidii maskini, *it is murmuring around*. Mimi nilitarajia *a responsible person* ataniambia Bajeti hii haisaidii maskini kwa sababu imezingatia moja, mbili, tatu, ilitakiwa izingatie moja, mbili, tatu. Huwezi kuona hilo, utakaloona ni mazungumzo kama ya watu wako kilabuni, hadithi za kilabuni mara nyingi zinakuwa hazina kumbukumbu wala hazitakiwi kukumbuka, mara mkishamaliza mazungumzo pale mmelewa basi mazungumzo ya siku ile yamekwisha asubuhi yake mnahitaji mapya. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi nikushauri tu Mheshimiwa Waziri Mkuu, hotuba yako inaonyesha utafanya bidii kuzungumza na hawa. Lakini labda wazaliwe, wengine hawa waliopo unapoteza muda wako bure. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kueleza jambo moja ambalo Waheshimiwa Wabunge pengine wengi mmesikia. Waandishi wa habari hawa hawa anaotaka kuongea nao Waziri Mkuu sijui ataanza, wametangaza karibu wiki mbili ni moja au mbili mfululizo kuwa eti mimi natafutwa na polisi, eti mimi nimekamatwa na polisi, eti mimi nimejisalimisha polisi. Kitu ambacho yumkini hakijatokea, wala haijapata kutokea, hizo habari na mimi nimekuwa nikisikia kwenye radio, magazeti kama wengine mlivyosikia *very irresponsible journalists*. Kama Sheria inatungwa mimi nilikuwa naomba Waziri Mkuu wanaotunga Sheria ni kweli wako waandishi wa habari wachache

wakomavu wenye upeo, wenye elimu kama hatutawashughulikia hawa kwa ajili ya wengi ambao ni butu kabisa itakuwa hatuwatendei haki.

Lakini ni vizuri *a responsible journalism* iwe na adhabu kali ya mara moja, isiwe hizi adhabu za kuwapeleka Mahakamani, kesi inaendelea miaka miwili, mitatu, nafikiri haitasaidia nchi yetu. Watu waliopo hivi sasa katika makundi kadhaa ya waandishi wa habari ni watu wa mitaani tu, ni watu ambao mtu yeyote yule anaweza kuwalipa fedha leo umtukane fulani basi kesho akaandika matusi anatumka mtu. *Journalism* ya namna hiyo nchi ikiivumilia yumkini nchi yetu itakuwa mahali ambapo hapana heshima, hapana utu, hapana amani, hapana mwelekeo wa kimaendeleo wa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naipongeza Serikali kwa pamoja, Mawaziri kila mmoja nampongeza kwa jitihada zake alizofanya kwa miaka mitano katika eneo lake alilogaiwa la kufanya kazi. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Lakini Waheshimiwa Wabunge niwapongeze sana kwa pamoja kama sehemu ya dola tumeshirikiana na Serikali yetu vizuri, tumeonya pa kuonya, tumeelekeza pa kuelekeza ndio maana nchi yetu imeondoka ilipokuwa. Tuliipokea nchi hii Waheshimiwa Wabunge mwaka 1995 awamu ya tatu ikiwa ina makusanyo ya shilingi bilioni isiyozidi 27. Leo tunamaliza tuna makusanyo yasiyopungua bilioni mia moja arobaini na tano *plus*. (*Makofi*)

Sasa hawa wapinzani yumkini wangepitia shule hizi ni *simple arithmetic*, siyo hesabu zinahitaji *professor* wa mahesabu, hapana, ni kujua tu kwamba 145 na 25 ni karibu mara sita au zaidi. Sasa mtu aliyefanya hayo yote ukisema hajafanya chochote inaeleke wao wanavyoelewa Serikali ina wajibu wa kupita nyumba kwa nyumba na hilo ndio ninalowaonya Watanzania wazingatie hawa wapinzani wanaoongelea vitu vya Alinacha, vitu vya hadithi za kusadikika kama kitabu cha Shaaban Robert. Hakika wakiwapa madaraka hata ya Udiwani tu wamepoteza nafasi ya maendeleo yao, ni watu ambao inatakiwa wakae, wajifunze, ndipo watakapopata uelewa waweze kupewa angalau nafasi ya Udiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa pekee Watanzania, nawapongeza Tanzania nzima ukitizama matokeo ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa mtu mnayeshindana *percent 93.6* yeye anapata *percent 2.6* kama haachi hiyo shughuli huyo ni mtu wa ajabu sana. Ni mtu ambaye haelewi analofanya na inawezekana nia yake siyo kuongoza nchi ila ni kuishi kwa njia ya kusema yeye ni kiongozi wa chama. Mara nyingi sana tunapata tatizo kwa sababu malengo ya Wapinzani siyo kuongoza wananchi, ila ni kutafuta ajira baada ya kukosa ajira. Kama Vyama vya Upinzani vitafanya kazi kama ajira mbadala basi nia na madhumuni ya Katiba ya Tanzania ya vyama vingi inashindwa kutekelezeka na pengine tutafika mahali tujifunze upya tufanye nini ili nchi yetu iwe ina-*safety balances* ambazo zina maana kwa maendeleo ya wananchi.

Leo kwa mara nyingine tunashuhudia ndani ya Bunge hili mtu anasema hatujafikisha maendeleo na Bajeti hii kwa wananchi, kuna njia zaidi ya elimu ya kuondoa umaskini? Nje ya elimu huwezi kuondoa umaskini. Kuna njia zaidi ya barabara vijijini na

kila mahali ya kuondoa umaskini kwa wananchi barabara, ni *noble system*, ni mishipa ya damu ya binadamu kwa uhai wake, ndio mishipa ya uchumi kwa nchi yoyote inayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti yako Mheshimiwa Waziri Mkuu imezingatia elimu, imezingatia barabara, imezingatia afya, imezingatia maji, imezingatia mambo yote muhimu kwa maendeleo ya binadamu, lakini bado wapinzani wanashindwa kuelewa. Labda ubadilishe lugha ujue kila kiongozi wa upinzani kabila lake muwe mnatengeneza Bajeti kwa lugha yake aliyozaliwa nayo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili aweze kusoma kwa sababu katika kusoma kuna kitu tunasema *reading between the lines*, halafu kuna kusoma tu baba, paka jana alikwenda, alirudi, sasa haya mambo yanatofautiana. Bajeti ya Serikali ni lazima uwe na hekima na busara, na ni lazima uzingatie unaposoma, unasoma nini. Mheshimiwa Waziri Mkuu yumkini mimi nakupongeza sana na ninakuombea maisha marefu sana na naomba kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu tena. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Kabla sijafanya hivyo naomba na mimi niungane na wazungumzaji waliotangulia, kwanza kwa kuipa pole familia ya marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga na wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa msiba wa Ndugu yetu Abu Kiwanga na *Inshallah* Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin*.

Vile vile naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea wa Urais. Vile vile naomba nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza, na vile vile nimpongeze Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuteuliwa kuwa mgombea Urais wa Zanzibar. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo naomba niungane na wenzangu pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Baraza lake la Mawaziri kwa kazi nzuri ambayo wameweza kuifanya katika nchi yetu kwa kuweza kuimarisha uchumi wa nchi na kuweza kuiletea maendeleo nchi yetu ya Tanzania. Vile vile naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji kwa hotuba zao nzuri zenye mwelekeo mzuri wa maendeleo. Vile vile naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hii hotuba yake ya leo. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, mimi nilikuwa naomba nianzie katika Bajeti nzima hasa nikianzia na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hasa jana alipokuwa akitoa majumuisho kwa kuelezea mafanikio ambayo yamefanyika. Nianzie pale alipokuwa amezungumzia juu ya Mikoa, juu ya Wabunge wa Mikoa waliokwenda kuongea naye juu ya Mikoa yao kupata Bajeti ndogo na Mikoa hiyo ilikuwa Singida, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yake ameelezea vizuri sana jana kwamba kulikuwa na mafanikio gani. Lakini nilikuwa namwomba katika yale mafanikio aliyoyaelezea kwa ile Mikoa ambayo amejaribu kuiongezea Bajeti kwa sababu ilikuwa ikipata fedha kidogo aendelee kuiangalia ile Mikoa ambayo kama ameisahau sahau na husasan Mkoa wa Singida na mingine ambayo hakuwa ameelezea mafanikio mazuri zaidi. *(Makofi)*

Kwa kuanzia mimi nilitaka nianzie juu ya suala la mawasiliano, ili kuweza kuleta maendeleo mazuri lazima kuwe na mawasiliano hasa katika upande wa barabara. Barabara zikiweza kuimarishwa kunaweza kukaleta maendeleo mazuri sana na hasa ukizingatia kwamba nchi yetu inategemea kilimo kama uti wa mgongo. Kwa sababu kama barabara zikiweza kuimarishwa basi hata hawa wakulima ambao wanazalisha wanakuwa na uwezo wa kuuza mazao yao, kwa sababu wanaweza wakayatoa mashambani na kupeleka katika maeneo ya masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika Jimbo langu barabara ambazo nataka kuzungumzia kwanza ni ya Itigi - Rungwa, pili, nataka nizungumzie ya Itigi - Tabora kwenda mpaka Kigoma ambayo vile vile inaunganisha na nchi ya Kongo. Barabara ya Itigi - Rungwa, kwa sasa hivi inafanyiwa matengenezo na *TANROADS* kwa mkopo wa kutoka *ADB*. Bahati mbaya fedha ambazo tumepewa kama mkopo hazitoshi kufanyia matengenezo barabara yote. Lakini naomba niishukuru Serikali kwa kuweza kufanikisha kupata huo mkopo na kuweza kufanya matengenezo katika sehemu ya barabara, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kuendelea kuiomba Serikali iendelee kutafuta fedha ili barabara yote iweze kufanyiwa matengenezo. Hii barabara ni muhimu sana, imekuwepo toka wakati wa ukoloni kama ilikuwepo wakati wa ukoloni sioni kwa sababu gani leo isiwe na umuhimu. Watu waliokuwa wanakaa Mikoa ya Kusini, Ruvuma, Iringa, Mbeya na Rukwa waliokuwa wanasoma Tabora na Makerere, walipokuwa wakienda katika shule au katika vyuo wanaijua sana walikuwa wakipita njia hii na waliokuwa wakitoka Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora na waliokuwa wanasoma shule kama za Mkwawa na nyingine za huko Kusini wanaifahamu sana hii barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini umuhimu na ubora wa hii barabara uliokuwepo miaka hiyo sasa hivi haupo kwa sababu barabara haijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu. Sasa huo ni umuhimu wa kwanza, lakini umuhimu mwingine hii barabara ndio ukanda wa uzalishaji kwa Mkoa wa Singida na ukanda wa kiuchumi kwa Mkoa wa Singida kwa sababu kwanza tuna mbuga za wanyama za *Rungwa* na *Muhesi Game Reserve* ambazo kwa Taifa letu zinaingizia sio chini ya milioni 180 kila mwaka. Lakini vile vile kuna mazao mengi tu kama mahindi, mazao ya misitu kama asali yanatoka katika eneo kama hili, na haya mazao yanaenda Mikoa mbalimbali kama Arusha mpaka Kilimanjaro na mpaka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile ninapooomba hii barabara itengenezwe tunaomba kufungua Mkoa wa Singida na Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1975 wakati Kiwanda cha Songwe cha Saruji kilipokuwa kinajengwa nilipata kusoma kwenye Gazeti kwamba hiki kiwanda kilikuwa kinategemea kupata *gypsum* kutoka Itigi. Lakini kwa sababu ya ubaya wa barabara, Itigi kuna *gypsum* nyingi sana, na *gypsum* inayotumika katika kiwanda cha *Wazo Hill* yote inatoka Itigi. Lakini huwezi ukapeleka *gypsum* kiwanda cha Songwe kwa sababu ya ubaya wa barabara, kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo lijaribu kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali pia ilikuwa ikiahidi kwamba itatengeneza barabara ya lami toka Mbeya mpaka Rungwa mpaka Itigi kwa awamu. Nashukuru kwamba mpaka sasa hivi huo mpango umeanza kutekelezwa mpaka Makongorosi. Lakini ukiongea na wataalam kwamba kuna mpango gani wa kutengeneza barabara ya lami, kunakuwa na hali ya mashaka mashaka wanakwambia hii barabara haina magari ya kutosha. Kiutaalam wanasema *average traffic per day* ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekulia Dodoma, zamani kabla ya kujengwa barabara ya lami kutoka Dodoma kwenda Morogoro, usafiri wa basi kutoka Dodoma kwenda Morogoro mpaka Dar es Salaam ilikuwa hakuna. Kuna wakati lilikuwepo *bus* moja *central bus*, wakaendesha, wakaacha likaingia basi moja linaitwa Mazengo basi hilo likaendeshwa ikaacha, *CRCU* waliendesha mara moja wakaacha. Lakini baada ya kujengwa lami Dodoma - Morogoro, leo hii kuna mabasi mia kidogo. Kwa hiyo, mimi nina amini kabisa na hii barabara kama itatengenezwa kwa kiwango cha lami, magari yatakuwepo mengi bila mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mwingine, barabara ya kutoka Dodoma kwenda Tabora mpaka kwenda Mwanza, Shinyanga mpaka Kagera ni ya vumbi. Leo hii mabasi mengine ya kwenda Mara au Musoma au Mwanza yanapitia Nairobi na yanayokwenda Bukoba na yenyewe yanapitia Nairobi, Kampala ndio yanakwenda Bukoba. Lakini, je, kama kungekuwa na barabara ya lami ya katikati hapa, nani angezunguka kwenda upande huo wowote? (*Makofi*)

Kwa hiyo, suala la kutanguliza kwamba kwanza kuwe na magari mengi, ndio uanze kutengeneza barabara ya lami, naomba kisiwe kigezo. Hata wanakokata mbao misituni, watu wanakwenda kukata mbao halafu wanatengeneza barabara japo sio nzuri ndio gari linapita. Hawapeleki gari kwanza ndani ya msitu halafu ndio ifuate barabara, hapana. Hilo nilikuwa naomba litazamwe vizuri na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ni ya Itigi - Tabora, barabara hii ni muhimu sana. Kabla ya matengenezo ambayo yamekwishafanyika mpaka hivi sasa kulikuwa hakuna magari yaliyokuwa yakienda Tabora kimsingi, lakini baada ya Mkoa wa Tabora kutengeneza na sisi Mkoa wa Singida kutengeneza, kwa huo muda mfupi tu ilifikia magari kwa siku yanafikia 32. Kati ya hayo magari, 20 ni magari makubwa ya zaidi ya tani 50 na mabasi makubwa. Sasa upande wetu wa Mkoa wa Singida walikuwa wamefikiria kuiomba Wizara ituongeze fedha ili iweze kufanyiwa matengenezo iweze kuruhusu magari ya ukubwa wa aina zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwe tunatazama tu maeneo ya katikati, tuelewe kwamba hii barabara ikiweza kutengenezwa mpaka kufika Kigoma, mizigo ya Kongo itapita pale kwa sababu kuna usafiri. Tusitazame tu pale Itigi mkaona kama ni mahali padogo sijui au Tabora, hakuna uchumi lakini tuangalie na zaidi ya hapo.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba nalo niliseme, kwa hiyo, nilikuwa naomba vile vile barabara hii Serikali iangalie uwezekano wa kuitengeneza katika kiwango cha lami na nina imani itaingiza uchumi mkubwa tu.

Nilikuwa napendekeza kwa matengenezo ya barabara kigezo cha kutoa pesa iwe ni urefu wa barabara. Kwa sababu mwenye barabara ndefu ndiye anahitaji pesa nyingi kwa ajili ya matengenezo, tusiwe tunagawa tu bila kuangalia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine nilikuwa naomba nizungumzie suala la Daftari la Wapiga Kura. Wakati wa kuandikisha wapiga kura Serikali iliweka waandikishaji katika ngazi ya vijiji tena katika kijiji kimoja walikuwa wanaweza wakawa waandikishaji hata wanne au watano au hata sita, lakini katika zoezi la uhakiki Serikali imefanya uhakiki katika ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitolea mfano nina Kata moja ya Rungwa ina vijiji vitatu, lakini kutoka kijiji cha mwanzo hadi cha mwisho kuna maili 40 laribu kilometa 64 na katikati kuna kijiji kimoja. Sasa kwa uhakiki wa aina hii wananchi hawakuweza kupata nafasi ya kwenda kufanya uhakiki kwenye hilo Daftari la Wapiga Kura katika ngazi ya Kata, kwa hiyo, kuna wengi sana hawakwenda kuhakiki majina yao.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali itakapofika wakati wa kupiga kura kama mwananchi jina lake litakuwa limekosewa kidogo basi asiwekewe kikwazo kwa sababu Serikali yenyewe ndiyo imesababisha. Sasa kama wakati wa kuandikisha umepolekwa katika kijiji waandikishaji wengi kwa nini wakati wa kuhakiki hukufanya namna hiyo kuwarahisishia. Kwa hiyo, hilo nilikuwa naomba lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho sijui kama muda utaniruhusu nilikuwa nataka nizungumzie suala la *Mafuta House*. *Mafuta House* ilikuwa mali ya Shirika la *TPDC* ambalo mpaka leo bado lipo na linaendelea kufanya kazi zake za uendelezaji wa nishati ya mafuta. Hawa *TPDC* walikuwa na jengo lao la *Mafuta House* ambalo Serikali imeamua kulipeleka kwa *NSSF*, wamelipeleka huko ina maana kwa sasa hivi *TPDC* wataendelea kufanya kazi katika utaratibu wa kukodisha majengo lakini lile jengo walikuwa wameli-*design* kuwa na mabohari yao ya kuweka sampuri zao za miamba ya mafuta ambazo sasa hivi hizo sampuri zimewekwa nje ya nchi kwa gharama kubwa.

Lakini vile vile walikuwa wame-*design* kuwa na ukumbi kwa ajili ya kufanyia mikutano na wawekezaji wa mafuta kutoka nje kwa hiyo, kama Shirika lipo na linaendelea na kazi zake ina maana itabidi lifanye kwa gharama kubwa, waliomba wapatiwe na wao nafasi au umiliki wakaambiwa hawataweza kama wanataka watapangishwa kama mpangaji mwingine kwa *rate* ya kibiashara, sasa mimi nilikuwa nafikiri huu uamuzi si sahihi ni vizuri Serikali ikafikiria upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile jengo lilikuwa ni mali ya umma, Serikali ilitoa pesa. Mali ya Umma kwa maana ya kwamba ni mali ya wananchi wote, unapopeleka *NSSF* maana yake itakuwa ni mali ya wafanyakazi tu ambao ndiyo maslahi yao yako pale, kwa hiyo, umenyang'anya sehemu ya haki ya Watanzania wengine. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo litazamwe na ikiwezekana *TPDC* warudishiwe na wao umiliki ili waweze kutumia zile sehemu zao ambazo walikuwa wamezi-*design* kwa ajili ya kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nilikuwa na lingine la kuzungumzia lakini kwa sababu nina uhakika muda hautatosha naomba niishie hapo na nikushukuru kwa kunipa nafasi lakini naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi kuweza kuchangia hotuba iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kutokana na hotuba yao ambayo ni nzuri kabisa, inafahamika na kwa kweli ukiiangalia hakuna hasa la kuchangia isipokuwa kuboresha tu kidogo lakini kazi hiyo tulikuwa tumeshamaliza kutokana na hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kwa niaba ya Jimbo la Chwaka kutoa rambirambi kutokana na kifo cha Mbunge mwenzetu, jirani yetu ambaye yuko katika mstari wetu, Mheshimiwa Abu Kiwanga. Mwenyezi Mungu roho yake ailaze mahali pema peponi. *Amin.*

Pili niwapongeze wenzetu ambao kwa kipindi kifupi tu tuliwachagua kugombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, mgombea mwenzake Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume. *(Makofi)*

Baada ya kupita tendo hili, nilichogundua kwa wenzetu hususan Chama cha *CUF* hawakufurahi, naamini walikuwa na imani wana mtu wao wamchague lakini kwa bahati kinachochagua siyo chama chao na ushahidi tumeuona hapa Msemaji Mkuu leo alithubutu kutaka kumtaja wanayemtaka wao. Lakini kwa bahati akajibana kidogo lakini sisi tunamjua. Kwa hiyo, huu ni ushahidi wa dhati kwamba Chama cha Mapinduzi kimeshapata ushindi kwa sababu shabaha walizotega wao hawakufanikiwa. *(Makofi)*

Lakini pia wale ndugu zangu hasa wa Tanzania Bara waliojiunga na Chama cha *CUF*, mimi nawapa pole sana. Nawapa pole kwa sababu historia ya Chama hiki hamuijui, na kuanzia leo mkiondoka Bungeni tafadhali nifuatani, mnifuate niwaelimisheni historia ilivyo na hata kikaja chama hiki kwa sababu niliona mnachapia gari lakini kwa bahati hamuijui inakwenda wapi. Mmeshafika mahali mnapokwenda mnasema huku unatupotosha na ndiyo mlifikoka, poleni sana, poleni ndugu zangu na ushahidi mzuri leo tumeuona. *(Kicheko)*

Hapa bajeti ambayo ndiyo inayofanikisha maendeleo ya nchi bado unasema *abstain, no*, maana yake nini? Kweli inaingia akilini? Sasa muwaelewe hebu angalieni yupo hata mmoja hapo? Yupo hata mmoja hebu angalieni.

WABUNGE FULANI: Wapo!

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Wako wapi? Kama ilikuwa sasa hivi tayari ofisi kule mngewaona *walahi* mbele, posho mbele Haki ya Mungu. Mara nyingi wana kawaida hapa labda kuikebehi Zanzibar kwamba Seif Shariff kashapata Urais, huyu mwacheni aende Mtambwe agombee Baraza la Wawakilishi, siyo kutawala Zanzibar, mimi nasema. Jina langu Yahya Kassim Issa, Mwandishi wa Habari nakuambia. Mwambieni akagombee Mtambwe siyo Zanzibar, Zanzibar maisha hatatawala Seif Shariff. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusijidanganye, tusijidanganye. Hebu angalieni hotuba zao na huyu Msemaji wenu Mkuu pia naye anapotea maskini, poleni sana. Jamani mimi nasema vijana wa Tanzania Bara, historia hamuijui ya Zanzibar, sisi ndiyo wazaliwa wa Zanzibar, mimi nina umri wa miaka 55 toka ukoloni, niliwahi kulipia *fees* niko darasa la saba. Mapinduzi mimi niko darasa la saba hebu njooni mniulize. Ninyi mnazungumza kitu hakina maana yoyote, hamuijui historia ninyi, mnapandia gari halina maana yoyote. Tazameni lilivyokubomoeni, lilivyokuangusheni huyu heka heka, heka heka shoga yangu huyu alikuwa amekwisha. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mimi kwa kweli sitakuwa na mengi sana, hasa nataka kuchangia kuhusu suala la uchaguzi na sitatumia muda mwingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelekea kwenye uchaguzi. Chama chetu, Serikali yetu haina dini na tumekubaliana, lakini chama kinaongozwa na watu, Serikali inaongozwa na watu na ndiyo tumo humo, hivi vitu viko wazi havikujificha, tumo humu na tunapanga mipango hivi.

Mimi nasema na ninatoa mawazo hivi, sasa 30 Oktoba, 2005 tunategemea uchaguzi wetu na uchaguzi uko katika mwezi wa Ramadhani. Mwezi wa Ramadhani ni moja katika nguzo za Waislam ni ya lazima hiyo katika nguzo tano, hiyo ni lazima na mwezi wa Ramadhani kwa akina mama ni mwezi wa heka heka, muda wao mwingi wanautumia kwa kutayarisha shughuli zao za futari. Kwa hiyo, muda mwingi sana wanatumia na kuanzia mnamo saa sita pengine mpaka wakati wa kufuturu kwa kweli akina mama wako katika shughuli za kazi na si sehemu zote zenye mifereji kwamba atainuka tu pale anakinga maji si kweli. Mengine lazima wafuatilie na tuliona wakati wa kuandikisha tu kuna sehemu watu wetu wanaishi masafa kutokana na vituo vya uchaguzi, wanaishi sehemu kubwa kama mimi nasema katika Jimbo langu watu wanatoka Ziwiani waje Kisomanga mahali hapapungui kama maili tano siyo mahali padogo, kwamba atoke kule mtu afate kituo na mwezi wenyewe ni ule hakula, kazi kubwa na kazi nzito kwa akina mama na wakati uleule mama anatakiwa akatayarisha chakula, sasa mimi suala hili nalitaka tupeane mawazo na tulifikirie kwa makini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mmoja ulitokea hapa Kilwa katika Serikali za Mitaa. Ninaye ndugu yangu ambaye kila wakati tunazungumza, kina mama wengi hapa wanajiandikisha na ilikuwa si mwezi wa Ramadhani tujiulize kwa nini? Muda unakuwa mkubwa sana na kunakuwa na shughuli za nyumbani lazima wakazifanye. Walimaliza mpaka saa sita za usiku nani atastahimili muda huo, sasa kuna mambo lazima tuyapange na sheria kweli zinakuja lakini haya mambo yetu wenyewe na kama hatukupanga sisi basi atatupangia nani? Kuna sheria ngapi za uchanguzi zimeondolewa, leo unaambiwa kama wewe unagombea na umeona mambo magumu unajitoa hata kama umeshapigiwa kura, kura zile hazihesabiwi yalikuwa hayapo haya, lakini yalipitishwa baada ya kuona hali halisi ilivyo.

Sasa mimi kubwa ninaloliomba kutokana na ushauri wangu kwanza vituo viongezwe kwa wingi sana katika sehemu zote. *(Makofi)*

Pili, zile sehemu ambazo watu wanafuatilia masafa marefu basi vituo sehemu zile navyo viwekwe ili wapunguze matatizo hayo. *(Makofi)*

Tatu, akina mama wapewe kipaumbele katika upigaji kura kwa sababu hawa kwanza ndiyo wengi, hawa ndiyo wengi. Tukifanya vingine vyovyote tutakuja kujilaumu watu wamejiandikisha tu kwa wingi lakini hawakupiga kura, tutakuja kujilaumu kwa sababu hakuna kipengele kwa muislamu atakachosameheka kwa kuwa hakufunga kwa sababu leo atapiga kura kwa hiyo, hafungi. Moto utachezea, hakuna msamaha huo, hakimo katika taratibu hicho. *(Makofi)*

Nne, upigaji kura uanze mapema mnamo saa moja. Hii ina maana tunafupisha ili shughuli mapema tuwape fursa akina mama kwenda kufanya shughuli zao mapema na mipango yetu kwamba isiharibike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, ulinzi uimarishwe kwa hali ya juu na ya pekee ili vurugu zisitokee na kusababisha ucheleweshaji wa kupiga kura. Nasema hivyo kwa sababu hawa wenzetu hawa, hawa wanajua hawapati kitu lakini ni watu walalamishi sana hawa, lakini wameshajua hata hiyo Zanzibar kuwaambia tena nawaambieni nyote na ulimwengu uelewe Chama cha Mapinduzi ndicho kitakachoshinda na kitaongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa kuwa nina uhakika na ndivyo yalivyo nasema ushindi kwa Chama cha Mapinduzi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. ESTHERINA KILASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Waziri Mkuu.

Kabla sijaanza kuchangia naomba niungane na Wabunge wenzangu kuwapa pole wananchi wote, ndugu na jamaa wa Jimbo la Kilombero kwa kuondokewe na mpendwa wao, Mheshimiwa Abu Kiwanga. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vile vile kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa kuwa mgombea anayetokana na

Chama cha Mapinduzi kugombea Urais uchaguzi ujao wa tarehe 30 Oktoba, 2005, ninaamini atashinda kwa kishindona namtakia mafanikio mema. *(Makofi)*

Nimpongeze Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kushika bendera ya CCM kugombea nafasi ambazo wamepewa na ninawatakia mafanikio mema vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nianze kuipongeza kwa dhati hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja. Hotuba ambayo ni nzuri, yenye mweleko, hotuba ndefu kwa mtu wa kawaida usingeamini kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu angeweza kusimama kwa saa mbili na dakika, bila kutetereka kwa hiyo, tunampongeza sana, haijawahi kutokea. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Haijawahi!

MHE. ESTHERINA KILASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri Mkuu kwa kazi ambayo ameifanya kwa vipindi vyote viwili na hii inaonyesha kwamba alionyesha imani kubwa kwa Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa na hatimaye akamteua kwa vipindi vyote viwili na *record* kwake. *(Makofi)*

Lakini niwapongeze na askari wa mianvuli wote kwa pamoja kwa sababu peke yake asingeweza kufanya kazi hii vizuri, wamemuunga vizuri na mimi kama Mbunge na mwakilishi wa wananchi wa Mbarali nawapongeza sasa hawa askari wa mianvuli kwa sababu wamepata nafasi niseme labda zaidi ya Mawaziri wa Baraza hili kama Mawaziri 20 wameweza kutembelea Wilaya yangu ya Mbalali. Sasa Mawaziri wote hawa wamekuja kwa njia ya kuendesha *harambee*, kuweza kutembelea miradi mbalimbali na wale waliofanikiwa kutembelea miradi mbalimbali hawakuweza kuondoka hivi hivi, wameweza kuchangia kwa hali na mali katika kuwaunga mkono wananchi wa Mbarali kwa hiyo, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri Mkuu ni nzuri na inajieleza vizuri na ndiyo maana wote tumeunga mkono kwa asilimia mia.

Sasa mimi nina maeneo machache ambayo ni kuboresha au ya kuchangia hapa.

Sehemu ya kwanza ningependa kuchangia kwa upande wa elimu hasa upande wa MMES. Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia katika hotuba yake kwa kweli tunapongeza sana Serikali upande wa MMEM, sasa MMES kidogo ningependa kupendekeza kwamba zile taratibu zilizowekwa katika kugawana pesa hizi za MMEM kwa madarasa kidogo ilileta tofauti kubwa na hasa kigezo ambacho kiliwekwa katika kugawa hizo pesa za MMES sana sana walizingatia idadi ya wanafunzi ambao wamemaliza darasa la saba. Sasa Wilaya nyingine unakuta wanafunzi idadi ni ndogo lakini shule ni nyingi na madarasa ni mengi kwa hiyo, unakuta Wilaya moja imepata vyumba vingi vya madarasa, Wilaya nyingine imepata vyumba vichache vya madarasa.

Sasa kama kuna uwezekano wa kuweza kubadili hili ili wote twende kwa uwiano kwa sababu kila Kata, kila Wilaya imeweza kujenga shule za sekondari kwenye kila

Kata. Lakini unakuta Wilaya moja inapata madarasa matatu, nyingine inapata vyumba na madarasa 40 na vingine 50 sasa labda huo uwiano uongezwe au urekebishwe ili tuweze kuwa na uwiano ambao unafanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ile Tume ambayo aliiteua ya kuweza kupitia kwenye kila Wilaya kujua matatizo ya walimu. Hii imetuletea kwa kweli sifa kubwa sana hasa kwa walimu kuondoa kero zao za mafao na mpaka sasa walimu wanaendelea kulipwa, wale ambao walilipwa awamu ya kwanza na sasa wanalipwa awamu ya pili. Kwa hiyo, nampongeza sana kwa hilo na ile Kamati ilifanya kazi nzuri sana na walimu kwa kweli wamefurahi sana kwa kazi ile ambayo ilifanywa na Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuchangia ni lile ambalo lilitolewa kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango kwamba sasa juhudi kubwa zinawekwa kuhakikisha kwamba pesa zinapelekwa kwenye Halmashauri ili ziwe karibu na wananchi. Sasa Waheshimiwa Wabunge wengine wakasema kwamba si vizuri, afadhali zibaki huko Wizarani kwani zikifika huko Halmashauri zitatumika vibaya.

Sasa mimi nafikiri la msingi wengi tumekuwa tukilia kwamba pesa zifike kwenye Halmashauri ili iwe rahisi sana kutumia na kufuatilia miradi kwa karibu kuliko zikikaa mbali sana na Halmashauri, cha msingi hapa ilikuwa ni kuboresha tu huduma za uhasibu kwenye kila Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maboresho yamepita na ninaamini kabisa baada ya hizi shughuli za maboresho kukamilika tutakuwa na wahasibu wazuri, tutakuwa na utumiaji mzuri sana wa pesa hizi za Halmashauri, kwa hiyo mimi nasisitiza tu na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge waungane na mimi kwamba hizi pesa kwa kweli zisogee kwenye Halmashauri ili iwe rahisi kupanga na kuratibu mipango yetu ya kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano mingi tumeiona kwenye hizi pesa za *TANROAD*. Hizi fedha za mikoa kuja kwenye barabara za mikoa ziliko kwenye Wilaya inakuwa ni tatizo sana kuzipata, kwa sababu inategemea pale Meneja wa *TANROAD* atapanga barabara ipi na barabara ipi. Lakini kama zikija moja kwa moja inakuwa ni rahisi ninyi mkikaa kwenye Kamati ya Fedha na Mipango, mkapanga vizuri na kujua ni barabara gani mtengeneze. Kwa hiyo, hili nalisisitiza kwamba kwa kweli tunaomba na tunapongeza uamuzi uliofanyika kwamba fedha nyingi zielekezwe kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichonigusa sana sana katika hotuba hii ya Waziri Mkuu ni pale ambapo amezungumza kabisa kwa dhati kwamba lengo kubwa la safari hii naye amesisitiza kwenye upande wa MKUKUTA. Waziri wa Fedha amesema hili. MKUKUTA maana yake Tukuze Uchumi na Kuondoa Umaskini kwa Wananchi. Sekta muhimu ambayo itasaidia na inayosaidia kwa wananchi kuondokana na umaskini wengi tumelalia kwenye upande wa kilimo, ukiboresha kilimo maana yake mwananchi wa

kawaida mwenye maisha yoyote ya chini, mwenye ardhi yenye rutuba na pembejeo nzuri akalima, akavuna, hakika ataondokana na umaskini.

Mimi naguswa na hili, ni bahati mbaya sana Wilaya ya Mbarali ardhi ambayo ilikuwa imeendelewa hapo nyuma na ambayo wananchi wengi walikuwa wanaitegemea wa Mbarali ni yale mashamba ya umwagiliaji na hayo mashamba ya umwagiliaji yalikuwa chini ya *NAFCO*. Sasa chini ya *NAFCO* wananchi pembeni angalau walikuwa wanalima, wanaweza kupata maji ambayo yanahudumiwa na *NAFCO*.

Sasa mwaka 2001 ndiyo nilitaka kujua Serikali kumetokea nini kwenye Serikali kwa sababu mwaka 2001/2002 hapa hapa ndani ya Bajeti Waziri wa Kilimo na Chakula, alisoma hotuba yake na akasema mashamba yote ya *NAFCO* yatabinafsishwa hasa yale ya Hanang, lakini mashamba haya mengine ya mpunga likiwemo shamba la Mbarali, shamba la Kapunga litagaiwa katika sehemu ndogo ndogo za ekari nne, nne, ili waweze kubinafsishiwa, wananchi siyo wapewe bure bali wamilikishwe kwa kulipa fedha ambayo Serikali itathaminisha kuonekana kwamba wanaweza kulipa kwa hiyo na mimi kama Mbunge nilivyotoka hapa na ile *speech* au ile hotuba nimefika kwenye mikutano ya hadhara nikasema Serikali imeamua kwamba mjiandae haya mashamba yatagaiwa katika ndogo ndogo ekari nne nne ili muweze kumilikishwa na tukaunda Kamati ya Wilaya na tukachukua wataalamu mbalimbali tukawa tunasubiri sasa *PSRC* waje wapime yale mashamba katika hizo ekari nne, nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya muda mwaka 2003/2004 ikasomwa tena hapa kwamba hatuwezi kugawanya kwa ekari nne, nne, sana sana tutaweka kama *plot* zilivyo, ila la msingi tutasema tu wale wenye uwezo wa kununua, wanunue tukasema ni sawa. Mwaka jana mimi na wananchi wangu tukaona tangazo kwenye gazeti kwamba shamba la Mbarali linatangazwa kwamba yeyote ambaye yuko tayari kununua atende aweze kuomba kununua.

Kwa hiyo, sasa kwa pale tulipokuwepo kwanza kulikuwa na wafanyakazi ambao wako pale wakahangaika kwamba labda tuunde ushirika tuweze kupata nafasi ya kununua haya mashamba. Wananchi walikuwa na hamaki kwa sababu wamekuwa wakikodi yale mashamba kwa muda wote kwa miaka yote hii ambayo *NAFCO* imeshindwa kuyaendesha, miaka mitano wamekuwa wakikodi ekari moja, moja, mbili, mbili, wanalipa, walikuwa wanakodisha ekari moja kati ya shilingi 20,000/= Kapunga kwenye shilingi 65,000/= lakini waliweza kumudu kukodi na kulima.

Sasa ilivyotangazwa kwamba yanauzwa wananchi wakaanza kuungana sasa labda tuombe ushirika. Wakaenda Wizara ya Kilimo wakaambiwa kwamba ninyi mkitaka kuwahi hili sana sana muungane ushirika ili muweze kuomba kama Ushirika, kwa kweli wananchi kwa harakati kwa haraka wakachanga wengine pesa zao, shamba lingine walichanga mpaka milioni 80, 90 ili waweze kuwahi hicho kitu.

Sasa wanaandika saa ngapi kwa sababu muda waliopewa ni mwezi mmoja, wataomba mfadhili gani ili aweze kuungana nao kusudi waweze ku-*tender* kwa pamoja

ilikuwa siyo rahisi kwa hiyo kile walichokuwa nacho na uwezo waliokuwa nao wakaweza kuandika ule mchanganuo wao na kuweza kuupeleka *PSRC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana vyama vyote vya ushirika ambavyo viliweza angalau kupata nafasi ya kuandika kuomba vikawa vimeshindwa, wengine walishindwa tu kwenye *financial proposal*, wengine walishindwa kwenye *technical proposal* kwa hiyo, wakabaki sasa wanatahayari kwamba tunafanya nini.

Sasa baada ya hapo wananchi wamekuwa wakiangalia tunafanya nini na huu MKUKUTA umefika fursa waliyonayo wananchi wa Mbarali ni sehemu ambayo imeendelezwa ambayo ndiyo hayo mashamba ya *NAFCO* na wamejitahidi kwa kila nia, kwa kila hali kwamba wachange pesa zao, wauze mali zao ili waweze kupata hiyo ardhi au Serikali iweze kubinafsisha tu ile miundombinu labda vile vinu au vile vitu ambavyo wao hawawezi kuviendesha, lakini mpaka sasa imekuwa ni tatizo wameshindwa kumudu kwa sababu muda umekwishapita na makampuni mengine yameshatangaza kwamba yamepata kutokana na *PSRC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa walichokuwa wanakisali kila siku kwamba waone uamuzi wa Serikali kama unaweza ukasitisha angalau tuboreshe huu ushirika, angalau wananchi watumie hiyo fursa ya hayo mashamba wajiendeleze na wao waendane na wenzao katika huu mkakati wa Serikali ambao umewekwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juzi tu tumepitisha kuwawezesha wananchi waweze kuondokana na umaskini sheria hapa imepita, wakajua na sisi tutawezeshwa kwa hili ili angalau hii fursa iliyopo kwa sababu Mbarali ni kama haina mvua na ninapozungumza sasa hivi mwaka huu hatukupata mvua wanachokitegemea ni mavumo tu mpunga na mpunga huo unalimwa kwenye hayo mashamba mawili kwa sababu wamekuwa wakikodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nishukuru Serikali kwa sababu mwaka jana walisitisha hii *process* isiweze kuendelea sasa hatujui hatma yake itakuwa ni nini baada ya hapa. Kusitisha ni moja kwa moja au hawa ambao wametangaziwa kwamba haya mashamba watayapata watapewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ubinafsishaji wake umekwenda vizuri sana zile *Ranch* wamezigawa katika vitalu vidogo vidogo, wamevitangaza na sisi tumepewa vile vitabu unapitisha mpaka kwenye kijiji watu wamepata nafasi ya kusoma wame-*tender* wenyewe pale waliposhindwa wameshindwa wao na ndiyo maana unakuta hakuna malalamiko yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa haya mashamba hasa ya *NAFCO* ekari 3000 ingeweza kudumisha wananchi sana na kuwaboresha katika maisha yao na katika kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hili, yeye mwenyewe Waziri Mkuu alipotembelea Mbeya katika ziara yake ya kikazi, walivyosikia Waziri Mkuu anakuja wananchi pale waliandamana, wanataka kumwona Waziri Mkuu. Lengo la kuja

kumwona, ni aone ni vipi atawasaidia, waone kwamba yeye atakuwa mkombozi wao na sasa wameungana hata watu Hanang, watu wa Kilimanjaro huko wana-*appeal* kwenye haya mashamba kwamba tuachiwe ardhi, vitu vingine tuwaachie watu wenye uwezo na ni bahati mbaya au bahati nzuri hao waliopewa mashamba ya Mbarali, wale wawili wote wanatoka wanatoka Mbarali, huyo mmoja aliyeomba kapata, ni mwananchi wa Mbarali.

Kwa hiyo, ingekuwa ni vizuri naye akashawishiwa akaungana na wananchi ukawa Ushirika ili waweze kugawana katika hiyo mali. Ardhi wapewe wananchi, yeye apewe vile vitu aendeshe ile miundombinu ambayo wananchi hawawezi kuendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, namwomba Waziri Mkuu na Mawaziri wote wanaohusika na dhamana hiyo, waangalie ni vipi wanaweza wakatengua hili ili kuweza kuwasadia hawa wananchi. Kwa kweli hali ni ngumu hawajui watajikwamuaje na huo mkakati.

Lingine naamini kabisa hili litakuwa limesikilizwa na mkikaa kwenye Baraza la Mawaziri muone ni vipi ambavyo mtawafanya hawa wananchi wa Mbarali wasitawaliwe kifikra, wasitawaliwe kiuchumi. Kwa sababu mkishawanyang'anya hiki kinachotegemewa, mnajua historia ya Mbarali, kwa kweli wananchi watajisikia ni wanyonge, watajisikia kwamba Serikali yao haipo na haiwaungi mkono, kwa hiyo, naomba sana sana mlifikirie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kwa upande wa UKIMWI, suala hili nililizungumza wakati nachangia Wizara ya Afya na kuna swali la nyongeza niliuliza, kwamba hizi dawa za UKIMWI, kuna hospitali chache tu ambazo ziliteuliwa kupelekwa hizi dawa za kurefusha maisha. Hali ilivyo ni ngumu, hali ni mbaya sana, kwa kweli sisi Wabunge tunaona na unaona watu kila mahali unapokwenda, wanapohitaji hizi dawa, sasa kusafiri mbali ni tatizo.

Ningependekeza tu kwamba, kwa sababu pesa hizi za UKIMWI tumeongezewa sana na dawa zinakuja, Wizara ifikirie au Waziri Mkuu katika Wizara yake katika Kitengo chake cha kudhibiti UKIMWI, aone ni vipi hizi dawa zitafika kwenye Hospitali Kuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini iwe karibu na wananchi, hasa hizi dawa za kurefusha maisha, kwa akinamama wajawazito, zile wanazomeza wakati wanasubiri labda mama ameathirika ili apewe kuinga mtoto asiambukizwe. Kwa kweli tungeomba na naendelea kuisitiza kwamba hizi dawa zinawafikia na zinakuwa kwenye hospitali ya Wilaya, kwa sababu Wilaya zote zina hospitali za Wilaya ili iwe karibu. Maana yake tulichaguwa hospitali chache labda tulikuwa hatuna uwezo wa pesa, sasa hali kutokana na Bajeti ambazo tumezisikia hapa na wafadhili mbalimbali wanaounga mkono katika kudhibiti UKIMWI, ninaomba lifikiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja.
(*Makofi*)

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kwa kushukuru na mimi kama walivyonitangulia wenzangu napenda nichukue nafasi hii kutoa rambirambi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Sikonge kwa wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kuondokewa na mwakilishi wao, Mheshimiwa Marehemu Abu Kiwanga, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuwapongeza wanachama wa Chama cha Mapinduzi wote 11 waliojitokeza katika zoezi la kuomba kuteuliwa kuwa wagombea wa Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Walionyesha ujasiri na kwa kweli walionyesha ni jinsi gani basi Chama cha Mapinduzi kimejengeka katika misingi ya demokrasia. *(Makofi)*

Kwa namna ya pekee ni mpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea wa Urais. Nami sina mashaka yoyote kwani nyota njema huonekana asubuhi, ni miezi michache ijayo atakuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya leo asubuhi, imejaa mafanikio ya utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi, na mimi sitaki kuyarudia, wale watako pata bahati ya kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi watakuwa wanaitumia hii katika kunadi sera za Chama cha Mapinduzi ili kiweze kupata kura, kwa hiyo, sitaki kuyarudia rudia. Lakini nataka niseme tu kwamba mafanikio haya yapo kwa wenye macho wanayaona, yamejaa vijijini, yamejaa mijini yanaonekana kwa macho. Sasa hotuba ya leo ya Mheshimiwa Wilfred Lwakatare ilikuwa inatonyesha kabisa kwamba wapo watu wengine hawayaoni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi tunafahamu kabisa kwamba wapo watu wenye tabia za kuzaliwa nazo, anaweza akazaliwa hivyo kwamba yeye malezi yake ni ya ubishi. Sasa ya kubisha hata kama kuna kitu ambacho kwa kweli kinaoneka yeye anabisha tu. Sasa mengine ni malezi inapaswa tuwasamehe, ndivyo walivyojaliwa na wengine inawezekana wakawa wanayo macho lakini yana matatizo, kama rafiki zangu wagogo, inawezekana anayo macho lakini yana matatizo.

Sasa kwa bahati nzuri tunayo Hospitali ya Mvumi hapa na Mzee wangu Mheshimiwa John Malecela yupo hapa na Mvumi ni Jimbo lake. Sasa naomba wale ambao hawayaoni mafanikio ya Chama cha Mapinduzi wamwombe Mzee Malecela awapeleke hospitali wapatiwe matibabu. Kama wana matatizo zaidi watapata miwani, waende wakayaone mafanikio ya Serikali ya CCM ambayo kwa kweli yanaonekana dhahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio mengi haya, nampongeza sana Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na Serikali yake ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri aliyofanya kwa kipindi cha miaka kumi na Mwenyezi Mungu kwa kweli naomba aendelee kumweka hai muda mrefu ili wananchi wa Tanzania waendeleo kuchota fikra ambazo zitaendeleza nchi yetu kwa miaka mingi ijayo. Sasa si kazi ya Mbunge kusimama hapa na kulalamikia Serikali tu, yale mazuri yanafanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi basi ni vizuri kuipongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilisimama hapa nikatoa malalamiko ya wananchi wa Jimbo langu la Sikonge juu ya Meneja mmoja wa Pori la Ugala na nilikuwa nimetishia kwa kweli kuliangamiza lile pori kimila. (*Kicheko*)

Lakini kwa bahati nzuri nataka nimpongeze sana Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa kazi nzuri aliyoifanya. Amekuja yeye mwenyewe Sikonge, amekutana na wananchi, wananchi wamempa kero na yale matatizo yote aliyamaliza pale pale. Sasa tunataka askari wa miavuli wa namna hii. Kwa hiyo, kwa kweli Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya wananchi wa Sikonge ninakupongeza sana, yale ambayo yaliyobaki naomba Mheshimiwa Waziri myafanyiye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo machache ambayo ningeiomba Serikali kwa kweli iyatekeleze, la kwanza ni suala la mawasiliano, Wilaya ya Sikonge ni moja ya Wilaya ambazo kwa kweli zimetengwa na mawasilino ya simu. Hatuna simu za mkononi, wala hatuna simu ya *TTCL* na mimi ningependa labda Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, angefika pale akakaa wiki moja na simu zake zile zisifanye kazi yoyote labda ndiyo angeweza akaona kwamba tunayo matatizo. Kwa kweli naomba, ingawa naendelea kufanya mawasiliano naye kwa kweli nampongeza sana anajitahidi sana kuhakikisha tunapata mawasiliano Sikonge na kwa fununu tu ameshaniambia kwamba wiki mbili, tatu, zijazo *Celtel* wataenda kuanza kufanya kazi ya kujenga mnara.

Sasa *Celtel* huko mliko msimwanguzhe Waziri akawa anatoa hapa ahadi, anatoa maelezo ya kutia matumaini halafu matumaini yenyewe hayapo. Naomba sana kwa kweli *Celtel* itekeleze hilo. Lakini naomba *TTCL* nao wafanyekazi, maeneo mengine yameachwa, *TTCL* hapo awali ilikuwa inafanya kazi ya biashara na huduma, sasa nafikiri inafanyakazi ya biashara tu. Maeneo mengine yameachwa kabisa, katika karne kama hii baadhi ya Wilaya zinakaa zina simu za kukoroga, ni aibu. Naomba *TTCL* kwa kweli ihakikishe inatoa mitandao yake katika maeneo yote kama ambavyo ilani ya uchaguzi inavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka niungane na Mheshimiwa Ismail Iwvatta, kuhusu suala la barabara. Kwa kweli barabara zetu za Mikoa ya Kati zimeachwa, sisi tunazungukwa zungukwa tu, pamoja na Mheshimiwa Basil Mramba hapa kusema tunayo mikakati, hiyo mikakati tutakapoiona inaanza kwa kweli ndipo tutakapoamini. Kwa sababu tunazungukwa tu, lami zinatuzunguka tu na sisi tunazihitaji hizo lami na pengine ndiyo maana hatupati hata viongozi wa Kitaifa kwa wingi. Kwa sababu kiongozi wa Kitaifa unamsafirisha masafa ya kilometa 200 au 300 kwenye barabara ya vumbi, ni taabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba, mimi nina barabara hapa za Itigi, Rungwa kama aliyoisema Mheshimiwa Ismail Iwvatta na barabara ya Manyoni, Itigi, Kigwe, Tabora mpaka Kigoma. Kuna barabara ya Tabora- Ipole, Rungwa- Mbeya, kuna barabara ya kutoka Tabora kwenda Nzega, kuna barabara ya Tabora- Ipole - Koga inayotuunganisha mpaka na wenzetu wa Mpanda, zinaachwa tu hata fedha zenyewe zinazotengwa kwa hizi barabara ni kidogo, naiomba sana Serikali ilianganalie tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala lingine ni la utawala bora, Mahakama, tunayo matatizo kwa kweli. Tukizungumzia suala la utawala bora, tunazungumzia vile vile kukidhi haja za wananchi wetu katika suala zima la kutafuta haki zao. Wilaya ya Sikonge mpaka leo hii ina Mahakama moja tu ya Mwanzo na Hakimu mmoja. Kwa maana ya kwamba kama ataugua wiki nzima, hakuna Mahakama. Sasa huzungumzii utawala bora katika misingi ya namna hii. Lakini vile vile tuna mrundikano wa kesi nyingi sana kwenye Mahakama zetu nchini na hii inatokana na kuwa na uchache wa Mahakimu na Majaji wetu nchini.

Sasa sielewi hawa Majaji wanakotengenezewa maana mimi naangalia takwimu hapa. Mahakimu wa Wilaya, Mahakimu wa Kazi na Majaji, kutoka mwaka 1995 idadi yao ilikuwa 192. Mwaka 2004 ilipanda na kufikia 319 yaani kwa miaka tisa tulikuwa na ongezeko la idadi ya watalaam hawa 127, miaka tisa. Sasa tulione hili ni tatizo, huwezi ukategemea tunaweza tukawa na uwezekano wa kupunguza tatizo la kutokuwa na wingi wa kesi katika Mahakama zetu katika kiwango cha ongezeko hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali iangalie hili na ijenge Mahakama katika maeneo ambayo tunakwenda kuanzisha Wilaya mpya, kwa mfano ya Sikonge. Sasa unamtegemea mtu atoke kilometa 71 kwenda Tabora na mhalifu akishaona kwamba akihamisha kesi kutoka Sikonge kupeleka Tabora, basi huyu mlalamikaji hawezi kwenda kule, anafanya hivyo. Anafanya hivyo na kwa maana hiyo haki yake sasa haita kuwepo, kwa hiyo nilikuwa naomba sana Serikali kwa kweli ili iangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, leo tumesikiliza hotuba mbili, ya kwanza hotuba ya Waziri Mkuu, lakini vile vile ikafuatia hotuba ya Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

Sasa nilikuwa nafuatilia maelezo yake, naomba sana, kama nilivyosema hapo awali tuelewe kwamba maudhui yaliyotolewa na Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, tuelewe kwamba huo ndiyo upinzani wa Tanzania ndivyo walivyo, kwa maana ya kubeza kila kitu ambacho kwa kweli kinafanyika hata kama ni kizuri. Sasa nataka nisema tu kwamba, nataka niwaambie Watanzania, kama unasafiri unakwenda kwenye kituo cha basi, ukikata tiketi kabla hujaingia kwenye basi nenda mbele yake, kule ndiko huwa kuna kibao kinaonyesha basi linakwenda wapi. Maana si vizuri kupanda tu basi hujaelewa mwelekeo ni wapi, unaingia kwenye basi limeandikwa tu Scandinavia, kumbe Scandinavia sasa hvi ziko nyingi. Kumbe basi lile linakwenda Iringa na wewe safari yako ilikuwa ya kwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kasome kwanza, lakini haitoshi kwenda kusoma kule, ukiingia ndani ya basi angalia dereva anafananaje. Sasa unangia kwenye basi unakuta dereva hana shati kifua wazi kiti alichokalia ni kinu, gia yake ni ya kukamatwa na watu watatu, mtafika kweli! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mabasi mengine ndivyo yalivyo hivyo. Lakini yako mabasi safi, basi kama la Chama cha Mapinduzi, dereva safi, siti safi na gia yake wala mtu hatumii *calories*, anaweka pole pole na basi lina piga hatua.

Sasa napende nichukue nafasi hii kuwaomba Watanzania kwa kweli na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, haya ameyasema katika kipindi kizuri, tunaelekea kwenye uchaguzi, sasa ni kipindi cha kupanga na kuchagua wapi na mpande basi gani ambalo litawafikisha kuzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono hoja, ahsante sana (*Makofi*)

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi nichangie mawili, matatu, katika hotuba hii ya Waziri Mkuu. Lakini kabla sijaanza naomba kutoa rambirambi mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Koani, kwa kifo cha Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, Mwenyezi Mungu amweke mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kwa sababu binadamu tumeumbwa na kusahau moja kwa moja napenda kuunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu na naipongeza sana, kwa sababu imetufahamisha tangu alipoingia madarakani katika kipindi cha mwaka 2000 hadi hivi sasa ambapo ataachia madaraka hayo badaaye.

Lakini vile vile najua kazi hii nzuri haikufanywa na yeye peke yake imesaidiwa na wasaidizi wake wawili, Mheshimiwa Alhaj Muhammed Seif Khatib na vile vile Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, ofisi yao vile vile ilikuwa ikiongozwa na Katibu Mkuu, lakini naogopa kulitaja jina lake kwa kizungu, kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu alituaambia tusichanganye kiswahili na kizungu na jina la Katibu Mkuu lina neno la kizungu. Kwa hiyo, mimi nasema Bibi Waridi, nampongeza sana na watendaji wake wote. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nachukua nafasi hii vile vile kuwapongeza sana wagombea wetu kupitia Chama cha Mapinduzi , kwanza Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kuinyakua nafasi ya kugomba Urais wa Muungano, vile vile Mgombea Mwenza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na nampongeza kwa njia ya pekee Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kupendekezwa kugombea Urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule walipojitokeza wagombea 11, katika nafasi hizi kwa kupitia Chama cha Mapinduzi wenzetu walianza kufanya vikao vyao, kuitisha mikutano na waandishi wa habari, kwa kusema kwamba miongoni mwao akienguliwa yeyoyte kati yao, basi watakihama Chama cha Mapinduzi na kwenda kwao. Basi mimi nawaambia ole wao, walioshindwa wote tuko nao pamoja, wanafanyakazi pamoja na wataendeleza Chama cha Mapinduzi. Viongozi wa CCM wanajua demokrasia na wanajua kwamba ule ndiyo ulikuwa ni wajibu. Hatukumweka mtu mmoja peke yake kwamba wewe gombea Urais na wewe gombea nafasi hii. Hatukuweka hivyo kwa sababu ilikuwa demokrasia inaeleza kwamba yeyote anayo haki kugombea nafasi zile.

Sasa wagombea wote walioshindwa 10 tunao, tutaendelea kuwa nao na wataendelea kukitumikia Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo, na ninyi mtaona hivyo hivyo, hamtokipata kitu kamwe. Unajua sisi tulipokuwa shule, nina umri kati ya miaka 10, 12 tulikuwa tunakwenda chini ya miembe pale. Kule kwetu Zanzibar kuna tumbiri, lakini wao tunawaita kima punju. Kima punju akikaa juu kula maembe basi sisi tunakaa chini tunatarajia kwamba labda zitaanguka, tutazipata sisi. Kumbe embe zote wanazila wenyewe sisi wanatuangushia kokwa. Kwa hivyo, na wao nawaambia kwamba watazipata kokwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nagusia kidogo tu, hotuba ya ndugu yetu, kipenzi chetu, tulikuwa tunamheshimu sana Mkuu wa Upinzani Bungeni, hotuba ile naamini ameandikiwa. Laiti ingekuwa ameandika mwenyewe asingetumia nafasi ya kuandika kurasa tano, kuzungumzia masuala ya Zanzibar wakati ambao hajui chochote kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Upinzani huyu Bungeni hapa haelewi hata ule mji wa Zanzibar ulivyokaa, haujui. Yeye anasema uchaguzi, uandikishaji daftari za uchaguzi kumefanywa njama, mimi namwambia hivi, tumepewa wiki tatu Mkoa wa Kusini Unguja. Tumeandikisha na ukweli hakuna tofauti baina ya vyama vya upinzani na CCM na uchaguzi ulimalizika salama. Huko kulitokea zogo ni lao wenyewe hao hao wapinzani ndiyo waliosababisha hilo, asiingilie mambo ambayo hayaelewi. Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, kawaambia mnachupia gari ambalo hamwelewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mdogo tu kabisa, kule Zanzibar kuna magari yana *route* namba 10 yanakwenda Makunduchi, kuna bwana mmoja nadhani mwehu yule, alimwona mwanamke akawa anamtaka, akamwambia ingia ndani ya gari. Kaingia ndani ya gari hajui gari inakwenda wapi, *break* yake ya kwanza, gari imesimama Makunduchi. Alipofika pale mwanamke anateremka anamwambia kwangu pale na mume wangu yule pale, kakuelewa. Sasa kilometa 60 atatembea kwa mguu na hata hivyo hakuna gari ya jioni ya kurudi na hao nawaambia watataka kurudi gari hakuna na mwanamke hawampati. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hotuba ile nasema, laiti angekuwa amepewa rafiki yangu Mheshimiwa Thomas Ngawaiya au Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, *wallah* wangeandika hotuba nzuri sana, wastaarabu bwana hawa. Hawa ndiyo wanasiasa, hawa ndiyo wapinzani kweli hawa, wasiunganika na mambo machafu machafu kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu huyu Kiongozi wa Upinzani Bungeni anaichezea *Quran*. *Quran* ni kitabu kitakatifu ndani ya Jumuiya zetu za Kiislam, tunaseama *Quran* haichezewi na mtu hovy hovy, anakuja kutaja aya hapa hata hajui maana yake nini, tena nakwambia ana hatari huyu, atafutwe Sheikh azinguliwe na kwa humu Bungeni labda amuone Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mheshimiwa Alhaj Ahmad Mpeme na wa nne ni mimi. Kama

hakuzinguliwa yule ni hatari hapati Jimbo, kama hakuzinguliwa tena atuone haraka sana. (Kicheko)

Mimi sasa nizungumzie kidogo suala la Zanzibar kuhusu biashara, na bahati nzuri nimemwoma rafiki yangu Mheshimiwa Basil Mramba ameingia pale, lakini kwa kupitia kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, juzi alizungumzia kidogo lakini hakufahamika, suala la bandari, yeye hakukusudia bandari, alikusudia suala la biashara Zanzibar imeteremka sana. Biashara zote sasa haziteremshiwi Zanzibar, ni chache sana. Kwa hivyo, mapato ya Zanzibar yameanguka kiasi ambacho kuna hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu utafute timu maalum ikakae angalau wiki mbili, ichunguze meli zinazokuja, biashara zinazoteremshwa na pato linalopatikana. Hali ni nzito, hali ni ngumu. Huu muungano wetu unaendeshwa vizuri na tunasema kwamba matataizo madogo madogo inawezekana hamyaelewi, kwa hivyo, mimi nimesema kwa kupitia kwako, tuliseme hilo ili ilisimamie pamoja na Mheshimiwa Wazi wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuchangia, si kubwa sana ni suala la pongezi, na kwa nini nikasema muungano wetu unakwenda vizuri na lazima, tuuzidishe. Mimi kwa kupitia hotuba hii ya Waziri Mkuu naipongeza sana Ofisi ya Spika, kwamba hivi sasa imeshaonyesha hasa Muungano utadumu zaidi hata miaka 1,000 mbele. Kwa taarifa kwamba Ofisi ya Bunge, imeshakamilika na hivi karibuni itakwenda kufunguliwa, Mgeni Rasmi atakuwa nani atajua mwenyewe Mheshimiwa Spika, kwa sababu siku ile alitupa *briefing* kidogo. Lakini vile vile hapo hapo ilipojengwa ofisi hiyo ya Bunge, pamejengwa ofisi nyingine ya Uhamiaji ya Mkoa wangu wa Kusini na yote hii ipo katika Jimbo la Koani.

Kwa hiyo, vile vile naipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani, tena kwa njia ya pekee nampongeza sana Naibu Waziri kwa sababu naye alichangia sana kuhakikisha kwamba ofisi ile inajengwa pale na nimepata habari kwa Mheshimiwa Spika kwamba zote zitafunguliwa siku moja. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali, lakini inaambiwa haikufanya kitu, labda wao hawaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia suala la biashara ndogo ndogo, ambalo ningemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, hapa tulisika kulikuwa na semina hapa, tuliambiwa kwamba biashara ndogo ndogo kutoka Mipakani, Kenya na Uganda hawatozwi ushuru wowote. Lakini bado mwaka jana nilisema hapa na nasema leo kwa masikitiko makubwa na nilisema nikatoa mifano hapa kwamba, kama Mawaziri hawa watatu, Waziri wa Fedha na Manaibu wake wako maarufu waanajulikana pale bandarini Dar es

Salaam basi wageuze geuze nguo zao, wavae nguo nyingine ili wasijulikane. Huyu avae tarabushi, huyu avae kikoi, huyu avae hiki ili wapite pale.

Lakini mambo yale mpaka leo yanaendelea, wananyanyaswa kina mama pale, tena sasa hivi wakitoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar wanaombwa pesa, sijui za nini? Wakitoka Zanzibar wakileta bidhaa tena ndogo ndogo tu, visidiria, vikanzu vidogo vya watoto vinatozwa pesa. Ya nini mambo haya jamani na mambo haya yalishaondolewa

ushuru? Sasa sisi tunaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu hili suala ulisimamie kwa njia ya pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri wa Fedha tulitajiwa mambo mengi mle ya kuondoa umaskini na yale ambayo ndiyo hasa yanamlenga kila mmoja wetu. Yale ndiyo yanamlenga kila mtu kwa sababu tumeambiwa mambo ya MKUKUTA, tumeambiwa mambo ya MEM na mengine. Ninavyoelewa mimi hakuna Serikali hata moja ulimwengu huu ambayo inamjazia mtu hela ndani ya mifuko yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kazi yake ni kuangalia miundombinu katika maeneo ya Vijiji, Wilaya na Mikoa yote inakamilika. Sasa kama Serikali imefanya yale, mnatarajia ninyi kipi zaidi kingine kifanywe? Sasa mimi napongeza sana na ninaelewa kwamba madogo madogo yaliyobakia yatatekelezwa na yanatekelezeka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea katika utendaji wa Mawaziri wetu wa awamu hii iliyopita. Hakuna zuri lisilokuwa na dosari hata kidogo. Hata nyumbani kwako mwenyewe usitarajie siku zote ikiwa wewe baba utatengenezewa mazuri matupu au mama utatengenezewa mazuri matupu na mmeo. Kwa vyovyote vile kulikuwa na kasoro ndogo ndogo, lakini tusiondoke na dukuduku sasa hivi katika kipindi hiki kilichobaki kwamba labda Mawaziri wetu walikuwa na njama au hili na hili. Ndugu zetu wamefanya kazi nzuri, kama walivyopewa jina la askari wa miavuli na walishirikiana na sisi katika hali ya juu kabisa.

Mwisho kulikuwa na Kamati Maalumu hapa chini ya Mheshimiwa Semindu Pawa, ilikuwa inawatathmini Mawaziri kwa kila njia wanaosema kwa *speed* kuliko wote, Mheshimiwa Semindu Pawa alikuwa akiwajua, anaongoza Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Mheshimiwa Zakia Meghji, lakini Mawaziri wapole na wenye busara walikuwepo wakiongozwa na Mheshimiwa Gideon Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi lakini kulikuwa na Mawaziri wengine wakikaa pale tu zile mbwembwe zake za kujibu maswali basi watu wote wanashangilia akiongoza Mheshimiwa Bakari Mwapachu. Kwa hiyo, lazima tuwapongeze kwa sababu wametutumbukiza na sisi tutawaomba dua, Mwenyezi Mungu awajalie warejee katika nafasi zao za Ubunge tena, yale mengine siwezi kusema kitu lakini vya Ubunge nawaomba dua wote warejee. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. CHARLES H. KAGONJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii leo jioni ili nami niweze kuchangia machache katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu pia nichukue dakika chache kuwapa pole ndugu zangu wa Kilombero na familia ya Marehemu, Mheshimiwa Abu Kiwanga kwa kumpoteza Mbunge wao na namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa ndogo, nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa na Chama chetu kuibeba bendera ya Chama hiki kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuteuliwa na Chama chetu kuwa mgombea mwenza. Nimpongeze pia Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuteuliwa na Chama chetu kubeba bendera hiyo kugombea Urais kule Zanzibar. Wote nawatakia kila la kheri na naamini Mwenyezi Mungu atatoa baraka zake ili wapate kile ambacho wamekiomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli niweke kauli yangu ya kuwapongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Dr. William Shija na wale wengine sita ambao na wao walikuwa wanawania kuteuliwa na Chama chetu kugombea nafasi ile ya Urais lakini kwa bahati mbaya safari hii kura hazikutosha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa ujasiri wao, kwa upendo wao na kusema kweli kwa uadilifu wao. Sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wote ni wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa, tulishuhudia salaam mbalimbali za wageni walioalikwa pale Chimwaga. Yule kijana kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo alisema, somo hili ni la Mwalimu Nyerere tu na Watanzania mmefuzu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi nyingine kinyang'anyiro kama kile kikamalizika kila mtu anakwenda na kundi lake porini. Kwa kweli tumshukuru Mungu na tuienzi nchi yetu kwa fahari hii kubwa ambayo ametuteremshia ya upendo na mshikamano na huenda hii ni muhimu sana ndani ya Chama cha Mapinduzi, nawapongeza sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri Mkuu ni nzuri sana. Wote tulimsikiliza hapa wakati akiwasilisha, amezungumza kwa muda wa saa mbili na mwenyewe amesema ni hotuba ya miaka kumi na ni kweli na ushahidi wote unaonyesha hivyo. Mimi nitachangia machache kwa namna ya maswali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Waziri Mkuu atueleze na kutufafanulia kidogo, hivi leo hii tatizo la kuhamia Dodoma linasuasua kwa sababu gani? Kwa sababu ni vizuri Watanzania tueleze. Suala la kuhamia Dodoma ni sera ya Chama chetu na Serikali yetu ndio inatekeleza suala hili kila mwaka unapopita tunaambiwa Wizara mbili, mara Wizara moja, tatizo hasa ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule nyuma tulikuwa tunaambiwa Dodoma bado haijakaa vizuri. Tuliambiwa Dodoma hakuna nyumba, leo kuna majumba chungu mzima. Tuliambiwa hakuna maji, leo maji yanamwagika hovyoy mitaani, tuliambiwa hakuna umeme au hautoshelezi, leo umeme chungu mzima unamwagika na barabara safi, inatengenezwa kila siku.

Sasa pengine ni vizuri tuelezane sisi Watanzania na wanachama wa Chama cha Mapinduzi wenye sera, tatizo ni nini? Kwa nini hatuhamii Dodoma? Bunge kwa hiari yake yenyewe imehamia Dodoma Serikali bado inasuasua, kuna matatizo gani? Waziri Mkuu tafadhali tueleze, najua tunafikia kikomo lakini Serikali ijayo bado ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa hiyo Watanzania na wana CCM wanataka kuelezwa vizuri wafahamu tatizo hasa ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika pia kusoma katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati ule akisoma kwamba sasa Serikali inaanza kutekeleza wajibu wake wa msingi wa shughuli zake za Kiserikali. Nimefarijika sana kuona kwamba sasa Serikali inaanza kujiingiza katika kujenga nyumba za Mahakama na majengo mengine ya Serikali, kwa kweli hii ndio kazi ya msingi ya Serikali.

Naomba Serikali iendeleze juhudi hizo. Makao Makuu ya Wilaya kule ambako hayako yajengwe na Serikali, nyumba za Polisi kule ambako hakuna Makao Makuu ya Polisi yajengwe na Serikali na nyumba nyingine za Serikali mpaka kule chini vijijini zijengwe kwa jinsi tunavyopata uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifika pale Wilayani kwetu Lushoto ukiona lile jengo la Polisi Makao Makuu ya Wilaya kwa kweli utasikitika sana. Sina hakika kama Mawaziri wanaohusika waliwahi kufika katika jengo lile. Halitazamiki, ni kijengo cha Mjerumani la miaka hiyo. Kwa hiyo, nafikiri na namwomba Waziri anayehusika kwa kweli aandae utaratibu wa kujenga upya jengo lile kwa sababu hakuna kabisa Makao Makuu ya Polisi pale Lushoto. Kajengo ka Mjerumani ndio walikofikiria kawe Makao Makuu ya Polisi Tanganyika, leo hakafanani hata na sura ya nyumba ya mswahili tu. Naomba Serikali iendeleze jitihada hizi za kujenga nyumba za Serikali sehemu mbalimbali.

Kwanza siku hizi tumeingia kwenye huo mfumo wa vyama vingi, kwa mfano mwaka huu hata kule ambako tutapigia kura lazima majengo yawe ya Serikali kule ambako hakuna majengo ya Serikali basi yatakuwa majengo ya shule za msingi ndio ya Serikali. Kwa hiyo, nawaomba mjitahidi kufanya jambo hili na wananchi muwape nafuu kidogo kwa sababu wana kazi nyingi za kufanya. Wanachangia ujenzi wa shule za sekondari, sisi kule kwetu karibu tunafuta kwenye Kata zote sasa, wanachangia majengo ya Zahanati, wanachangia hata miradi ya maji, wanachangia hata Misikitini na Makanisani kwa hiyo, wapeni nafasi waendeleo na shughuli hizi nyingine muhimu lakini majengo ya Serikali wasichangie tena kujenga, Serikali ifanye kazi yake ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisoma pia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na amesisitiza masuala ya kilimo, umwagiliaji maji, mifugo, ameyasema vizuri sana katika kitabu chake hiki. Lakini pengine nimfahamishe tu Waziri Mkuu kwamba mimi ni miongoni mwa Wabunge wale wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi. Katika shughuli zetu za Kamati ile katika Wizara hizi tumegundua mambo kidogo ambayo hayaendi sawa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ni sera yetu ya kupeleka madaraka Mikoani, Wilayani na kule chini Vijijini. Tulishakubali, sera ilipitishwa na kazi hiyo imeshaanza na kuna programu hii ya kuimarisha Serikali za Mitaa. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu, maagizo mengi ya kitaalamu na maagizo mengi tu hata ya utafiti kutoka juu ya Wizara hayafiki kule chini kwa mkulima, hayafiki kule chini kwa mfugaji, hayafiki kule chini hata kwa masuala mengi tu yanayohusu ardhi. Sasa hapa tuna matatizo, kama ni tatizo la kisera naomba liangaliwe upya ili maelekezo yanayotoka Wizarani kwa wataalam yaweze kumkuta mkulima kule chini aliko lakini sasa hivi sivyo na hata Wizara hizi nina hakika hazina uwezo wa kupata *feedback* moja kwa moja kutoka kule chini kwa mkulima, *extension services* imekufa hakuna anayefuatilia, haya tunaita nini?

MBUNGE FULANI: Ugani!

MHE. CHARLES H. KAGONJI: Ndiyo huduma za Ugani hazifiki kule chini. Kwa hiyo, mipango mizuri ya Serikali, pesa nyingi zinazopelekwa kule chini basi hazina mwangalizi, sijui tufanyeje.

Mimi naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na kwamba tunaelekea kumaliza kipindi chetu lakini ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kuwepo kwa hiyo, jambo hili mliangalie, vinginevyo tutazungumzia kilimo, mifugo bora, maendeleo ya watu lakini hayapo kwa sababu kuna kizuizi hapa katikati. Sina hakika tutafanyaje na hawa Wakurugenzi maana wengine inaelekea hawana hamu hata na kilimo na mambo ya mifugo. Kwa hiyo, hapa kuna tatizo kubwa tumeliona na naona kama ni la kisera tafadhali litupiwe macho vinginevyo tutakuwa tunaimba wimbo ambao hauna mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pia kusoma na kumsikiliza Waziri Mkuu katika kitabu chake akizungumzia suala la amani na mshikamano wa Kitaifa. Hili ni jambo muhimu sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu umelizungumzia kwa nguvu zote na uhodari wako wote. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna mambo mengine yanajitokeza hapa katikati, mimi nadhani Serikali iyakemee kwa nguvu kwa sababu ukiacha jambo kidogo kidogo halishughulikiwi baadaye inakuwa mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kujitokeza kwa vikundi vya kijamii na vikundi vingine vya kidini hadharani kabisa vikizungumzia masuala ya siasa hadharani kabisa vikundi vinatoa wito kwamba msikichague Chama cha Mapinduzi, hakifai, sasa tunakwenda wapi? Kama hivi vikundi vimejiingiza kwenye siasa basi viruhusuni vikaandikishwe na Msajili wa Vyama viwe Vyama vya Siasa na visiwe vyama vya kijamii au vya kidini tujue kwamba tunazungumza na wanasiasa wenzetu, mambo haya tusiyaachie kidogo kidogo tunaingia kwenye matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili sasa wametokea wanasiasa bila woga, wala aibu wanazungumzia dini yangu ni bora kuliko ya huyu. Leo hii wanasiasa wanazungumzia kabila langu ni bora kuliko la huyu. Nina hakika Serikali mnajua, nina hakika Chama chetu kinajua na wala sio vyama vingine hata CCM inafanyika hiyo.

Mimi naomba haya myaangalie. Najua Watanzania hawashawishiki sana na mambo haya leo lakini kiongozi mzito wa aina yetu sisi tukitoka nje tukiyahubiri mambo haya kwa watu wataamini na mwisho mtasikia watu wanaanza kumalizana, sio jambo zuri. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo hili mliangalie vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho katika amani hiyo na mshikamano wa Kitaifa, nimesoma kitabu cha Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, cha Mheshimiwa Basil Mramba na hata kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu sijaona mipango mizuri ya maandalizi ya vijana. Wote tumekubaliana kwamba vijana ni Jeshi kubwa sana katika Taifa hili. Tumekubaliana kwamba Jeshi hili lisipoangaliwa vizuri tunaweza kuwa tumekalia bomu. Kwa nini nasema hivyo? Hata bila hesabu ya msingi tu sasa hivi inaonekana waziwazi walionacho wanazidi kuwa nacho, wale wasionacho hata kile kidogo walichonacho kinazidi kupungua na kwa bahati mbaya wale wasionacho ni wale vijana tunaosema ni Jeshi. Wala sisemi hawa walionacho wamekipata kwa njia tofauti au mbaya, hapana. Inawezekana ni njia halali lakini sisi zamani tulizoea sera tofauti kabisa lakini sasa tumeingia kwenye utaratibu huu. Sasa walioko karibu na sera za sasa ndio wanaweza kujiongezea zaidi na kupata zaidi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, jeshi la vijana kama halikuandaliwa utaratibu maalum wa namna ya kupata maisha yao na kutegemea nguvu zao wakafanyiwa mipango mizuri, tuna nchi kubwa tunasema walitakiwa wafanyiwe mipango ya kilimo, wapewe matrekta, wawekwe mahali waangaliwe, wafanye kazi hiyo ili waweze kujitegemea vinginevyo hili jeshi litakuwa matatizo na ni hatari kwa usalama wa Taifa letu.

Naomba tafadhali waangaliwe. Sasa hivi wamejaa mijini Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, kwa nini? Vijijini hapakaliki. Naomba tujitahidi pia kuboresha miundombinu vijijini, umeme, simu vijana wengi watapunguza kasi ya kwenda mijini lakini kama hatukuangalia jeshi hili, Mheshimiwa Waziri Mkuu nina mashaka kabisa kwamba mbele ya safari tutapata matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie moja au mawili hivi ya Jimboni kwangu. Juzi niliuliza swali hapa Bungeni linahusu barabara za Jimbo langu. Nilijibiwa na Serikali vizuri kabisa na ni kweli kwamba Serikali inajitahidi sana kuziangalia barabara za nchi hii hata zile za kule kwangu. Lakini zile za kwangu nilisema zilipata ajali mara mbili, mafuriko makubwa na maporomoko ya milima ile, zile barabara za changarawe karibu nusu ya changarawe ikaondoka halafu zikaja mvua ndefu sana za *El-nino* nazo zikasaidia kuharibu barabara zile.

Kwa hiyo, kwa sehemu kubwa barabara zile ambazo zilikuwa za changarawe kamili sasa ni za mchanga na nilisema hapa kwamba wakati ukiwadia hali ikiwa nzuri barabara hizi zirudishiwe changarawe ili sizije zikarudi kuwa za mchanga kabisa badala ya kujali barabara mpya zikawekwa changarawe hizi za zamani tusizisahau ndio wito wangu kwa Serikali. Barabara ya kijijini inayoweza kupitisha magari 150 kutwa sio barabara ya kawaida tena magari ya mizigo. Mimi naomba Serikali ifikirie suala hilo ili barabara zile ziweze kurudia katika hali yake ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, umeme. Tumelalamikia umeme kwa muda mrefu na nashukuru kwamba chombo hiki sasa cha kueneza umeme vijijini kitaanza hivi karibuni. Naomba Serikali iangalie yale maeneo ambayo tulikuwa tunalalamikia ambayo kwa kweli watu wamejitahidi kufikia *standard* ya juu ya maisha lakini hawawezi kutoka pale walipo kwa sababu hawana umeme. Kwenye Jimbo langu nimetaja Kata ya Rangwi, Sunga, Mtae, Mnazi na pale Mng'aro wapatiwe umeme kwa sababu kuna viwanda vya mbao, mashine za kusaga na kadhalika. Naomba wakati ukifika, nashukuru kumuona Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, yupo karibu, tafadhali nisikilize ulifika sehemu zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni *TVT*. *TVT* ni Televisheni ya Taifa bado haionekani sehemu kubwa ya nchi hii hata kule kwangu napata taabu sana ya kuiona, matatizo ni nini? Mbona hizi za watu binafsi wala hazijengwi kwa gharama kubwa sana zinaonekana kila mahali, tatizo ni nini? Tunaomba mtusaidie na sisi tufaidike kama wenzetu walio karibu na stesheni hiyo. *(Makofi)*

Lakini la pili muwaangalie watumishi wake. Hivi vyombo vya kisasa vina utamaduni wake, mtu anatakiwa atangaze taarifa ya habari amevaa suti yake safi au gauni lake safi, hawa wa *TVT* siwaoni vile! Wapeni posho ya mavazi ili waweze kushindana na wengine, wapeni mishahara mizuri ili waweze kushindana na wengine, wapeni *promotion* ili waweze kushindana na wengine. Chombo hiki ni cha maana, cha manufaa kwa ajili ya kuelimisha na kwa kiwango kikubwa kinaelimisha lakini mkiwaacha kama cha Serikali hivi hivi watu wataendelea kukimbilia vyombo vya binafsi halafu tutakuwa tumepoteza pesa zetu bure wala elimu tuliyotaka iwafikie wananchi haitafika.

Naomba Waziri Mkuu ukiangalie chombo hiki, wanasononeka hawa, ukiangalia *TVT* na *ITV* wakati wa matangazo tofauti unaiona wazi wazi hawa wengine wamevaa kienyeji tu nguo za nyumbani na haipendezi. Naomba chombo hiki kifike mbali, uchumi wa nchi unaboreka basi tunataka watu wetu wafaidike kwa elimu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

MHE. BEATUS R. MAGAYANE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Awali ya yote, naomba niungane na Wabunge wenzangu kwa kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga aliyekuwa Mbunge wa Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie fursa hii kuwapongeza wale wote ambao wameteuliwa na Chama cha Mapinduzi kushika bendera ya chama hicho katika uchaguzi ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa leo asubuhi. Kwa kweli hotuba hiyo ni ripoti ya kazi ya miaka kumi ambayo amekaa madaraka. Kwa namna ya pekee, nampongeza kwa jinsi

ambavyo ameaminiwa na Mheshimiwa Rais kwa kumteua kuwa Waziri Mkuu kwa vipindi viwili na sisi kama Wabunge tukathibitisha uteuzi huo, nampongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba nichangie mambo mawili, matatu. Kwanza, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Waziri Mkuu anaposema kwamba sasa ajira imekumbwa na utandawazi na kutushauri kwamba vijana wetu, wataalam wetu wathubutu na wao kuomba kazi katika nchi za wenzetu hasa za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maudhui mazima ya suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tufike mahali tukubali kwamba pamoja na kuthubutu kwenda kutafuta kazi kwa wenzetu ni vema Serikali ikawa na mipango ya makusudi kabisa ya kulinda kazi za humu nchini mahususi ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania tu na sio kila kazi iweze kuja kufanywa na wageni watakaokuja. Hii ni muhimu ukizingatia hata uzalendo wenyewe, lakini pia ni muhimu kwamba kwa kuzingatia tofauti ya elimu iliyowekwa na historia inawezekana kabisa vijana wetu wasiweze kushindana katika soko la ajira kama hatutakuwa tumelinda ajira zetu tunaweza kukuta ajira nyingi na muhimu zimechukuliwa na watu wa nje. Ni vema basi tukaweka utaratibu wa kuweza kulinda hizi ajira ambazo ni *specific* kwa ajili ya Watanzania wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira nazo zimekumbwa na matatizo kama Mheshimiwa Charles Kagonji alivyosema kuna tofauti kubwa sana ya vipato sasa inanza kujitokeza na hii tofauti ya vipato imepelekea kuwe na tofauti katika mifumo ya elimu na tukishakuwa na tofauti katika mifumo ya elimu tunajikuta tena tuna tofauti katika ajira. Ukichunguza hivi sasa wale ambao wana nafasi ndio wamepata elimu bora na ndio wamepata nafasi nzuri sana katika Mashirika yaliyobinafsishwa na Mashirika ambayo yamekuja kuwekeza katika nchi yetu. Hili ni lazima kabisa Serikali tulielewe, tulitambue tujue namna ya kuboresha elimu ili vijana wetu tunaowaandaa waweze kushindana katika soko la ajira lakini tuweze kuondoa hizi tofauti za wazi ambazo hivi sasa zinajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti iliyotolewa ni nzuri lakini nina wasi wasi hasa kufuatana na bei ya mafuta ambavyo inapanda siku hadi siku. Kama hatutadhibiti mfumuko wa bei ya mafuta tunaweza kujikuta kabisa Bajeti hii ikasambaratika. Kwa kuwa tuna chombo kinachodhibiti, nafikiri tulikipitisha hapa *EWURA*, naomba chombo hiki kianze kufanya kazi kama Tume ya Mawasiliano hivi sasa inavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,, kama wao wameweza kuainisha na kufikia viwango vya maingiliano vya mitandao hii hivi inashindikana nini hiki chombo cha *energy and utilities (EWURA)* kupanga bei ya chini au ya kuanzia kwa mlaji kwa nishani hasa kwa mafuta ya dizeli na petroli? Kama tusipofanya hivi, mipango yetu yote tunaweza kukuta haifanyi kazi vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie suala la UKIMWI. Nadhani hivi sasa elimu imeshaenea hasa kwa mjini watu wanajua chanzo cha UKIMWI na namna ya kujikinga. Naiomba Serikali sasa ielekeze juhudi zake vijijini kuwalinda ambako wengi bado hawajaambukizwa ili elimu hii ambayo wenzetu wa mjini wameweza kuipata kwa

sababu wana vyombo vya habari hasa televisheni iweze kufika vijijini ambako wanaweza kuokoa maisha ya walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa dawa zinazoitwa za kurefusha maisha kana kwamba tunajua maisha ya mtu ni miaka mingapi, zimeanza kutolewa lakini bahati mbaya zinatolewa kwa walio wachache kwa watu 400,000 katika ya watu 2,500,000 walioathirika. Ni vema hii huduma ikaandamana na elimu juu ya matumizi sahihi ya dawa hizi kwa sababu hivi sasa hizi dawa watu wengi wameanza kuzitumia kama kinga dhidi ya UKIMWI na wengi wanazipata kwa njia zisizo za kawaida na hii ni hatari. Utoaji wa dawa hizi au upatikanaji wa dawa hizi uandamane kwa kweli na elimu sahihi ya jinsi ya kuzitumia. Kazi iliyokwihafanyika ni nzuri lakini ni vema kwanza ikatolewa elimu lakini pia zikasogezwa karibu na wale ambao ni walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza juu ya kuondoa umaskini, juu ya MKUKUTA na MKURABITA lakini naomba nizungumzie suala moja. Kama hatuwezi kufungua nchi yetu hii kwa barabara na miundombinu mingine na tukalenga katika barabara ambazo zinaifunua nchi na kuiweka wazi kwenye njia za uchumi, tutakuwa bado hatujafanya kazi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha jana ametueleza mikakati waliyonayo, ni mikakati ambayo kwa kiwango kikubwa au chote inategemea sana pesa kutoka nje sijui ni kwa kiwango gani tunaweza kujihakikishia kwamba hizo pesa tutakuwa tumezipata. Lakini ni vema tukaziangalia hizi *corridor*. Tumeanza *SDIs* kuendeleza *corridors* hizi naomba kwa makusudi kabisa *corridor* ya Kanda ya Kati ambayo inaenda mpaka Kigoma itiliwe mkazo ili tuweze kuunganisha Tabora kwa barabara na Mkoa wa Kigoma walau Makao Makuu ya Mkoa wa Kigoma. Lakini pia barabara ya kutoka Nyakanazi kuja Kigoma imekuwa inazungumzwa kwa muda mrefu sana na chini ya *NEPAD* imepewa kipaumbele namba moja kwa miaka mitatu mfululizo lakini hakuna ambacho kimekwihafanyika.

Naomba Serikali hivi sasa hasa kwa kutumia unafuu tutakaoupata kwa kusamehewa madeni barabara ya Nyakanazi-Kigoma na barabara ya Tabora-Kigoma ipewe umuhimu wa namna ya pekee kwa sababu sio tu kwamba tutakuwa tumefungua Mkoa wa Kigoma tutakuwa tumefungua biashara na nchi za jirani za Rwanda, Burundi na Kongo, hii ndio njia pekee ambayo tunaweza kufungua uchumi wetu. Wala tusizungumzie Mkoa wa Kigoma tuiangalie kwa upana zaidi kama ni uchumi wa kijiografia tutakuwa tumeupata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu mingine muhimu kwa Mkoa wa Kigoma ni umeme. Nakumbuka kabisa Mheshimiwa Waziri kila siku anatuahidi. Kwa kweli sisi watu wa Kigoma inatusikitisha tunapopitisha Muswada wa kuanzisha chombo cha kupeleka umeme vijijini wakati Makao Makuu ya Mkoa hatujawa na umeme. Kwa kweli inatusikitisha na Mkoa wa Kigoma hatuwezi kuendelea, naona Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha anacheka, kama hatutakuwa na umeme wa uhakika. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupeleka umeme Kigoma hapa walituambia ni dola milioni 34. Lakini ukiangalia *context* ya Mkoa wa Kigoma kuwa na umeme

tusizungumzie Mkoa wa Kigoma tuone kwamba tuna-*tap* uchumi wa nchi jirani, hiki ndicho cha msingi. tukiangalia Kigoma kama Kigoma inawezekana tusione umuhimu lakini Kigoma tunakuwa tunazungumzia na *potential* nyingine ambayo iko katika nchi jirani, hapo ndipo tunapoweza kuona kwamba dola milioni 34 sio pesa, si lolote katika maendeleo na maendeleo yana gharama yake lazima tukubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie Vyama vya Siasa. Mengi yamezungumzwa sitaki kuyarudia lakini kinachojitokeza inaonekana kwamba kuna tatizo la ukomavu wa vyama vya siasa vyote kwa ujumla ikiwemo CCM kwa maana ya utaratibu mzima wa jinsi tunavyotakiwa kuendesha siasa. Zamani tulikuwa na Vyuo vya Chama kama vile Kivukoni na matawi mengine na pale tulikuwa tunawatoa watu tunaowaita makada wa chama, leo hii vyuo hivi havipo na leo tunaanza kupata watu ambao hawaelekei katika mfumo wa siasa kama siasa inavyotakiwa kwa sababu siasa ni taaluma, siasa ni fani ya peke yake na lazima ujifunze, huwezi kuipata tu mitaani kama wengi tunavyowaona kwamba mtu amefukuzwa kazi Serikalini anaingia upinzani, haiwezekani huyu akawa ni mwanasiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba kwa makusudi kabisa mimi naiomba Serikali irudie utaratibu wa kuanzisha chuo cha siasa cha kufundisha wanasiasa wakiwemo wa vyama vya upinzani ili wajue wanaelekea wapi kisiasa. Lakini zaidi kwenye hicho chuo tufundesheuzalendo kwa sababu tatizo kubwa tulilionalo hata hizi vurugu ambazo zinatokea ni kwamba watu hawana uzalendo wa nchi yao, hawana uzalendo na kule wanakoelekea.

Kwa kweli hawa wenzetu wanaoitwa *Partners in Development*, wanaotusaidia, badala ya kutoa pesa za semina wanazotoa kwa Vyama vya Siasa, watusaidie kuanzisha Chuo cha Siasa ili hao wanaojiita wanasiasa wafundishwe siasa, akina Mheshimwa Aggrey Mwanri wako wakawafundishe, wawafundishe uzalendo, kwa sababu tatizo kubwa tunaloliona ni uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naishukuru Serikali kwa maendeleo ambayo wamefanya katika Jimbo la Buyungu. Lakini naomba kama Serikali itasema ikubali kwamba kutakuwa na barabara za Ulinzi na Usalama katika Majimbo na Mikoa ya mipakani. Ningeomba barabara ya kutoka Bitale kupita Bukililo kwenda Lumashi mpaka Mlusagamba - Ngara, ili hii barabara ipewe umuhimu wa pekee kwa sababu barabara hii iko kwenye *hub* na ni muhimu katika masuala ya Ulinzi na Usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukitokea tatizo lolote, ni vyema tukawa na barabara ambayo inaweza kuaminika na vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vikaweza kwenda kukabili matukio yanayoweza kuwa yametokea hapo Mpakani. Naomba Serikali ilizingatie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kwa kuwa ni Sera ya Serikali kwamba kila Tarafa iwe na Kituo cha Afya na Serikali katika kujibu swali langu iliahidi kwamba wataanza kujenga kituo cha Afya katika Tarafa ya Kasanga, naomba basi kama ilivyoahidi kwamba wataanza kujenga katika mwaka huu wa Fedha 2005/2006 na

kwamba shilingi milioni 60 zimeandaliwa basi Kituo cha Afya katika Tarafa ya Kasanga kiweze kuanza kazi mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib.

MHE. HASSAN RAJAB KHATIB: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu, kwa kumpongeza Waziri Mkuu, Mawaziri wake wote wawili, Ndugu yangu Mheshimiwa William Lukuvi na Ndugu yangu Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, wataalam wote katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuandaa hotuba nzuri sana yenye mwelekeo mzuri kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii imezungumzia shughuli zote za maendeleo zilizofanyika kwa kipindi chote cha miaka 10 ambayo mtu yeyote ambaye akisikia hotuba hiyo, mimi nafikiri hakuna mazungumzo mengine yoyote, isipokuwa jambo kubwa kuiunga mkono tu na mimi kuanzia sasa nasema naiunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Ndugu yangu Damian Foka. Ndugu Damian Foka kwa kipindi kifupi ambacho amekuwa Katibu wa Bunge, kaonyesha uimara wake wa utekelezaji wa majukumu yake katika Ofisi ya Bunge. Ndugu yangu Foka, karibu sana na endelea na sisi tuko pamoja na wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii tena kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu. Naipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu kwa namna ilivyotekeleza Sera na Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Nampongeza Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Waziri Mkuu na Mawaziri wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya kuitumikia nchi hii.

Mimi nafikiri Chama cha Mapinduzi hakina kazi kesho kutwa. Chama cha Mapinduzi hakina kazi hata kidogo, mtu yeyote ambaye ameona hali ya maendeleo na shughuli zilizofanywa ndani ya nchi hii, basi bila wasiwasi wowote Chama chama Mapinduzi kitachukua ushindi wa vishindo na siyo ushindi wa vishindo tu bali nasema ushindi wa *Tsunami*. *(Makofi)*

Wale ambao walikuwa hawaoni, tuwaache kama walivyo, wale ambao walikuwa hawasikii, maana unaweza kuwa huoni basi hata kusikia hata husikii basi tumwache kama alivyo. Kwa hiyo, mimi nasema tuwapongeze sana. Lakini pia niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jinsi walivyoisimamia Serikali kwa ukamilifu kabisa kufika hapa tulipo. Mimi nawaombea kwamba hiki ni kipindi chetu cha lala salama basi nawaombea wote kwa imani na idhini ya Mwenyezi Mungu, tutarudi sote hapa Bungeni, *Inshallah*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika hali ya uchumi Tanzania. Nilimsikiliza sana Waziri wa Fedha alipoitoa Bajeti yake yenye matumaini, yenye mwelekeo mzuri, yenye kutia imani kwa Watanzania kwamba Bajeti hii ni Bajeti yenye mwelekeo ya wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli, makusanyo yaliyokuwa yanakusanywa ni makusanyo makubwa kabisa. Tuwapongeze ndugu zetu wa *TRA* kazi nzuri walizozifanya na tuipongeze Wizara kwa ujumla namna ilivyosimamia makusanyo mpaka yakafika hapo yalipofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo yaliyokusanywa ni makubwa na yanatia moyo kwa kukusanya kwamba kila mwezi kukusanya bilioni mia moja na kitu, si kitu cha mchezo, hicho ni kitu cha kupongeza sana. Utaratibu uliowekwa mpaka ukafikia hapo ndio lazima tuwasifu sana Wizara hii ikiongozwa na mwenyewe Waziri wa Fedha Ndugu yangu Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba. Hongera sana Ndugu yangu Basil Pesambili Mramba, lakini nina ombi rasmi na hilo lisikilizwe vizuri sana. Waziri Mkuu nataka ulisikilize vizuri sana vizuri ombi hilo, Waziri wa Fedha upo, unisikilize vizuri sana ombi hilo, wataalam wako wa uchumi wanisikilize vizuri sana ombi langu hilo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi tunajua kwamba Tanzania ni moja, inaongozwa na Chama cha Mapinduzi na Tanzania tunajua tuna nchi moja lakini ina Serikali mbili, lakini inaongozwa na Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uchumi Zanzibar iko hali mbaya sana, sana, sana! Wala tuiseme kwamba hali yetu tumeishakuwa nzuri Tanzania Bara tukasema tumeibuka, bado. Haiwezekani kwamba wewe unashiba na ndugu yako ana njaa, si kitu kizuri wala si uungwana wetu Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha, ninachokiomba, tutazame kitu gani kinachosababisha kupungua kwa uchumi Zanzibar. Tuone wenzetu nini kinachowasumbua. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mkae mtizame, wataalam wetu watizame kitu gani kinachokuwa kinateremsha uchumi siku hadi siku, ni nini! Hali ya Uchumi Zanzibar ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale Bandarini utashangaa, utafikiri siyo Bandari. Watu hawana kazi, bidhaa haziingii, Meli haziingii, tatizo ni nini? Lakini mimi ninachoshauri, labda kutokana na utaratibu wetu wa namna ya kubadilisha utaratibu wetu wa kodi nafikiri moja katika *source* ambayo iliwatia *damage* Zanzibar. Sasa utaratibu wetu wa kodi ni lazima tuangalie vizuri zaidi. Kuna sehemu moja ambayo imeinuka na kuna sehemu nyingine imeporomoka, tuliangalie hili, wala hili tusilifumbie macho.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili si jambo la mchezo wala si la mzaha. Sisi sote kijiti chetu kimoja cha CCM. Ilani yetu ni moja, safari yetu ni moja, mwendo wetu ni mmoja, kesho kutwa tutakwenda pamoja, tuwe na kijiti kimoja, lazima twende sawa sawa.

Wakati ilipopata Uhuru nchi hii mwaka 1961, Mwalimu hakuridhika akaona kwamba Kenya haijapata Uhuru na Uganda haijapata Uhuru, akaona bado sijajitawala vizuri. Sasa na sisi tuna mwendo huo, tuiseme kwamba sisi hali yetu ya uchumi imeinuka, kubwa, lakini sehemu ya uchumi wa upande wa pili ni mbaya. Nafikiri siyo sahihi hata kidogo, hili lazima tuliangalie kwa undani kabisa, tuiseme hapa hili si letu, hapana hili ni letu Watanzania, hili ni letu kabisa.

Mimi nafikiri kuna *plug* kidogo imeweka Tanzania Bara ngumu kidogo na ndio maana *drop* ya uchumi wa Tanzania Zanzibar ume-*drop*, hili liangaliwe. *Plug* hiyo ichomolewe, iko *plug* imechomekwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *plug* ipo imechomekwa, iondolewe, Zanzibar nao waibuke na uchumi wao, waendeshe Serikali yao, waende vizuri katika kuinua uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningewaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kabla hatujamaliza, hatuja ng'atuka, suala hili liwe limepatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili liwe limepatiwa ufumbuzi, tujue kuna nini, kulikoni? Tuanajua uchumi wetu ni mmoja, *tariff* yetu ni moja, lakini upande wa pili umeathirika na *tariff* hiyo. Kwa hiyo, tutizame kitu gani kilichokuwa kimefanya athari hiyo, tukiangalie kwa undani na kitaalam kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo lilikuwa ni ombi kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninalotaka kuzungumza, niishukuru sana *TASAF*. *TASAF* ni ukombozi kweli wa wanyonge. *TASAF* imefanya kazi vizuri sana katika Vijiji mbalimbali, Wilaya mbalimbali hasa Zanzibar. Mimi nashukuru na mimi Jimboni kwangu nimepata hiyo *TASAF*. Tulikuwa na matatizo makubwa ya maji katika Shehia ya Amani, sasa hivi wananchi wa Jimbo la Amani wanatoa pongezi sana kwa *TASAF* iendelee vizuri zaidi. Lakini tatizo sasa *TASAF* inakwenda vizuri lakini urasimu wake unakuwa ni mkubwa. Sasa ningeshauri kwamba ili twende vizuri na lile lengo lililokusudiwa liende vijijini basi urasimu kidogo upungue. Ukishapungua tunajua maendeleo yatakwenda haraka haraka kabisa, hiyo ni moja katika ukombozi wa wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumza, Kamati yangu ya Maliasili na Mazingira ilifika Kigoma. Ilipofika Kigoma bahati nzuri ilitembelea sehemu za wakimbizi. Inavyoonyesha wakimbizi wale si rahisi kuhama katika nchi hii. Isitoshe, tulipofika kule tuligundua kwamba sehemu kubwa imeathirika sana na mazingira hasa ukataji wa miti, eneo kubwa sana limeathirika katika sehemu ile. Sasa katika sehemu ya Kigoma, ningeiomba Serikali, watu wale ingewatafutia mbinu yoyote nayo ikawatizama kwa jicho la huruma angalau wakasaidiwa pembejeo mbali mbali wakarudisha miti ile katika sehemu ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho ni kitu muhimu sana, wale wakimbizi ni kwa mujibu wa sheria ni lazima tuwapokee na si wao watu wa Kigoma tu lakini wale ni wakimbizi wetu Tanzania nzima. Sasa ningeshauri kwamba suala la wenzetu wale walioathirika na wakimbizi basi kidogo wakasaidiwa, wakajisikia kwamba na wao wamo ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninataka kuzungumza ni habari ya Vyombo vya Habari. Nawapongeza sana watu wa vyombo vya habari kwa kazi zao nzuri sana wanazozifanya. Niipongeze hasa *Radio Tanzania*. *Radio Tanzania* imejitahidi kabisa kufanya wajibu wake wa kuelimisha jamii katika nchi hii. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wa kuahirisha Bunge umefika, kwa hiyo, sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa
Tarehe 17 Juni, 2005 saa tatu asuhuhi)*